

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

#### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Arobaini na Mbili - Tarehe 27 Juni, 2014**

(Mkutano Ulianiza Saa Tatuh Asubuhi)

#### D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu tuendelee!

#### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, atakaeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Esther Bulaya.

Na. 317

#### Kutengeneza Jokofu la Kuhifadhia Maiti – Bunda

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Jokofu la kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Bunda limeharibika kwa muda mrefu na kupelekea Wananchi kuhifadhi maiti Mwanza na Musoma kwa ghamra kubwa.

Je, Serikali itatatua lini adha hii kwa wakazi wa Bunda na Mwibara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)**  
aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Jokofu la kuhifadhia Maiti katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Bunda (DDH) liliharibika hivyo kusababisha Wananchi kuhifadhi maiti Mwanza na Musoma. Tatizo lilikuwa ni kuziba kwa bomba (pipe) linalopitisha gesi kutoka kwenye compressor na kusababisha bomba hilo kupasuka na kuruhusu gesi kutoka. Aidha, kulikuwa na tatizo la umeme katika jengo hilo la kuhifadhia maiti.

Mheshimiwa Spika, Jokofu hili lilishindwa kufua baridi kiasi cha kushindwa kuhifadhi Maiti mnamo tarehe 20 Aprili, 2014. Hata hivyo, Jokofu hilo limeishafanyiwa matengenezo na limeanza kufanya kazi toka tarehe 5 Mei, 2014. Hadi muda huu sehemu zote Sita za kuhifadhia maiti zinafanya kazi kwa ufasaha.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ninaishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kushughulikia tatizo hilo, lakini nina maswali mawimi ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mbali na hospitali ya DDH mahitaji ya Wilaya ya Bunda ni kituo cha afya cha Manyamanyama kuwa Hospitali ya Wilaya, mwaka 2006 Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi kutaka hospitali ile iwe ya Wilaya lakini mpaka sasa hivi bado Wizara haija- confirm kwamba ile iweze kuwa hospitali ya Wilaya.

Swali la pili, katika mchakato huo huo wa kuhakikisha kituo cha afya cha Manyamanyama kinakuwa hospitali ya Wilaya, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi mbalimbali ikiwemo kutengeneza chumba cha kuhifadhi maiti pamoja na X- Ray na mashine ya Ultra Sound. Sasa ni muda mrefu umepita na hospitali ile inatoa huduma si kwa wilaya ya Bunda tu, bali hata Musoma Vijiji pamoja na mkoa jirani wa Simiyu.

Nilitaka kujua ahadi hii itatekelezwa lini ili huduma hiyo iwanufaishe wananchi wa wilaya ya Bunda pamoja na mikoa ya jirani? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninataka nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu katika jambo hili amekuwa na ufuatiliaji wa karibu sana. Pia ninataka nimhakikishie kwamba, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuifanya hospitali hiyo kuwa ya Wilaya na ambapo tayari ameweka jiwe la msingi, inaendelea na kazi zinazoendelea sasa ni kuhakikisha kwamba, huduma zote zinaratibiwa vizuri ili hospitali ya Wilaya inapoanza inaanza kazi mara moja.

Kwa mfano sasa tumeanza kuwapunguza Watumishi tuliokuwa tumewapeleka kwenye hospitali tuliyokuwa tumeifanya DDH kuwarudisha huku na pale tumeacha watumishi 37 ili sasa kuwaweka watumishi wanaotosha hasa kwa yale madaraja yao; kuwa na Madaktari, Manesi na Wahudumu wa kawaida ili sasa tunapoanza tuanze mara moja.

Mheshimiwa Spika, suala la ahadi mbalimbali za uwekaji wa vifaa mbalimbali kwenye hospitali hii, jambo hili limefikishwa pia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambapo Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tunafanya kazi kwa pamoja na hasa kwenye maeneo ambayo yamepewa hadhi ya hospitali ya Wilaya na Mkoaa.

Kuhusiana na X-ray, sasa hivi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imesitisha kutumia X-ray zote za analogy, inataka zitumike za digital na sasa zabuni imeishatangazwa na Wizara ya Afya, pindi watakapopatikana wakati wanasambaza itakuwa ni pamoja na Manyamanyama ambapo pia watapata mgao huu kikiwemo chombo kinachoitwa ultra sound. (Makofii)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na matumaini na wananchi wa eneo lile wapate matumaini kwamba, huduma hizi zitakamilika na hospitali itaanza na hadhi yake mara moja.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo la majokofu liko katika hospitali nyingi za Wilaya karibu nchi nzima, lini sasa Serikali itajenga Majokofu ya kuhifadhi maiti katika hospitali zote za Wilaya hasa katika Hospitali Teule ya Namanyere ambayo ina hali ngumu na haina Jokofu? Wananchi wengi wanategemea hiyo hospitali na vifo vingi vinatokea pale kutokana na ajali za magari na wengine kufia kwenye maji.

**SPIKA:** Inatosha, majokofu ni ya maiti ndiyo hoja, amekufaje siyo hoja. (Makofi/Kicheko)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Keissy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majokofu ninayozungumza hapa ni yale ya maiti, na kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la swali la nyongeza la Mheshimiwa Bulaya, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imeendelea na utangazaji wa zabuni za mashine hizi ambazo zinasaidia sana katika kuendesha hospitali ikiwemo na ile ya Namanyere.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, jambo hili liko kwenye hospitali zote nchini zenye matatizo ya majokofu ya kutunzia maiti, lakini pamoja na mitambo ya X-ray na Ultra sound ambazo ni muhimu zaidi katika utoaji wa huduma kwenye hospitali zenye hadhi ya ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, awe na matumaini kwamba moja ya maeneo ambayo yameangaliwa zaidi ni pamoja na Namanyere.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hospitali yetu ya Mkoa wa Kilimanjaro ina Majokofu Sita na kiti ya hayo ni moja tu linalofanya kazi na kusababisha maiti kutokehifadhiwa vizuri.

Je, Serikali ina mpango wowote wa kuhakikisha majokofu haya yanafanya kazi kwa haraka ili Maiti ziweze kuhifadhiwa?

**SPIKA:** Siyo Hospitali ya Mawenzi? (Makofi/Kicheko)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Kiwelu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hospitali hii imezungumzwa mara nyingi na tunazo taarifa za kuharibika kwa mitambo hii kati ya hayo Sita limebaki moja, ninataka kumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutafanya ufuutiliaji wa karibu kujua mamlaka tulioipa dhamana ya kufanya uratibu wa pale hospitali wamefikia hatua gani ili sasa tuweze kushirikisha Wizara tuweze kutoa huduma hiyo kwa Wananchi wanaopata huduma eneo lile. (Makofi)

**SPIKA:** Katika Kanuni zetu Viti Maalum hakuna mkoa, naomba tuelewane hapo. Katika Kauni zetu Viti Maalum vinaitwa Viti Maalum hakuna mkoa wowote, utaratibu wa mikoa ni ya vyama vyama huku, lakini humu ndani ni Viti Maalum.

Kwa hiyo, ninaomba, maana nimesikia Bulaya ni Viti Maalum Mara, siyo ni Viti Maalum tu. Tunaendelea, Mheshimiwa Margareth Mkanga.

**Posho ya Shilingi Laki Tano (500,000/=) kwa Walimu wa Maeneo ya Mazingira Magumu**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali ilieleza kuwa itatoa posho ya Shilingi Laki Tano (500,000/=) kwa Walimu wanaofundisha katika maeneo yenyé mazingira magumu.

Je, ni lini maelezo hayo yatakelezwa kwa vitendo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)**  
aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari kwa kushirikiana na Benki ya Dunia mwaka 2010/2011 ilipanga kulipa posho ya mazingira magumu ya shilingi 500,000.00 kwa mara moja kwa Walimu 3000 wa ajira mpya wa Shule za Sekondari ambao wange pangwa katika mazingira magumu.

Mpango huu ulionekana kuwa na mapungufu kadhaa ikiwemo; kuwabagua Walimu wa Sekondari na Watumishi wengine wanaofanya kazi katika maeneo hayo wakiwemo Walimu wa Sekondari wa zamani, Walimu wa Shule za Msingi, Watumishi wa Afya, Kilimo na Watendaji wengine. Aidha, Mwalimu aliyelipwa posho hiyo anapohama changamoto ya ugumu wa mazingira huwa inaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Serikali ilikubaliana na Benki ya Dunia kutomlipa Mwalimu mmoja mmoja na badala yake zitumike kujenga na kukamilisha ujenzi wa nyumba za Walimu katika mazingira magumu ikiwa ni pamoja na kuweka samani. Ni katika kutekeleza azma hii, Serikali imeanzisha mpango kabambe wa ujenzi wa nyumba za Walimu kwa awamu kupitia mipango na Bajeti ya kila mwaka.

Mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu katika Halmashauri 40 ambazo kila moja imetengewa shilingi milioni 500. Katika Bajeti ya mwaka 2014/2015 jumla ya Halmashauri 120 zitanufaika na mpango zikiwemo 40 za awali. (Makofii)

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya kutia moyo, lakini ninaomba kufahamu kwamba kuwajengea nyumba na kuwawekea samani si njia pekee ya kutosheleza kuwasaidia hawa kuondokana na mazingira magumu, hapa nilikuwa napenda tu kushauri.

Swali, je, ni lini Walimu wenyé ulemavu ambao wao waishi kwenye mazingira magumu au mijini bado wana changamoto nyingi sana, Serikali itaweza kuwafikiria kuwapa posho ya mazingira magumu kutokana na hali zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margareth Mkanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niendelee kurudia kusema kwamba, tunakiri tunayo maeneo ambayo yanawakwaza Watumishi wetu kwa ujumla wake katika utendaji wao kutokana na ugumu wa mazingira hayo, lakini Serikali haiko kimya na kama ambavyo tumeleza mara nyingi tumeendelea kuboresha mazingira hayo kwa kuimarisha miundombinu mingine yoyote ambayo inaweza kuwawezesha watumishi na wananchi wanaokaa kwenye maeneo hayo kufanya kazi zao kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, Walimu ni kweli na utaratibu wa lini tunaweza kuwashudumia Walimu Walemavu kufanya kazi kwenye mazingira hayo ni ule ambao sasa Ofisi ya Waziri Mkuu, imeuweka katika mipango yake kwa Walimu mpaka Wanafunzi kwa kuwatengea Bajeti yake na kuanza kuwashudumia.

Tumeanza kuwashudumia kwa vifaa vyao vya kufundishia lakini tunapozungumzia suala la motisha tunawachukua kama Watumishi wengine ambao pia tunaangalia mahitaji yake na aina ya ulemavu wake ili kumfanya kuweza kuishi kwenye maeneo haya na kufanya kazi yake kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaendelea kuratibu vizuri suala la Walimu Walemavu kufanya kazi vizuri kwenye mazingira yao.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Utaratibu wa Serikali kukabili mazingira magumu umekuwa wa kiujumla bila kuzingatia matatizo ya sehemu husika. Napenda kuiuliza Serikali kwamba, kwanini isichukue jithada za ziada kwenye Kata za Goziba, Kerebe, Bumbire na Rutoro na kujua adha wanazopata Watendaji walioko kule hasa Walimu na kutoa suluhisho ambalo linalenga mazingira ya pale?

Mheshimiwa Spika, eneo ninalolitaja unahitaji kusafiri ndani ya maji kwa saa Nane katika Mtumbwi mbovu ili kuweza kufika Kerebe na Goziba. Sasa naomba kujua Serikali ni lini itakwenda kuangalia specific problems za watu wale na itoe jibu ambalo litapelekea Walimu waende kule?

Sehemu zote nilizosema kila shule ina Mwalimu mmoja au wawili.

**SPIKA:** Eeh, unamkaribisha aende huko maana yake hakuenda huko kabla ya hapo!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ninawakaribisha mawaziri wote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwijage kama ifuatavyo:-

Kwanza tumekabidhi mamlaka ya kuangalia huduma zinazotolewa kwenye maeneo yote kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, mtu wa kwanza ambaye anapaswa kujua ugumu za mazingira ya eneo lake na namna ya kutatua tatizo hilo ni Halmashauri yenye kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Spika, suala la Waziri sasa kwenda kuona ni ule mpango ambao tunao, na Mheshimiwa Mbunge anayo taarifa kwamba baada ya session ya Bunge hili nina ziara ya mkoa wa Kagera, kwa hiyo mionganoni mwa maeneo ambayo nitatembelea ni pamoja na Kata zile. Nitakwenda kuona mimi mwenyewe na tutashirikiana katika kutoa ufanuzi wa ufumbuzi wa jambo hili.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya Watumishi kama vile askari Polisi, Magereza na Wanajeshi, wana posho maalum, na kwa kuwa kazi ya ualimu ni ngumu na ninafikiri Mheshimiwa Naibu Waziri amekuwa Mwalimu na anajua ugumu ile kazi:-

Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu wa kuwafikiria Walimu kuweza kupewa pengine ration allowance kama sehemu ya kuwapatia motisha na hatimaye waweze kuondokana na tatizo la kukata tamaa kutokana na kazi yao kuwa ngumu. Ni lini pengine Serikali inaweza ikafikiria juu ya suala hili?

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Waziri...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo hili la kuangalia motisha au posho maalum kwa Watumishi hasa wa sekta ya elimu limefanyiwa kazi na Serikali, kwa namna ipi? Kwa kuunda Bodi ya Mishahara na Motisha ambayo inafanya mapitio ya jumla ingawa ni ya Watumishi wote kwa kuangalia mishahara yao, uwezekano wa kuongeza posho mbalimbali kulingana na ugumu wa kazi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo kwa sasa ninataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, inaendelea kufanywa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ili iweze kuboresha hasa maeneo haya.

Mheshimiwa Rais amepata nafasi ya kukutana na viongozi wa Chama cha Walimu mara nydingi kuona namna bora ya kuweza kuwahudumia Walimu kwa kuwapa kile ambacho kinawenza kuwasaidia katika utendaji wao na hasa katika kuwatia motisha ya kazi yao wanayoifanya.

Kwa hiyo, tuna matumaini baada ya muda mfupi chombo hiki kikikamilisha kazi kitatoa matokeo ya namna Watumishi wote wakiwemo Walimu watakavyohudumiwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, Mheshimiwa Mariam Kisangi atauliza swali hilo.

Na. 319

#### **Gharama kubwa kwa Masomo ya Vyuo vya Elimu ya Juu**

**MHE. MARIAM NASORO KISANGI** aliuliza:-

Gharama za masomo katika Vyuo Vikuu vya Tanzania zimezidi kuwa kubwa sana hasa kwa wanafunzi ambao hawapati mkopo, hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa Wazazi wa Wanafunzi hao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama za masomo kwa Wanafunzi hao hasa ikizingatiwa kuwa Vyuo Vikuu vinazidi kuwa vingi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimia Spika, ada za masomo katika Vyuo Vikuu nchini zimekuwa zikitofautiana kati ya chuo na chuo na kati ya programu na programu. Ili kupunguza tatizo hili, Serikali mwaka 1994 ilianzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa Wanafunzi wanaosoma Vyuo Vikuu wakiwemo wenyewe uhitaji. Mwaka 2004, Serikali ilianzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu wa Juu, kwa Sheria Na. 9 ili kuimariha utaratibu wa kutoa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia changamoto ya utofauti wa ada, Serikali kwa kushirikisha wadau mbalimbali ilifanya utafiti wa kina kuandaa mfumo wa kupanga ada elekezi kwa programu zote zinazofundishwa katika Vyuo Vikuu vyote nchini. Mwongozo wa Ada Elekezi ulizinduliwa tarehe 13 Machi, 2014 na ada mpya zitaanza kutumika mara baada ya utaratibu wa mfumo huo mpya kukamilika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kupitia Sheria Na. 7 ya mwaka 2005 ya Vyuo Vikuu, Kifungu cha 11(1)(f), Serikali kupitia Tume ya Vyuo Vikuu, itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ada Elekezi ili kudhibiti utozaji wa ada usiozingatia hali halisi ya gharama za uendeshaji.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, na ninapongeza sana juhudzi za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, kwa kuliweka vizuri hilo suala ili kupunguza mzigo kwa Wazazi ambao watoto wao wanakosa mkopo, lakini ninayo maswali mawili tu madogo na ushauri wa nyongeza:-

Kwa kuwa, tofauti ya ada kati ya chuo na chuo ni kubwa sana, na tofauti ya ada kati ya vyuo vya Serikali na vile vya binafsi ni kubwa sana.

Je, Serikali iko tayari kuongeza kasi ya mchakato wake huo ili uweze kufanyika kwa haraka kuwapunguzia mzigo Wazazi?

Kwa kuwa mpaka sasa kuna baadhi ya vyuo wanatoza ada kwa Dola ya Marekani, kwa nini Serikali inaruhusu wenyewe vyuo kutoza ada kwa Dola ya Marekani badala ya shilingi ya Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mheshimiwa Mariam Kisangi kwa juhudzi zake kubwa katika kusimamia sekta hii ya elimu ya juu nchini kwa manufaa ya watoto wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini katika maswali yake haya mawili nikianza na hili la kwanza la mchakato naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba hatua tuliyofikia katika mchakato huu ni nzuri sana karibu hatua zote ambazo zinahitaji Serikali izifanyie kazi sisi kama Serikali

tumeshakamilisha. Sasa hivi kilichobakia ni kazi kubwa tuliyowapa wamiliki wa vyuo vyote nchini, vyuo vya Serikali na vyuo binafsi kufanya mapitio ya gharama zao.

Narudia tena kufanya mapitio tena kwa haraka ya gharama zao katika vyuo vyao na hasa katika kupanga ada ili watuletee gharama halisi za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja na tunasema lengo hili ni kuhakikisha kwamba hawapangi ada ili ada zile zifanye kazi za kuendesha vyuo vyao.

Kwa hiyo naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kama watamaliza haraka tunaweza kuanza mfumo huu mwaka huu na kama wamiliki wa vyuo watachelewa mwakani lazima tuanze na hakuna msamaha na Serikali iko serious katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika swalii la pili la Mheshimiwa Mbunge ameuliza ni kwa nini vyuo vingine na taasisi nyingine zinazotoa elimu zimeendelea kutoza ada kwa kutumia Dola. Naomba niseme Serikali ilishatoa tamko ni kinyume na sera ya elimu ya nchi ya Tanzania kutoza ada katika taasisi za elimu, Vyuo Vikuu hata Shule za Msingi na Sekondari kwa kutumia Dola ya Marekani.

Naomba niwakumbushe wamiliki wote waache mara moja kama wanaendelea kufanya hivyo na niwaombe Watanzania sisi kama Serikali jambo hili tunalifuatilia kila siku mara nyingi sasa kama bado kuna wengine wanaendelea watupe taarifa wazazi na wanafunzi ili Serikali ichukue hatua na kuhakikisha kwamba tabia hiyo inaendelea kukoma katika kuwatoza watoto wetu wa Kitanzania ada kwa kutumia Dola ya Kimarekani na siyo *Tanzanian Shillings*. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabati umevaa ushungi hata sikutambui.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, leo ni Ijumaa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu nchini hata kusababisha wanafunzi hao kusoma katika mazingira magumu sana.

Je, nini sababu ya ucheleshwaji wa fedha hizo za wanafunzi wa Vyuo Vikuu?

**SPIKA:** Unachanganya mambo hii ilikuwa shule sasa tena wanafunzi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swalii lake zuri sana la nyongeza. Ni kweli kabisa wakati mwingine kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa kutoa fedha za mikopo kwa ajili ya wanafunzi wetu na Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua sababu.

Mheshimiwa Spika, sababu ziko nyingi ikiwemo wakati mwingine watoto wetu pia wanapojisajili katika vyuo vyetu vikuu wakati mwingine data zinazozungumzia masuala mbalimbali ya watoto hao zimekuwa zikichelewa kukamilika na kuifiki Serikali.

Lakini wakati mwingine pia mchakato wa uhamishaji wa fedha kutoka Hazina kuja kwenye Wizara ama kwenda kwenye Bodi ya Mikopo pia umekuwa ukichukua muda kwa kiasi fulani kutokana na sababu mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza hapa na pale.

Lakini naomba niwahakikishie Wabunge tunapokuwa tumemaliza michakato hiyo kwa wakati huu wa zoezi hilo linafanyika kwa haraka sana, lakini pale ambapo zoezi hilo linakuwa

limeingiliwa na mambo mbalimbali zoezi hilo limekuwa likichelewa na kweli watoto wetu wamekuwa wakipata shida lakini kwa niaba ya Serikali naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge sio nia ya Serikali ya kuchelewesha mikopo hiyo.

Kwa hiyo kama mazoezi hayo yatakuwa yanakamilika kwa wakati tutaendelea kutoa mikopo hiyo kwa wakati kuwasaidia watoto wetu wa Tanzania.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa ya kuuliza suala dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wawekezaji katika elimu hususan Elimu ya Juu ni ya ghamara kubwa sana na wanafunzi wanajitahidi hasa wale ambao hawapewi mikopo wanajitahidi sana kulipa lakini kumejitokeza baadhi ya Makamu Wakuu wa Vyuo na Uongozi wa Vyuo Vikuu wamekuwa wakizua wanafunzi kutokufanya mitihani kama hawajalipa ada.

Wakati sheria inaeleza wazi kwamba wanafunzi wanapaswa tu mitihani lakini mitihani hiyo izuiwe mpaka pale wanapolipa.

Nilitaka kupata kauli ya Serikali inasema nini kwaongozi wa baadhi ya vyuo ambao wamekuwa wakiwazuia watoto wetu kufanya mitihani wakati tayari wameshagharamia kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi, maana yake juzi kulitolewa maelezo hapa hapa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Susan Lyimo Waziri Kivuli wa sekta yah ii ya Elimu kwa swali lake zuri la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niliarifu Bunge lako Tukufu tatizo hilo limekuwa likitonea mara kadhaa. Lakini Serikali imekuwa ikisimamia kwa kweli na kuhakikisha kwamba inatatau tatizo hilo kila linapotoka. Sasa nitoe wito tu kwa viongozi wote wa vyuo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania wanapotaka kusimamisha zoezi la mitihani kwa watoto kama kuna sababu ya msingi wasifanye hivyo bila ya kuwasiliana na Wizara ili tuweze kupeana ushauri na miongozo ya kuweza kutatua matatizo hayo kabla hayajawaathiri watoto wetu. (Makofii)

**SPIKA:** Ni juzi hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba wanafunzi wafanye mitihani masuala mengine yataendelea baadaye. (Makofii)

Na. 320

#### **Sheria Kuhusu Stahili za Majaji**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Serikali ilishatunga Sheria ya Majaji tangu miaka mitatu iliyopita ambayo ilianisha bayana haki na marupurupu ya Majaji lakini mpaka sasa haijaanza kutumika:-

Je, ni lini Sheria hii itaanza kutumika ili Majaji wapate stahili zao na hatimaye kuwatia nguvu zaidi katika kutekeleza majukumu yao?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Bunge lilitunga Sheria ya Majaji iitwayo *The Judges (Remuneration and Terminal Benefits) Act, 2007*. Sheria hii ilianza kutumika tarehe 30 Machi, 2007 baada ya kutiwa sahihi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii inaainisha stahili mbalimbali ambazo mtu anayeteuliwa kuwa Jaji Mkuu, Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji Kiongozi au Jaji wa Mahakama Kuu anastahili kupata. Stahili hizo ni mishahara, posho mbalimbali, ghamama za likizo, usafiri, ghamama za matibabu, mafao ya kustaafu na ghamama za mazishi. (Kifungu cha 4(2) cha Sheria hiyo kinaleza wazi kuwa stahili zote za Majaji zitalipwa na Mfuko Mkuu wa Serikali (*Consolidated Fund*).

Hivyo ni imani ya Serikali kwamba posho na stahili mbalimbali ambazo wanapewa Majaji zinawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu mazuri nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

La kwanza kwakuwa stahili ambazo amezieleza Mheshimiwa Waziri mpaka sasa baadhi yake hawaajaanza kupata Waheshimiwa Majaji hasa posho mbalimbali. Je, Serikali itakuwa tayari kupitia stahili hizi kwa kila Jaji ili kuhakikisha kwamba Majaji hawa wanapata marupurupu yao yaende sambamba na uchapaji kazi wao?

Swali la pili, kwa kuwa Waheshimiwa Majaji kazi yao ni ya ku-risk sana na wanapata ulinzi ambaa si kamilifu hasa wachache wanapata kwenye makazi yao na wengine hupata tu pale wanaposafiri safari ndefu lakini wanapoenda kazini na kurudi kwenye makazi yao hawapati ulinzi.

Je, Serikali haioni kwamba hawa Majaji wana risk sana ukizingatia wanahukumu watu kunyongwa mpaka kufungwa maisha?

Je, ni lini Serikali itawapatia Majaji hawa ulinzi wa kudumu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo kwa maswali yake na naomba kumshukuru pia kwa kuendelea kufuatilia maslahi ya Majaji na watendaji wengine wa Mahakama.

Kama nilivyosema katika jibu la msingi sheria hii imeshaanza kutumika, katika utekelezaji wake ilionekana kwamba yapo mambo yanayohitaji kuwekewa utaratibu maalum ambaa unaendana na mazingira maalum ya Majaji kama yeye mwenyewe alivyoeleza. Hadi hivi sasa ghamama za mafuta, simu, umeme zinatolewa pamoja na mshahara.

Ziko stahili zingine kama vile matibabu ambazo zinatolewa kwa kadiri ya mahitaji. Lakini kama nilivyosema Serikali inaweka utaratibu maalum kwa sababu Majaji wetu na watendaji wengine wa Mahakama wanafanya kazi katika mazingira ya pekee, kwa hiyo kwa mfano kwa mafao ya afya tunaweka utaratibu maalum na funategemea kwamba hivi karibuni taratibu hizo zitakamilika ili Majaji waweze kupata mfumo endelevu wa matibabu.

Kwa stahili nyingine napenda kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitazifutilia na Serikali itafutilia ili kuona kama kuna mahali pamekwama tuweze kupakwamua mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake dogo la pili la nyongeza ni kweli kwamba Majaji kwa mujibu wa sheria wanastahili kupata ulinzi katika maeneo yao ya makazi na pia wakati wanaposafiri.

Lakini lazima nikiri kwamba kwa upande wa Dar es Salaam kumekuwa na changamoto kubwa ya ulinzi kwa Waheshimiwa Majaji hasa majumbani kwa sababu nyumba zao zimetapaka maeneo mbalimbali ya jiji. Lakini hata hivyo Serikali inao mpango wa kujenga nyumba za Majaji katika eneo moja na hivyo itakuwa ni rahisi kuimarisha ulinzi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikoani. Mikoani kwa kuwa Majaji ni wachache makazi yao yanapata ulinzi. Lakini endapo kutakuwa na eneo lolote ambalo lina changamoto basi tutakuwa tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kukabiliana na changamoto hiyo.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi namwomba nimwulize Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kumekuwa na mlundiko wa kesi katika Mahakama zetu na Majaji wengi wamekuwa wakifanya kazi hizo katika mazingira magumu.

Je, Serikali ina mikakati gani kuwawezesha Majaji hawa ili waweze kutatua kesi za wananchi kwa wakati muafaka?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana .

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, mlundikano wa kesi ni changamoto ambayo tumekuwa tukiikibili kwa muda mrefu na kama tulivyoeleza katika hotuba yetu ya Bajeti hivi sasa Mahakama imeweka utaratibu wa haraka wa kushughulikia mlundikano wa kesi kwa sababu tunaamini kwamba haki iliyocheleweshwa ni kama haki iliypotea.

Kwa hivyo tunaendelea kuweka mikakati hiyo na tayari tumeshaona matokeo mazuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwawezesha naomba kumjulisha Mheshimiwa Maryam Msabaha na Bunge lako Tukufu kwamba wanapata yale yote ambayo wanastahili usafiri, makazi yao yanatazamwa na posho ambazo wanastahili walipokuwa nje ya vituo vyao zinalipwa kwa wakati. Lakini kama kuna suala lolote ambalo ni mahsusini nitafurahi sana Mheshimiwa Spika kama Mheshimiwa Maryam Msabaha atalileta kwetu, lakini kwa sasa huko utaratibu endelevu.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kilianzishwa kwa lengo la kuandaan wataalamu katika fani hii ya sheria na hasa kuondoa tatizo la wafanyakazi hasa Mahakimu pamoja na Majaji ambao wangeweza kwenda kwa Refresher Course. Chuo kile mpaka sasa hivi kinaonekana vijana wanapomaliza shule wanatafuta kazi wakati kuna uhaba wa Mahakimu, Serikali inatoa tamko gani?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Chuo cha Mahakama cha Lushoto kilianzishwa kwa nia ya kuongeza sio tu weledi bali kuongeza idadi ya watendaji wa Mahakama wakiwemo Mahakimu. Hivi sasa tunapata wahitimu wengi na kama alivyo sema Mheshimiwa Shekifu ni kweli kwamba wapo wanaotafuta kazi, lakini hawatafuti kazi kwa sababu kazi hazipo ni kwa sababu labda wanakuwa na utashi mwengine.

Lakini sasa hivi kwa mpango ambao Serikali umeuweka kuanzia Mahakama ya Mwanzo tunaajiri Mahakimu wa Ngazi ya Diploma mpaka ngazi ya Shahada.

Kwa hiyo tunapenda kutoa wito kwamba vijana wetu wanaomaliza Chuo cha Lushoto waweze kuchukua nafasi hizo kwani kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge tunao uhaba. Lakini pia tunaboresha mazingira mazuri ili wale ambao wana sifa na uwezo waweze pia kuvutika kwa kazi muhimu ya kutoa haki na katika ngazi nyingine za utendaji.

Na. 321

### **Mahakama ya Mwanzo**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuliza:-

(a) Je, Mahakama za Mwanzo nchini ziko ngapi na zinahudumiwa na Mahakimu wangapi?

(b) Je, Hakimu mmoja wa Mahakama ya Mwanzo anahudumia Kata ngapi?

(c) Je, ni upungufu gani au changamoto zipo zinazoukabili uendeshaji wa Mahakama hizo na kuathiri upatikanaji wa haki kwa Wananchi na Serikali imejipangaje katika kukabiliana na upungufu/changamoto hizo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania ina jumla ya Mahakama za Mwanzo 960 zenye Mahakimu 991.

(b) Mheshimiwa Spika, wastani wa Hakimu mmoja kuhudumia Kata unategemea idadi ya Kata zilizopo katika Wilaya, idadi ya Mahakama za Mwanzo na idadi ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo waliopo katika Wilaya husika pamoja na kiwango cha mashauri yaliyopo katika eneo husika.

(c) Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoukabili uendeshaji wa Mahakama hizo na kuathiri upatikanaji wa haki kwa wananchi ni pamoja na:-

- (i) Umbali wa kijigrafia kati ya Mahakama na Makazi ya wananchi;
- (ii) Usafiri kwa Mahakimu na watumishi wengine wa Mahakama;
- (iii) Uchakavu na uhaba wa majengo ya Mahakama;
- (iv) Uhaba wa watumishi wa kada mbalimbali; na
- (v) Ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo Serikali imeweka mikakati ifuatayo:-

- (i) Ongezeko la Bajeti ya Mahakama kwa kila mwaka wa fedha;
  - (ii) Nafasi za ajira kuongezwa kwakada mbalimbali;
  - (iii) Kujenga majengo mapya 97 ya Mahakama ya Mwanzo;
  - (iv) Kukarabati Mahakama 380 zilizochakaa; na
- (v) Kutoa ajira za Mkataba kwa Mahakimu wastaifu wa Mahakama za Mwanzo wenye sifa na uwezo wa kuendelea kufanya kazi.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika ahadi ya Serikali ya kujenga Mahakama mpya 97 na kukarabati Mahakama nyingine 380.

Je, Serikali itakuwa tayari kukarabati Mahakama ya Mwanzo ya Rongai na kujenga ile ya Holili ambapo kuna kiwanja muda mrefu maeneo yako pembezoni na mpakani mwa nchi yetu na Kenya ili kuweza kuwarahisishia wananchi wa maeneo hayo wenye shida mbalimbali kutatua matatizo yao yanayohusiana na sheria?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mahakama ya Wilaya ya Rombo inatuhumiwa kuwaachia watuhumiwa wanaopatikana na makosa mbalimbali makubwa na madogo kwa tuhuma za rushwa. Siku za karibuni mtuhumiwa mmoja ambaye alikuwa Mwalimu wa Shule ya Msingi aliyetuhumiwa kwa kuwabaka wanafunzi mara mbili aliachiwa huru na kitendo hiki kinafanya Mahakama idharauliwe na wananchi kwa kiwango kikubwa.

Je, Serikali iko tayari kuichunguza Mahakama hii ili kuchukua hatua kama inabidi ili wananchi waweze kurejesha imani na Mahakama hii na kukomesha kabisa vitendo hivi ambavyo wananchi wanashirikiana na Polisi kukamata watuhumiwa halafu wanapofika ngazi ya Mahakama, Mahakama inawaachia?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Selasini amekuwa akifuatilia kwa karibu masuala yanayohusu Mahakama katika Wilaya ya Rombo na katika Jimbo lake, kwa swali lake dogo la kwanza ningependa kujibu kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa Mahakama ya Holili ni kweli kwamba kunahitajika kujengwa Mahakama ya Holili na kumekuwa na kiwanja. Tunapenda kuwapongeza wananchi wa Rombo kwa kutenga kiwanja hiki toka mwaka 2008. Lakini tumekuwa na uhaba wa Bajeti na mahitaji yamekuwa ni mengi lakini ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Mahakama ya Mwanzo ya Holili itaingia katika mpango wa ujenzi kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Kwa upande wa ukarabati wa Mahakama ya Rongai tunakwenda kwa awamu na ni matumaini yetu kwamba tutaifika Mahakama hii. Kwa sasa tumekwenda kwenye maeneo ambayo yalikuwa yana changamoto kubwa zaidi kuliko Rombo. Lakini tunaitambua changamoto hiyo na tutaiangalia katika mipango yetu ya ukarabati kwa siku zijazo. (Makofii)

Kuhusu swali lake dogo la pili, ningependa kujibu kama ifuatavyo. Katika kushughulikia masuala ya jinao Mahakama huwa zinazingatia Sheria za nchi yetu ambayo inatambua kwamba mtuhumiwa hatataiwa hatiani mapaka itakapothibitika amefanya kosa kwa hiyo yapo mazingira ambapo mtuhumiwa anaweza akawa amefikishwa Mahakamani kukawa na

ushauhidi usio tosheleza au kesi ikawa inaendelea na kwa hiyo akapewa dhaman kwa mujibu wa Sheria.

Lakini ninatambua kuwa tumekuwa tukipokea malalamiko kutoka sehemu mbalimbali kuhusu watuhumiwa kuachiwa kwa macho ya wananchi isivyo sawasawa kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amezungumzia masuala mawili moja la kulawiti na moja la pombe haramu ningependa baada ya hapo Mheshimiwa Spika tupate taarifa zaidi kutoka kwa Mheshimiowa Mbunge ili tufuatilie na kuona kama kuna tatizo lolote liilo nje ya Sheria.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza, tunafahamu kabisa kwamba Mahakimu hawa wa Mahakama za Mwanzo huwa wanafanya kazi zao katika mazingira magumu lakini pia huwa wanapata msaada mkubwa sana kutoka kwa Wazee wa Baraza.

Ninaomba kufahamu hivi Wazee hawa wa Baraza wanaofanya kazi katika Mahakama za Mwanzo huwa wanapewa posho kiasi gani kutika Serikalini?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninamba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Idd Azzan kama ifuatavyo. Serikali inatambua kwamba Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na bila shaka wa ngazi zingine wanazo changamoto mbalimbali katika utendaji wa kazi zao. Ni kweli kwamba Wazee wa Baraza wana mchango mkubwa katika kusaidia utoaji wa haki katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Hivi sasa tunaendelea kuboresha mazingira ya kazi ya Mahakimu kwa kuwapatia vyombo vyta usafiri hivi karibuni tumeweza kutoa vifaa vya usafiri kwa Mahakama mbalimbali kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na kwa upande wa Wazee wa Baraza zipo changamoto kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Lakini kwa mwaka huu wa fedha tumeongeza kasi ya kuhakiki madai ya Wazee wa Baraza ili na wao wapate motisha ya kuwasaidia Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Kwa upande wa kiasi gani wanalipwa nitapenda Mheshimiwa Mbunge anipe fursa kidogo niangalie ni kiasi gani kwa sababu sinacho hapa kwa sasa. (Makofii)

**SPIKA:** Ni sawa, swali lenyewe lilikuwa nje ya swali la msingi. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, atauliza swali.

Na. 322

#### **Operesheni Kimbunga**

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR** aliuliza:-

Operesheni Kimbunga ilikuwa ni tishio kwa baadhi ya Watanzania.

Je, ni mafanikio gani yamepatikana na ni nini changamoto za opereshemi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, operesheni Kimbunga haikuwa tishio kwa baadhi ya Watanzania bali ilikuwa na lengo la kuondoa Wahamiaji haramu na wahalifu wanaojihusisha na vitendo vua uhalifu hasa vya mauaji, unyang'anyi wa kutumia silaha na utekaji wa magari. Mafanikio yaliyopatikana katika Operesheni Kimbunga ni kama ifauatavyo:-

- (a) Jumla ya wahalifu 16,096 walikamatwa, wahamiaji haramu 31,203 waliondoka au kuondoshwa nchini.
- (b) Mabomu kumi na moja ya kutupwa na mikono, bunduki themanini na nne, risasi 1369 na mitambo miwili ya kutengeneza silaha za kienyeji aina ya gobore vilikamatwa.
- (c) Ng'ombe 8226 walikamatwa kwa makosa ya kuchungwa kwenye hifadhi na mapori ya Taifa sambamba na kukamatwa nyara mbalimbali zikiwemo mbaao 2,105 na magogo 86.
- (d) Kesi 223 za makosa mbalimbali zilifunguliwa zikiwemo za unyang'anyi wa kutumia silaha, kupatikana na nyara za Serikali. Kupatikana na bangi kilo 77 na kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya Hifadhi za Kitaifa kinyume na Sheria.
- (e) Kupunguza matukio ya uhalifu katika Mikoa iliyohusa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafaniko hayo Operesheni Kimbunga ilikumbwa na changamoto kadhaa zikiwemo:-

- (a) Ukosefu wa vitambulisho vya Taifa vya uraia katika kuwatambua raia halisi wa Tanzania;
- (b) Uhaba wa rasilimali fedha na rasilimali watu na vifaa jambo ambalo liikwamisha zoezi kwenda kwa haraka kama ilivyokuwa imepangwa;
- (c) Baadhi ya viongozi wa kisiasa kujaribu kuingilia zoezi hili kwa maslahi ya kisiasa ikiwemo hofu ya kupoteza wapiga kura ambaao kimsingi ni wapiga kura bandia; na
- (d) Baadhi ya Wahamiaji haramu kumiliki vibali na nyaraka za kughushi ambazo hutolewa kwa raia wa Tanzania pekee na hivyo kupelekea zoezi la utambuzi kuwa gumu. (Makofii)

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jawabu lake zuri alilolitoa ambalo limetoa elimu kwa Watanzania na kuelewa kazi hii ni vipi Serikali ilivyochukua hatua nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa baadhi ya Wahamiaji haramu ambaao tayari walikuwa wamerejeshwa nchini kwao na hivi sasa baadhi yao kwa kasi kubwa wanarudi tena Tanzania. Je, Serikali inatambua suala hilo?

(b) Kwa kuwa Operesheni Kimbunga wakati ikitekeleza shughuli zake iliathiri hata wale watu ambaao walikuwa hawahusiki na masuala hayo.

Je, Serikali itaeleza vipi kuhusu kasoro hizo ambazo zilijitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia pamoja na kumpongeza kwa uungwana.

Kuhusu Wahamiaji ambao walirudishwa nchi kwao kurudi hili ni jambo ambalo tulilielewa kabla hata Operesheni haijaanza na kwasababu hiyo Operesheni hii ilifanywa kwa awamu tatu na awamu ya nne ikawa ni kuhakikisha kwamba tunaunda tusk force Mikoani na Wilayani kuhakikisha kwamba saa zote wanafutilia wageni ambao watakuwa wanarudi au bado wanakuwa hawajabanwa na hatua za awali na katika hili niwapongeze tusk force za Mikoa kwasababu katika mwezi wa Desemba mwaka jana wahamiaji 825 walikamatwa na kurejeshwa tena nchini kwao.

Pia katika Mwezi Aprili, 2014 wahamiaji wapatao 564 pia walirejeshwa katika jumla hii, kwa hiyo Operesheni ni Operesheni lakini shughuli za kuzuia Wahamiaji haramu zipo na zitaendelea kuwadhibiti wale ambao watajaribu kurudi.

Ni kweli kwamba kulitokea baadhi ya wakati mikanganyiko na kuna Watanzania mambo kwa bahati mbaya walihusika au kuathirika kwa namna fulani kwa niaba ya Serikali ninatoa pole pale ambapo watu waliathirika bila ya sababu. Lakini tatizo ambalo bado litaendelea kuwepo kama hatuna vitambulisho. Wakati mwingine ni vigumu sana mtu kujieleza kuwa yeye ni Mtanzania na ikatosha.

Wapo waliosema kuwa ni Watanzania lakini bado wakachukuliwa, wakahojija na ikachukua muda na ile haikuwa haikuwawezesha kufanya shughuli zao kama kawaida. Lakini operesheni ni operesheni na Ulinzi ni Ulinzi kwa hiyo, tuendelee kufahamu kuwa hili linaweza kutokea na pale linapotoka basi wananchi tuwaombe watuelewe.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, kubadilisha sura za Mawaziri hakujaleta tija katika Operesheni hizi, kumekuwepo na ukiukwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa Sheria za kazi kwa watendaji na askari. Ningependa kujua wale waliokosea baada ya kuwa tumewafukuza Mawaziri wao wamechukuliwa hatua gani?

**SPIKA:** Uliwafukuza wewe? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Nyerere, Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaziona tofauti sana za uelewa ukiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na ukiwa Waziri kivuli, lakini wa Wizara nydingine. Ndugu yangu anaanza kuchanganya mambo sasa. Operesheni ambayo ninaizungumzia hapa ilikuwa ni operesheni Kimbunga na hii Operesheni ilifanyika kwa mafanikio na hakuna Waziri aliyewajibika kwa Operesheni hii.

Pamoja na hilo ninaomba nimsaidie kuwa Operesheni ambayo ilitukwaza ilikuwa Operesheni Tokomeza ambayo kwa bahati mbaya kuna vitendo vilifanyika na kuna Mawaziri ambao waliachia ngazi.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kulikuwa kuna wasiwasi kwamba pengine kuna haki za binadamu zilivunjwa na kwa ajili hiyo tulikubaliana kwamba itaundwa Tume kufuatilia kwa undani nini kilitokea, ili tujue nani kafanya nini na kwa nani.

Nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwamba ameshachukua hatua ya kuunda Commision hiyo na hivi karibuni aliwaapisha Mwenyekiti na Watendaji wa Commision hiyo.

Baada ya muda ripoti itatoka lakini itaenda kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliyeiunda. Jambo hili pengine tutapata taarifa ambazo tutaendelea kuzijadili Bungeni. (Makofii)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa miaka ya nyuma ilikuwa ikitumia sana Mfumo ule wa Mabalozi ambao ulisaidia sana mgeni yoyote anapoingia kwenye Kaya ile ni lazima aka - ripoti kwa Balozi na hivyo iliweza sana kudhibiti wageni hasa wale wasiofahamika na kutambua wahamiaji haramu.

Je, Serikali iko tayari sasa kurudisha mfumo ule ili iweze kusaidia na kuimarisha ulinzi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba ujibu kwa kifupi siku hizi unajua siasa unajibu kwa kirefu sana. (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ninaomba njibui swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifutavyo, bado Serikali inawatambua Mabalozi wa Chama Tawala na wanaendelea kufanya kazi zao kama ilivyo kawaida.

Aidha, kuna wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji ambao kazi yao inafanana na hawa Mabalozi na wanaendelea kufanya kazi hii ipasavyo. Kuna baadhi ya maeneo kuna matatizo kwamba hata hawa tunaowaita wakuu wa vijiji ni watu ambao walikuja wakahamia na wameloweaa.

Kwa hiyo, jambo hili haliendi inavyopaswa, tutachukua hatua kuhakikisha kwamba tunahuisha shughuli za Ubalozi katika maeneo yote ili tuweze kuhakikisha kwamba taarifa za Wahamiaji haramu zinakuja haraka Serikalini.

**SPIKA:** Ninaomba tuendelee na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Technolojia, Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, atauliza swali hilo. Wakati wa maswali hakuna taarifa wala nyongeza Mheshimiwa Mwatuka ndiyo unauliza eh! Sikutegemea kwa niaba yake Mheshimiwa Mwatuka. (Makofii)

Na. 323

#### **Kulinda afya za Watumiaji wa Simu za Mikononi**

**MHE. CLARA D. MWATUKA (K.n.y. HAROUB MOHAMMED SHAMIS)** aliliza:-

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imekiri kuwa utumiaji wa simu za mikononi una madhara kwa afya za watumiaji hasa unapoongea na simu kwa zaidi ya dakika sita (6) mfululizo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kulinda afya za watumiaji wa simu hasa vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI - MHE. CHARLES M. KITWANGA ( K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swala la Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mbunge wa Chonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya simu za mikononi husafirishwa kutoka shemu moja hadi nyingine kupitia mawimbi ya radio yanayozalishwa na umeme. Mawimbi haya ya mawasiliano ya simu katika hali ya kawaada yamethibitishwa kitaalamu kuwa yapo katika kiwango cha chini na hivyo kutokuwa na madhara kwa binadamu.

Hata hivyo, taarifa za maendeleo za uchunguzi zaidi uliofanywa na taasisi mbalimbali za afya duniani umebaini kuwa mawimbi hayo ya simu yana madhara yake pale mtumiaji anapoongea na simu kwa muda mrefu na hasa kwa kutumia simu zenye ubora ulivyo chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda afya za watumiaji Serikali kupitia mamlaka zake mbalimbali za udhibiti wa mawasiliano na viwango inaendelea na jitihada za kuwaelimisha wananchi kuhusiana na madhara hayo yanayoweza kujitokeza kutohaka na kuongea kwa muda mrefu, pamoja na kuendelea kuhakikisha uingizaji wa bidhaa bora za simu zenye viwango vinavyotakiwa pamoja na na uwezo wa kumkinga na madhara yanayoweza kujitokeza kutohaka na kuongea na simu kwa muda mrefu.

Kupitia Bunge lako Tukufu ninapenda kuwasihii wananchi kutumia simu za mikononi zenye ubora unaokubalika pamoja na kushirikiana na Serikali katika kupambana na wafanya biashara wanaoingiza bidhaa za simu za mikononi zilizo chini ya kiwango cha ubora.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninapenda kuuliza swali dogo tu la nyongeza kwamba kwa kuwa, humu madukani simu zilizojaa ni hizi za Mchina zilizo chini ya viwango na kwamba uwezo wa wananchi walio wengi vijijini ni huo wa kupata hizi simu kwa kuwa bei inakuwa ni nafuu.

Je, Serikali inasemaje juu ya kudhibiti hawa waingizaji wa simu hizi ambazo ziko chini ya viwango kwamba wasizidi kuziingiza?

Swali la pili, kwa kuwa simu zenye ubora wa viwango bei zake ni kubwa na watu wa kipato cha chini hawawezi kuzifikia.

Sasa Serikali inasemaje juu ya kuwafanya hawa wenye viwango vya chini nao waweze kuzipata?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI - MHE. CHARLES M. KITWANGA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ninaomba kujibu maswali ya ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi simu za Mchini zenyenye bei nafuu, siyo zote zilizo chini ya kiwango kuna simu ambazo zina bei ya chini kabisa lakini zina kiwango kizuri kabisa ambacho mwananchi yoyote wa kawaida anaweza kumudu kununua.

Tunachozungumzia ni zile simu ambazo zimetengenezwa kwa kuigiza na ambazo hazina kiwango na Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba watu hawa hawaziingizi katika soko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu simu ambazo Mheshimiwa Mbunge ameomba kwamba tufanyeje, kwa kweli simu za kawaida ambazo zinaingizwa na ambazo ni za kiwango kwa mfano hizi za tochi. Ni simu nzuri tu na zina kiwango kizuri tu. Kwa hiyo, niwaombe wananchi washirikiane na Serikali kuhakikisha kwamba wanapoona simu ambazo si za kiwango watupe taarifa na tuhakikishe kwamba tunaziondoa sokoni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Opulukwa, swali la nyongeza!

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, swali nililotaka kuuliza limeshajibiwa tayari. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vullu, swali la nyongeza!

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Afya inaweza ikaathirika kutokana na mionzi au hata kwa ubora hafifu wa simu, lakini pia afya inaweza ikaathirika kwa kuangalia vitu ambavyo vinapatikana kwenye simu, kwa mfano picha ambazo zipo kinyume na maadili yetu na hasa vijana wakawa wanaathirika.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba picha au maelezo ambayo yapo kinyume na maadili yetu kwa vijana, yasiweze kuathiri afya zao, watalindwa vipi hawa vijana na sisi watu wazima? Naomba majibu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI- MHE. CHARLES M. KITWANGA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Spika, wajibu wa malezi ni wa mzazi na wajibu wetu sisi kama viongozi ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti kadri iwezekanavyo picha zozote ambazo zinakwenda kinyume na maadili yetu.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Watanzania wote na Waheshimiwa Wabunge, watambue kwamba wajibu wa kwanza wa kuhakikisha kwamba tunazuia ni wa mzazi mwenyewe. Kwa hivyo tuhakikishe tunawaelekeza watoto wetu waweze kufahamu kwamba hili ni jambo jema na hili ni jambo bayo, lakini kwa kutumia teknolojia, tunajitahidi kupilta TCRA kuhakikisha kwamba mitandao hiyo ambayo si mizuri sana kwa jamii yetu inazuiwa.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Leticia Nyerere!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa simu zisizo na ubora zimeleta madhara makubwa sana na hata vifo na kwa kuwa ni Serikali ndiyo inatakiwa kuhakikisha kwamba inalinda afya za Watanzania, lakini kwa bahati mbaya imeshindwa kufanya hivyo. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kuwalipa fidia wale wote ambao wameathirika kutokana na simu mbovu zinazoingia nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI- MHE. CHARLES M. KITWANGA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Spika, wajibu wa kwanza wa kuhakikisha kwamba unatumia chombo bora ni wa mtumiaji yeye mwenyewe. Kwa hivyo, Serikali imeweka vyombo mbalimbali vya kuhakikisha kwamba bidhaa zote zinazoingia ndani zinakuwa ni za viwango vinavyotakiwa. Sasa itakuwa ngumu sana pale Serikali itakapotakiwa kumliipa mtu wakati mtu amesafiri labda akaenda Kenya akanunua hiyo simu akaja nayo.

Mheshimiwa Spika, tunachosema sisi ni kwamba vyombo vyetu, kwa mfano TBS na TRA wote hao wanahakikisha kwamba vifaa vinavyoingia ni vya ubora unaotakiwa. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba popote pale ambapo kifaa kitapatikana, wajibu wa kwanza ni wa mtumiaji mwenyewe.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Said Juma Nkumba swali linalofuata.

Na. 324

#### **Ahadi ya Kujenga Minara ya Simu Kata za Kipiri, Kiloli na Kitunda**

**MHE. SAID J. NKUMBA (SIKONGE)** aliuliza:-

Ahadi za kujenga minara ya simu kwenye Kata za Kipiri, Kiloli na Kitunda ni ya siku nyingi lakini mpaka sasa bado haijatekelezwa:-

- (a) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?
- (b) Kwa sababu ahadi hiyo ilipata Baraka za Mheshimiwa Rais alipotembelea Tarafa ya Kiwere na kuahidi tatizo la kukosa mawasiliano kwenye Tarafa hiyo kupatiwa ufumbuzi. Je, Serikali inawaahidi nini wananchi hao ili waweze kujenga imani kwa Serikali yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI- MHE. CHARLES M. KITWANGA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina nia ya kufikisha huduma za mawasiliano maeneo yote yasiyokuwa na huduma za mawasiliano hapa nchini. Zoezi la kifikisha mawasiliano ya simu katika eneo moja linahusisha hatua nyingi zikiwemo kuyaainisha maeneo husika, kufanya tathmini ya ukubwa wa eneo husika, kupata idadi ya Wakazi, kuangalia hali halisi ya huduma ya mawasiliano na kuangalia kiasi cha ruzuku kinachohitajika kwa eneo husika. Baada ya hayo eneo husika huingizwa katika mchakato wa zabuni.

Mheshimiwa Spika, Kata za Kipanga, Kiloli, Kipili na Kitunda katika Wilaya ya Sikonge ni mionganoni mwa Kata zilizoainishwa kupelekewa huduma za mawasiliano ambapo Kata zote zimepatiwa Wazabuni.

Kata ya Kipanga imepata Mzabuni TTCL (awamu ya kwanza A) kwa gharama ya sh. 594,057,000/= na Kata za Kiloli, Kipili na Kitunda zimepata Mzabuni anayeitwa Vodacom (awamu ya kwanza B) ambapo maeneo yote yanatarajiwa kupata mawasiliano mwishoni mwa Mwezi Desemba, 2015. Gharama ya kupeleka mawasiliano katika Kata hizo ni; Kiloli- sh. 237,800,000/=, Kipili- sh. 326,360,000/= na Kitunda sh. 451,060,000/=.

(b) Mheshimiwa Spika, tunawaahidi wananchi kuwa, maelekezo ya Mheshimiwa Rais yanatekelezwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma ya mawasiliano. Wakati mwagine ucheleweshaji wa kufikisha huduma unasababishwa na mambo mbalimbali yakiwemo ukosefu wa miundombinu muhimu kama barabara na umeme na ukosefu wa fedha kufadhili miradi yote kwa wakati mmoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nkumba, swali la nyongeza!

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, maswali mawili madogo. La kwanza, nataka nifahamu huo muda alioutaja ni wa mkataba wa kazi au ni makadirio aliyojatoa?

Swali la pili, sasa Serikali kwa sababu limeshughulikia jambo hili kwa muda mrefu.

Je, Serikali ipo tayari kushirikiana na Makampuni husika kuhakikisha kwamba muda huo unafupishwa ili wananchi wa maeneo niliyoyatajwa waweze kufaidika na huduma hii ya simu za mkononi?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI- MHE. CHARLES M. KITWANGA( K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kwamba muda niliousema ni wa kimkataba. Sehemu ya pili, Serikali itajadiliana na Wakandarasi kuona kwamba wanafikisha mawasiliano mapema iwezekanavyo kwa kadri itakavyowezekana, lakini tutambue tu kwamba mchakato wa kufikisha mawasiliano unahuishisha mambo mengi. Kwa hiyo, tutajaribu kuona kwa namna gani ambavyo muda huo unaweza ukafupishwa bila kuathiri ubora wa kazi.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chiligati. Nataja ambaa huwa hawasimami simami.

**MHE. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa huko huko jirani na Mheshimiwa Nkumba kuna Kata za Manyoni, Makanda na Sanza ambazo nashukuru sana kwamba zimeshapata Mkandarasi, Vodacom. Ameshafika lakini baada ya kufika kachagua eneo halafu akatoweza, sasa karibu mwezi wa pili huu. Sasa Mheshimiwa Waziri, atasaidiaje ili Mkandarasi arudi na afanye kazi kuondoa shida katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI- MHE. CHARLES M. KITWANGA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Spika, Mkandarasi si kwamba ametoweka, Mkandarasi ameagiza vifaa na vifaa vitakapofika, atarudi pale kuendelea na kazi kama inavyotarajiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lwanji!

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Kata ya Mwamageme ni jirani kabisa na hizo Kata za Wilaya ya Sikunge kama vile Kipili. Waziri anasemaje kuhusu hiyo Kata ya Mwamageme ambayo imesahauliwa kwa muda mrefu? (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wote hawa wanataka simu. Sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI- MHE. CHARLES M. KITWANGA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Spika, natambua hiyo Kata ya Mwamagemebe, nilikwenda nikakaribia kufika kule hivi karibuni na nimhakikishie tu kwamba Kata ya Mwamagemebe ni kati ya Kata ambazo zipo kwenye awamu ya kwanza 'B' kuwekewa mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Arfi, wa mwisho!

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa Mamlaka ya Mawasiliano baada ya kuweka mtambo wa kudhibiti mapato imejiongezea mapato maradufu.

Je, sasa ni kwa nini Serikali isiiagize Mamlaka ya Mawasiliano kupeleka fedha hizo kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ili waweze kujenga minara badala ya kutegemea Makampuni na kwenda kuwabembeleza?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI- MHE. CHARLES M. KITWANGA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kabisa mahitaji wa pesa kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Iakini vile vile tutambue kwamba Serikali hiyo hiyo ina mambo mengi ikiwa ni pamoja na Vituo vya Afya pamoja na barabara, ndio sababu pesa hizi zinakwenda kwenye Mfuko Kuu, Iakini baadhi ya sehemu ya pesa hizo zinabaki TCRA na kiasi kidogo kinakwenda mawasiliano kwa wote. Nimhakikishie tu kwamba Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba mawasiliano yanafika kwenye kila eneo ambalo halijapata mawasiliano mpaka sasa hivi.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge mda wa maswali umekwisha. Tume-relax sana kwenye maswali kwa sababu tulikuwa na muda lakini siyo utaratibu. Utaratibu ni kwamba maswali yajibiwe kwa ufupi ili wengi wapate nafasi na waulizaji maswali wasipige hotuba ili wengi wapate nafasi.

Naomba niwatambue kwanza wageni. Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni 20 wa Mheshimiwa Captain Chiligati kutoka shina la kwanza la Tawi la CCM Chikuyu Wilaya ya Manyoni wakiongozwa na Kaimu, sijui wakiongozwa na nani, naomba wasimame! Anayeongoza hapo amekosea kuandika na mimi sina muda wa kusoma. Ahsanteni. Karibuni sana. (Makofii)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Juma Nkamia, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ambao ni wanafunzi 50, Walimu na wazazi 14 kutoka shule ya msingi Kwamtoro, Wilaya ya Chemba. Naomba hawa wote wasimame walipo. Ahsante sana na karibuni sana. (Makofii)

Tuna wageni wa Mheshimiwa John Lwanji wa Jimbo la Manyoni Magharibi. Ni wanafunzi na Walimu wakiongozwa na Bwana Rajabu Majala Mratibu wa Kata ya Sanjaranda. Naomba na hao wote wasimame walipo. Ahsanteni sana, msome kwa bidii. (Makofii)

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, kutoka Jimboni kwake Hanang wakiongozwa na Ndugu Mhishaa Chaloda. Hawa wako wapi? Wako kule nyuma kabisa karibuni sana! (Makofii)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira ambao ni wanafunzi 60 na Mwalimu mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana

Tanzania Dar-es-Salaam. Naomba wasimame na hao wanafunzi kutoka Chuo Kikuu hicho, ahsante sana tunaomba msome kwa bidii. (Makofij)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Michael Laizer ambaao ni Ndugu Joseph Sadira, Mwenyekiti wa Halmashauri na Mrs Furahisha Makubila, Afisa Utumishi kutoka Longido. Naomba wasimame hapo walipo! Ahsante sana, wako pale wamesimama, karibuni sana!

Waheshimiwa Wabunge mnapozungumza mjue sauti zenu zinakuja. Tutawataja kwa majina wanaoongea kwa sauti.

Halafu nina mgeni wa Mheshimiwa Martha Mlata ambaye ni Ndugu Mariam Msangi kutoka Dar-es-Salaam. Sijui yeye ni nani, wameandika Mariam tu. Ahsante Mariam. (Makofij)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Richard Ndassa ambaao ni Walimu 14 kutoka shule ya Msingi Ngubalu, Kata ya Mantare, Tarafa ya Ngulla, Jimbo la Sumve wakiongozwa na Ndugu Leticia Bundala na hawa nao wasimame walipo! Ahsante sana. Karibuni sana. (Makofij)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Stephen Wassira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uaratibu ambaao ni wafugaji kutoka Bunda wakiongozwa na Ndugu Mrida Mshota, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Kanda ya Ziwa. Hawa pia wasimame walipo kama wamepata nafasi. Wako hapa, karibuni sana ndugu wafugaji. (Makofij)

Tuna wageni ambaao wamekuja kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 18 kutoka Chuo Kikuu cha Eckernford Tanga wakiongozwa na Mlezi Ndugu Gervas Silau. Naomba wasimame walipo kama wamepata nafasi. Ahsante. Karibuni sana mwendelee kusoma vizuri. (Makofij)

Kuna wanafunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha Saint Johns Dodoma. Naomba na hawa pia kama wapo wasimame! Inawezekana nafasi imejaa.

Wanafunzi wengine 60 na Walimu wanne kutoka shule mbalimbali za English Medium, The Future Vision Tuition Center. Naomba na wao pia wasimame kama wako ndani. Ahsante. Ni watoto wadogo, someni vizuri. (Makofij)

Tuna wageni wanne kutoka Nuru Lutheran Church Mbalizi, wakiongozwa na Askofu Dokta Eric Mwambigija. Ahsanteni sana. Nashukuru kwa kuiombea nchi. Wafanyakazi kutoka Benki ya Posta wakiongozwa na Ndugu Twaha Khalfan, Meneja Tawi la Benki ya Posta Dodoma. Naomba hao wasimame! Wenyewe wako pale watatu. Ahsanteni sana. Pale Bungeni kwetu tunafungua Benki pia na nyinyi mkiweka sawa. (Makofij)

Tuna wageni wa Mheshimiwa John Mnyika ambaao ni wanafunzi 30 na Walimu wawili kutoka Shule ya Daughters of Mary Immaculate na washiriki wake Dar-es-Salaam. Naomba wasimame hapo walipo kama wamepata nafasi. Wako kule nyuma ahsante sana. Msome kwa bidii. (Makofij)

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni. Pia nina matangazo mengine machache. Unajua wageni wanaoletwa kwenye vikaratasi wanaachwa. Kuna wageni wa Mheshimiwa Martha Mlata, kuna Ndugu Izadini Msangi. Hebu asimame mama Msangi, yeye ni mke wa dereva wake Mheshimiwa Mlata.

Mheshimiwa Pauline Gekul Katibu wa Wabunge wanawake wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Wabunge wanawake wa CHADEMA kuwa kutakuwa na kikao mchana wa leo baada ya Bunge kusitishwa. Kwa hiyo, nadhani baada ya Bunge kusitishwa siyo mchana, ni

baada ya Bunge kusitishwa, watakuwa na kikao lakini hakusema ni wapi, wanajua? Simama useme ni wapi?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, ni ukumbi Na. 227 imeandikwa hapo juu kabisa.

**SPIKA:** Haya ni ukumbi Na. 227, Wabunge wanawake wa CHADEMA, mnafanya ubaguzi!

Mheshimiwa Suzan, ni lazima ujibu kila kitu? Tunaendelea.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Hapana nina kazi kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaeleze kwamba kama mnavyoona order paper hii, tunatakiwa kuingia kwenye Muswada wa *Finance Bill*, lakini hatuwezi kuingia asubuhi hii tutaingia mchana kwa sababu kumekuwa na masahihisho mengi, Muswada ukiletwa kama ulivyo utawachanganya ninyi wenyewe na utawachanganya na watakaoupokea.

Kutokana na hilo, inabidi uchapishwe upya baada ya masahihisho yanayostahili. Kwa hiyo utakuwa tayari mtagawiwa mapema ili kusudi jioni saa kumi na moja muwe tayari. Kwa hiyo nategemea Kamati inayohusika itakuwa imejijandaa na Kambi ya Upinzani pia itakuwa imejijandaa kwa maelezo. Tatizo ni kwamba ule Muswada inabidi uchapwe upya baada ya marekebisho mengi yaliyofanyika.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hivyo, kama mnavyofahamu na kama ratiba ya shughuli za Mkutano huu inavyoonesha, Bunge linatakiwa kujadili na kupidisha Muswada wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani wa mwaka 2014 (*The Value Added Tax Bill 2014*), pamoja na Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi wa mwaka 2014 (*Tax Administration Bill 2014*).

Waheshimiwa Wabunge, Miswada hii miwili ilielekezwa kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti ili kwa kushirikiana na wadau mbalimbali Kamati iweze kuichambua na kuiboresha na hatimaye kuingia Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na Bunge zima.

Kutokana na ukweli kwamba wakati Kamati ya Bajeti inapewa jukumu hili ilikuwa na kazi pia ya kushughulikia bajeti ya Serikali pamoja na Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2014, na kutokana na sababu kubwa kwamba, Miswada hii ililetwa ikiwa imecheleweshwa sana licha ya kuwa Miswada hii miwili ni mikubwa sana na inahitaji kufanyiwa kazi kwa undani kwa kutoa fursa kwa Kamati kushirikisha wadau wa kutosha, imekuwa vigumu kwa Kamati kuweza kukamilisha kazi ya kuchambua Miswada hii ili kuliwezesha Bunge kujadili katika mkutano huu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwapa taarifa kwamba Miswada hii haitafanyiwa kazi katika Mkutano huu wa Kumi na Tano ili kutoa fursa kwa Kamati za Bunge nyingine zaidi ya ile ya Bajeti kuishughulikia Miswada hii katika Chapter zinazohusika. (*Makofii*)

Kwa hiyo, kilichotokea ni kwamba, ile Miswada inagusa sekta mbalimbali, halafu ni Miswada mizito ya VAT na suala la *Tax Administration*. Wamejaribu Kamati zile kama nilivyowaagiza juzi kushughulikia chapter zinazohusu, lakini wakajikuta hawakuwaita wadau. Sasa usipowaita wadau, ukitunga mwenyewe, halafu kesho ikashindikana inakuwa ni tatizo la Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Miswada hii tutaahirisha mpaka Bunge linalofuata ili Kamati zinazohusika katika chapter zao wafanye kazi nzuri na baadaye waunganishe katika Kamati ya Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, lakini naomba niseme kwamba, si tabia njema hasa kwetu sisi Waheshimiwa Wabunge kuzua maneno. Unajua maneno ya uzushi na ya uwongo ni kitu kibaya sana katika jamii yetu wenyewe. Hii naweza kuwasema Waheshimiwa Wabunge lakini pia hata Waandishi wa Habari.

Katika sheria zetu za kawaida za utungaji wa sheria, kifungu cha *Public Hearing* ni official. Hakuna Muswada wowote unaopaswa uende hivi bila kuwashirikisha wanaohusika na matumizi ya Miswada ile, halafu professionally na *Internationally Mabunge* yote duniani lobbying ipo, *lobbyist* wapo. Maana yamezuka maneno ohh! Wamekuja wafanyabiashara, wamewashika Kamati ya Bajeti, wamefanya nini, haya ni maneno ya uzushi na uzushi mkubwa. Kwa sababu hata wewe Mbunge mmoja mmoja unaweza kuwa *lobbied*, ama Kamati yenye we ya hearing yenye we ni lobbying lakini ile tunaifanya official kwa sababu wanaitwa na Kamati na kukaribishwa wadau.

Sasa busara ya kila lobbying yeote wewe unayekuwa *lobbied* siyo kwamba unachukua package yote unaondoka nayo unakuja kuirundika humu ndani, hiyo siyo busara. Tumia mawazo yao kuweza kuchanganua kile kinachotakiwa kufaa kwa wananchi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo jamani, tuache majungu yanayoendelea bila sababu, haya yanaitwa majungu. Katika kufanya kazi zetu tunataka kuimarishe ufanyaji kazi wa Wabunge, sisi siyo watalaam wa kila kitu, kuna watalaam sehemu nyininge ambao wanaweza kutufaa zaidi na hata ikibidi tunatafuta consultancy na kulipia sisi wenye we Bunge. Tuache tabia hii inatupeleka tunakuwa wadogo mno, tunakuwa wadogo kabisa, wafinyu.

Kwa hiyo, hata magazeti kuandika ooh! Kamati ya Bajeti sijui inakula fedha wapi, nani kawapa fedha? Kama wapo nimesema vyombo vinavyohusika vipo na wewe kama unajua kwa nini usiwaambie fulani anachukua fedha? Lakini ni majungu, majungu, jamani hatujengi nchi kwa majungu, nawaombeni sana tuwe waangalifu wa midomo yetu na hisia mbalimbali. (Makofi)

Naipongeza Kamati ya Bajeti. Bunge hili mjadala wa bajeti wamezungumza watu 181, kila aliyezungumza hapa neno lake ilikuwa la muhimu kabisa, lakini hakiwezi kila kitu kikawa muhimu, yatakuwepo muhimu machache ndiyo wenzetu wale wanaingia, wanapata ushauri wa watalaam mbalimbali ndiyo yanaletwa humu ndani, siyo kila kitu ni muhimu na kama hivyo ndivyo basi hatuna kitu.

Kwa hiyo, tunapopata maoni pale wenzetu wanakaa usiku na mchana, ninyi wengine hamwendi kuwatembelea kule, mpaka saa nane, saa tisa za usiku wanafanya kazi, lakini wanaambiwa wanafanya hivyo kwa sababu sijui kitu gani. Jamani acheni majungu, mahali popote panapoendeshwa na majungu pamepungukiwa. Kwa hiyo, nawaomba sana, tabia za majungu zisipendi wala siyo mshiriki nazo. Kwa hiyo, naomba sana mambo haya tujirekebishe. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge wanatangaziwa kuwa Benki ya Posta Tanzania, naona tuliwaona wale vijana wetu pale wanaendelea na shughuli yao ya kutoa maelezo juu ya huduma yao mpya ya akaunti ya Simba na Yanga katika viwanja vya Bunge maeneo ya parking. Leo ni siku yao ya mwisho kueleza huduma yao hapa Bungeni. Hivyo, wanawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote kutembelea na kunufaika na huduma hiyo.

Baadaye huduma hiyo itaendelea kutolewa katika matawi yao yote nchini mnakaribishwa huku.

Waheshimiwa Wabunge kuhusu utaratibu kwanza nilimwona Mheshimiwa Mnyika. Naomba kwanza Mheshimiwa Mnyika ukae chini nimwite Naibu Waziri tafadali. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. MWIGULU L. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yako mazuri ulipoongelea Muswada wa VAT pamoja na Muswada wa Utawala wa Kodi, ningependa kuweka kumbukumbu sawa tu ili na Watanzania wajue. Jambo la Muswada wa VAT na Utawala wa Kodi ni jambo ambalo lilipitia kwenye kikao cha Makatibu Wakuu wote wa Wizara zote ambao wote wanashiriki na kila Katibu Mkuu alichukua akashirikisha watalaam wake na wadau wa sekta ya Wizara yake.

Pia ni jambo ambalo lilikwenda kwenye cabinet ambapo kila Waziri anakuwepo na watalaam wake na ni jambo ambalo tangu tuje hapa Bungeni Wabunge wote, Kamati zote, ripoti zote za Kambi Rasmi ya Upinzani tangu tuje hapa, ripoti zote za Mkaguzi wa Hesabu za Serikali tangu tuje hapa, kwa hiyo sioni jambo geni sana ambalo Wabunge hatulijui na wadau hatulijui kuhusu mambo yaliyopo kwenye Muswada huo wa VAT.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu moja ya jambo ambalo linaila sana nchi yetu, ni kutokuchukua hatua ya mambo tunayodhani yanakwamisha maendeleo. Ramani ya Dodoma hapa ndiyo iliyotumika Abuja, wenzetu walishajenga wametaja na mitaa Mtwara, Lindi, Mazengo sisi hata leo hatujawahi kufanya, lakini tunalalamika.

Sasa Serikali tulishaleta jambo hili ili liweze kuiokoa nchi kutokana na fedha zinazopotea hasa kwenye misamaha isiyo na tija. Mara zote Serikali tukichelewa kuleta kitu hapa, Bunge huwa linahoji ni lini Serikali italeta. Sasa kwa kuwa jambo hili tuliweka kwenye bajeti na tuliweka kwenye makubaliano ni lini litakamilishwa na Bunge?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu Utaratibu!

**SPIKA:** Naomba utulivu, mimi nasikiliza, naomba kuwa na uvumilivu. Mheshimiwa Naibu Waziri maliza.

Mheshimiwa Mcchemba tumekubaliana na viongozi wako kwamba hii inakuja baadaye. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako katika kipindi cha maswali, wakati Wizara ya Mambo ya Ndani...

**SPIKA:** Sasa Mnyika wewe umeniandikia mwongozo ndiyo ninaokupa, huo mwingine unatoa wapi?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Limetokea leo hapa sasa.

**SPIKA:** Hapana, anza ule tuliokupa ndiyo maana nilikupa wa kwanza, anza ile ya mwanzo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ningemba Mwongozo wako katika mkutano huu wa Bunge niliomba Mwongozo tarehe 12 Mei, 2014 kuhusu matatizo makubwa ya maji yaliyopo maeneo yanayohudumiwa na mtambo wa Ruvu Juu na Serikali

ikatoa kauli Bungeni juu ya matatizo ya mtambo huo na ikakiri uwepo wa tatizo, lakini Serikali ikasema vile vile hapa Bungeni ndani ya kipindi cha mwezi mmoja itatoa taarifa ya uchunguzi juu ya kujirudia mara kwa mara kwa matatizo hayo ili kubaini kama ni sababu za kiuendeshaji au kuna makosa ya kibinadamu katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, sasa mwezi mmoja umepita na bado kuna matatizo, mwezi huo wa uchunguzi umshakamilika. Naomba Mwongozo wako ili Serikali itakiwe kuwasilisha taarifa ya huo uchunguzi ambaa imeufanya ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa John Mnyika na kwamba ni kweli tuliahidi hivyo, lakini nataka niseme tu taarifa ipo katika hatua za mwisho kabisa kuwasilishwa kwa Waziri wa Maji na tutaileta hapa Bungeni, lakini pia ieeweke tatizo la maji ni la nchi nzima. (Makofii)

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Hapana, kaeni. Mheshimiwa Mama Sitta mwongozo wako nimeukataa kwa sababu haifuati utaratibu. Mheshimiwa nimemwona Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako, Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Baraza la Mitihani la Taifa limetoa mfumo mpya wa madaraja ya kidato cha Nne na kidato cha Sitta na mfumo huo utakuwa ni ule wa kutumia GPA yaani Grade Points Average, wastani wa alama.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limeleta mtafaruku mkubwa sana kwa sababu unaanza kutumika mwaka huu, kwamba mwaka huu watoto wa kidato cha nne watatumia mfumo huu mpya ambaa kimsingi haujaeleweka vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Mheshimiwa Rais alipokuwa anaongea na Wakurugenzi wa shule kule Mbeya mwaka jana mwezi wa Nne alitamka bayana kwamba Sera ya Elimu ingekuwa tayari mwisho wa mwaka na mambo yote haya yangekuwemo kwenye hiyo sera.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako Serikali inatoa kauli gani na ni lini sera ya elimu itakuwa tayari ili haya mambo yawe kwa ujumla wake na siyo kwa piecemeal kama ambavyo sasa hivi Baraza la Mitihani linafanya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona mnachanganya mambo. Mwongozo ni jambo fulani lililotokea humu ndani kipindi kilichopita, sasa sisi Baraza la Mitihani, mimi nitakuwa na Mwongozo nautoa wapi! (Makofii)

Kwa sababu Mwongozo ni jambo, soma kanuni ya Mwongozo, ni jambo lililotokea ama sasa, ama kipindi kilichopita humu ndani na mimi nikiwa nimekaa hapa nikalisikia na Hansard ipo. Sasa unaniuliza jambo limetokea nasemaje? Kwa hiyo, ningesema kweli na mimi nilisikia, lakini hili ni jipya wala sihusiki nalo hata sina Mwongozo. Sana sana naweza kuwaambia Serikali mmesikia basi. (Kicheko)

Mheshimiwa Mama Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mwongozo wangu unahu su jambo lililoteka humu Bungeni wakati maswali yakijibowi na Waheshimiwa Mawaziri.

Wakati Naibu Waziri akijibu swalii la Mheshimiwa Rosweeter kuhusu watoto wanaopata mimba shulenii, alijibu kwamba Serikali inaendelea na mkakati wa kushughulikia hili suala la watoto wanaopata mimba shulenii ili waweze kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, kwa kuwa mwaka 2007 kwa niaba ya Serikali, mimi nikiwa Waziri wa Elimu a Mafunzo ya Ufundu niilunda Tume ambayo iliongozwa na Profesa Galabawa na mtalaam anaitwa Mary Lusindi wakiungana na Mheshimiwa Susan Lyimo, Faida Bakar na Zaynab Vullu pamoja na wadau wengine, wakatembea nchi nzima. Tume ile ikaleta taarifa kwamba wadau wanasema watoto wanaopata mimba shulenii warudi na waendelee na masomo.

Mheshimiwa Spika, kama Tume ilizunguka nchi nzima na ikaleta taarifa hiyo, je, ni nini hata ya ile taarifa kwa sababu wadau walikubali. Ukiangalia usawa uko wapi? Wenzetu wa Zanzibar dakika 15 tu ukiruka na ndege pale wanaruhusu watoto wao wanaopata mimba wanaendelea na mafunzo. Juzi mwezi wa Pili tumekwenda Kenya wametushangaa kwamba khee! Ninyi watoto wenu wanaopata mimba hawaendelei, wenyewe wanaendelea tu.

Malawi wana policy tena wala siyo sheria re-entry policy watoto wanaendelea na masomo wakishapata mimba. Sasa cha ajabu ni kitu gani hapa Tanzania, watoto wetu wanaopata mimba wasiendelee na masomo? (Makofii)

**SPIKA:** Mwongozo siyo hotuba!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, namalizia kwamba *fifty fifty* haiwezi kupatikana kwa utaratibu huu, hawawezi kusoma na kuendelea, wanaoathirika ni watoto wa maskini.

Mheshimiwa Spika, ni nini mwongozo wako?

**SPIKA:** Kama swalii la Mheshimiwa Susan, swalii hilo siyo. Naomba Wizara zinazohusika kama mmesikia mkachukue hatua zinazostahili, mimi sina Mwongozo mwininge wowote. (Kicheko)

Mheshimiwa Kafulila!

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niombe Mwongozo kwa Kiti chako.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka ukiwa kwenye kiti hicho nilipoanza kuzungumza suala la ufisadi wa ESCROW wa takribani bilioni mia mbili, wewe wakati wa Wizara ya Nishati na Madini ulielekeza kwamba nitoe ushahidi. Mimi na Mheshimiwa John Nyika tukawasilisha ushahidi.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana kwamba mpaka sasa ushahidi ule hatujui uliupeleka wapi zaidi ya kuambiwa kwamba Waziri anautumia kukosoa. Mwenendo wa jambo hili tangu ulipoanza wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu na baadaye Wizara ya Nishati na Madini kwa namna unavyokwenda hata jana, kwanza kabla ya jana tukiwa Bungeni Mheshimiwa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali akaonesha kusudio la kutaka kunipiga na baadaye tukiwa nje ya Bunge akatoa kauli ambayo inahatarisha usalama wangu.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa nawaambia wananchi wa Jimbo langu watambue kwamba *in case* kikitokea chochote kile mhusika wa kwanza awe yeye kwa sababu ya kauli hiyo ya kusema kwamba atachukua kichwa changu.

Mheshimiwa Spika, mlolongo wa mambo haya...

**SPIKA:** Mwongozo siyo kesi.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nimejaribu kutoa *background* ili kuweka uelewa mmoja.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa jambo hili linalohusu zaidi ya bilioni mia mbili katika nchi ambayo imeshindwa kutatua tatizo la shuka za hospitali na madawati nchini ni dhahiri kwamba linaleta mashaka kuhusu dhamira ya Kiti kuweza kulishughulikia hata kuhtarisha maisha yangu mimi mwenyewe na wengine.

Mheshimiwa Spika, ni katika msingi huo, naomba Mwongozo wako hili jambo unalifanyia maamuzi gani ili kusudi lifike mwisho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafulila, kwanza kabisa wewe umeniandikia barua, kabla sijaona barua naisikia kwenye vyombo vyahabari, hiyo ni adabu hiyo? Siyo adabu. (Makofii)

Pili, suala hili lina uamuji kamili kabisa, tumepeleka kwa Controller and Auditor General na TAKUKURU, documents zako zote zinakwenda huko, ulitegemea sisi tufanye hukumu hapa? Ndivyo tunavyofanya hata ulipoleta juzi nimekushangaa sana.

Mheshimiwa Kafulila, nafanya naye kazi katika IPU, ni mmoja wa vijana ambaa ni hodari sana, lakini hili naona kama anali-mishandle kabisa. Sasa tunaanza kupata mashaka ni suala la kawaida ama siyo la kawaida. (Makofii)

Kwa hiyo, nataka kukuambia suala hili limeagizwa lipo kwa Controller and Auditor General na TAKUKURU, documents zako zote zitapelekwa hata huko peleka na hayo mengine. Hapa kwa sababu wewe umem-provoke na mwenzako amekuwa provoked, ndiyo mjue kabisa mnapotumia lugha mbaya mjue kabisa yote haya, kila mtu ni binadamu, tulieni suala la IPTL lina utaratibu wake. Kama mna documents mnapaleka kwa Controller na kwa TAKUKURU kama mnaziamini. Hakuna namna nytingine hatuwezi kubaki sisi tunasambaziwa makaratasii hapa tunafanya nayo nini, hatuwezi! (Makofii)

Jambo ambalo mtu anajua lina tatizo anakuwa na utulivu, kama unaamini unakuwa na utulivu, kama hujiamini huna utulivu. Sasa naomba documents zako zote uendelee kuzipeleka, tutapeleka zilipo zingine.

Mheshimiwa John Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Wakati wa kipindi cha maswali leo, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri Pereira Silima akijibuu swali kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani alisema kwa swali lilitohusu operesheni kimbunga kwamba, Serikali itaendelea kuwatambua Mabalozi wa Chama Tawala yaani CCM

akimaanisha kwamba mfumo huu wa Mabalozi ndiyo ambao unatumika kama mfumo rasmi wa utambulisho wa wananchi ngazi ya chini kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Nyalali ya mfumo wa Vyama vingi ilipokusanya maoni ya wananchi ilibaini kwamba katika kuingia mfumo wa Vyama vingi kati ya mambo yaliipaswa kufanyiwa marekebisho ni Chama Tawala kuhodhi mifumo ambayo kimsingi ni mifumo ya wananchi. Kufuatia ripoti ya Tume ya Nyalali Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 tulivoingia mfumo wa Vyama vingi ikaweka mifumo huru.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata Mwongozo wako ili Serikali itakiwe ama ifute hiyo kauli ya kwamba mabalozi wa Chama cha Mapinduzi ndiyo ambao wanahusika na utambulisho wa wananchi huko ngazi ya nchi, kwa kuwa hakuna sheria inayoweka mfumo wa namna hiyo, au itamke kwamba mabalozi wa vyama vyote ni halali kwa utambulisho rasmi wa wananchi maeneo popote pale nchini. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amekiuka Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kutoa kauli aliyoitoa. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, alichokusudia kusema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ambayo ndiyo kauli ya Serikali, Serikali nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mnyika inawatambua Viongozi wote wa Vyama vya Siasa, inawatambua katika ngazi zao kwa sababu ni mfumo rasmi uliowekwa katika Katiba zetu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, sasa mifumo hii katika ngazi mbalimbali kule chini, kwa CCM kuna mabalozi, kwa Vyama vingine sijui kuna nini lakini kuna alama zao tunazona zinatumika. Kwa hiyo la kwanza, nataka nithibitishe hapa kwamba Serikali inawatambua Viongozi wote wa Vyama vya Siasa, inawatambua Viongozi wote wa Dini, inawatambua Viongozi wote wa Kijamii na wa Kimila na itaendelea kufanya nao kazi. Kazi ambazo tunafanya nao Viongozi hawa kwa ujumla wao, ni masuala ya kuhimiza maendeleo na usalama wa nchi. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, ukienda Umasaini bila kumtambua Leigwanani hufanyi kazi yoyote. Kwa hiyo, hili ni lazima lieleweke. Viongozi hawa wote wa kijamii wamechaguliwa katika mifumo ya kisheria na Serikali itaendelea kuwatumia na tunawatambua, wakiwemo Mabalozi wa CCM. (Makofij)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, na wa CHADEMA!

**SPIKA:** Naomba mkae, hakuna maswali ya nyongeza. Unajua tatizo la Waheshimiwa Wabunge wanapenda kuotea mambo. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni. (Kicheko/Makofij)

(Saa 4.42 Asubuhi Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### **Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2014 (The Finance Bill, 2014)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

**SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele yako na mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2014 ambao umechapishwa upya unoajumuisha marekebisho katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya kiuandishi ambayo nitaeleza katika maelezo yangu kwenye sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia jioni hii ya leo kukutana hapa tukiwa wazima wa afya na vile vile nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Napenda kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali sasa imejipanga kutekeleza bajeti ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri kwa lengo la kuuboresha. Serikali inathamini sana ushauri na michango iliyotolewa na Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati na pia tunaendelea kufanya kazi maoni, ushauri na mapendekezo mengine kwa lengo la kuuboresha na kutekeleza bajeti ya Serikali kama ilivyokusudiwa. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao walichangia katika hotuba ya Bajeti ambayo niliwasilisha hapa Bungeni tarehe 12 mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wataalam wake wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakishirikiana na Wataalam wa Wizara ya Fedha kwa kufanya kazi usiku na mchana katika kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Ofisi ya Bunge, wadau mbalimbali katika Sekta ya Fedha, Biashara, na Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti wameitoa ushauri wao ambao tumeizingatia.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaelezea lengo la Muswada huu, naomba kuchukua dakika moja kutoa maelezo kuhusiana na taswira ambayo ilijengwa leo asubuhi kwamba Waziri wa Fedha amwaga chozi ambayo imeleta kidogo hali halisi ambayo si nzuri. Tunaomba Waandishi wa Habari wawe wanatafuta habari zilizo za kweli na za maana kabisa katika kuuza magazeti yao. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti haikunitoa chozi, tumeefanya kazi vizuri kwa maelewano na maafikiano kwa maslahi ya Taifa hili. Jambo liliotokea kwa lile liliotangazwa kwenye magazeti halikutokea na picha iliyowekwa ni picha ambayo ilichukuliwa wakati wa msiba wa marehemu Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, naomba sana Sekta hii tuithamini ya kuwapasha habari wananchi, ni haki yao, lakini tusipotoshe umma. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada huu ni kuboresha mfumo wa kodi na ada mbalimbali kwa kubainisha kisheria hatua kadhaa za mfumo wa kodi kama zilivyoainishwa katika hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kuzifanyia marekebisho Sheria 11 zinazohusu masuala ya fedha, kodi na ushuru kwa lengo la kuweka, kurekebisha, kupunguza, au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kupunguza misamaha ya kodi kwa wawekezaji ili kubakiza misamaha yenye tija na yenye kuchochea uwekezaji mkubwa katika Sekta mbalimbali pamoja na kupandisha kiwango cha chini cha mtaji wa uwekezaji ili kuwa na wawekezaji walio makini zaidi kwa kuwa kiwango cha sasa kimepitwa na wakati.

Pili, kupunguza kiwango cha kodi cha mapato ya ajira kwa ngazi ya chini kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12 ili kutoa nafuu ya kodi kwa wafanyakazi.

Tatu, kuainisha katika Sheria, Taasisi mbalimbali zinazostahili kupata msamaha wa tozo ya mafunzo ya ufundi stadi yaani STL.

Nne, kuweka sharti kwa Wakala, Mamlaka na Taasisi za Serikali kuwasilisha mapendekezo ya bajeti zao kwa Mpapaji Mkuu wa Serikali kwa uchambuzi ili kuwezesha Taasisi hizi kuchangia mapato yasiyo ya kodi kwa Serikali.

Tano, kufuta misamaha ya kodi kwenye saruji, nondo na mabati kwa wawekezaji na Makampuni ya Simu isipokuwa kwa vifaa vya ujenzi wa minara ya simu na miradi inayohusu ukarabati na upanuzi.

Mheshimiwa Spika, Sheria zifuatazo zitafanyiwa marekebisho: Sheria ya Leseni za Biashara, Na. 25 ya mwaka 1972; Sheria ya Ushuru wa Forodha, Sura 403; Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura 245; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; Sheria ya Mauzo ya Nje, Sura 196; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura 220; Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38; Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370; na Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura 82.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Muswada. Muswada huu pamoja na marekebisho yake yamegawanyika katika sehemu 12. Sehemu ya kwanza yenye vifungu namba moja na namba mbili inahusu masuala ya utangulizi, yaani jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo Sheria itaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2014.

Sehemu ya pili yenye vifungu vitatu mpaka nane. Inapendekeza kufanya marekebisho Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972 ili kuweka utaratibu wa kutoa leseni za biashara zinazodumu kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kutolewa leseni husika au kwa kipindi cha miaka mitatu kwa mkupuo badala ya utaratibu wa sasa ambapo leseni zinazotolewa humaliza muda wake tarehe 30 Juni, ya kila mwaka. Vile vile mfanyakibashara ataruhusiwa kulipa ada ya leseni kwa mkupuo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu. Marekebisho haya yanalenga kuimarisha kumbukumbu za biashara, kurasimisha biashara na vile vile kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu yenye vifungu namba tisa hadi 11. Inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 194(4) cha Sheria ya Ushuru wa Forodha, Sura 403 kwa lengo la kufuta misamaha ya kodi inayotolewa kwa Makampuni ya Simu. Aidha, yamefanyika

marekebisho ambapo vifaa vya ujenzi wa minara ya simu vitaendelea kupata misamaha hii ili kuhakikisha huduma hii muhimu ya mawasiliano inawafikia wananchi hadi vijijini.

Mheshimiwa Spika, sehemu nne yenyenye vifungu 12 hadi 26 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kama ifuatavyo:-

Kwanza, kufuta ushuru wa bidhaa wa asilimia 0.15 uliokuwa unatozwa kwenye huduma ya uhawilishaji wa fedha yaani Money Transfer na badala yake kutoa asilimia 10 kwenye tozo na ada za huduma hiyo zinazotozwa na mabenki na Makampuni ya Simu katika uhawilishaji wa fedha.

Pili, kuondoa Mamlaka ya Waziri wa Fedha ya kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petrol isipokuwa tu misamaha iliyopo inayotolewa kuitia Existing Agreements pamoja na misamaha kwenye mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali na Washirika wa maendeleo ili kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mamlaka haya yako kwa Waziri wa Fedha, hivyo kuondolewa kwa Mamlaka haya kunamaanisha kwamba, hakuna mtu mwingine atakayeruhusiwa kutoa misamaha hiyo. Lengo la hatua hii ni kudhibiti matumizi mabaya ya misamaha hii na kuelekeza misamaha ya aina hii kwenye miradi ya maendeleo na yenyenye manufaa kwa umma.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua hii ina lengo la kuifanya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 iwe sambamba na Sheria ya Uwekezaji, Sura 38 na Sheria ya Fedha mwaka 2013 ambazo zilifanyiwa marekebisho ili kuondoa msamaha wa kodi kwenye mafuta ya petrol.

Tatu, katika eneo la kutosha Ushuru wa Bidhaa kwa magari, Serikali baada ya kutafakari hoja za Waheshimiwa Wabunge imefanya marekebisho kama ifuatavyo:-

Kwanza, kutoza ushuru wa bidhaa kwenye magari yasiyo ya uzalishaji yaani *non-utility motor vehicles* na kuweka ukomo wa umri wa miaka minane kwa magari hayo badala ya miaka 10. Aidha, magari yenyenye umri wa miaka minane hadi tisa yatatozwa ushuru wa bidhaa wa asilimia 15, badala ya asilimia 25 kama vile niliviotangaza katika hotuba ya bajeti. (Makof)

Aidha, magari yenyenye umri wa miaka 10 na zaidi yatatozwa ushuru wa asilimia 30 ili kutoa hamasa kwa watu kuagiza magari yasiyo chakavu. Lengo la hatua hii ni kupunguza wimbi la uagizaji wa magari chakavu ambayo yanababisha ajali, vifo na kusababisha gharama ya kutumia fedha za kigeni kuagiza vipuri mara kwa mara na vile vile kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua hii inakusudia kuwianisha umri wa magari yaliyoingizwa nchini kwetu na ya nchi jirani ili kuepusha hatari ya magari ya Watanzania kuzuiwa kuingia katika nchi hizo. Pia inakusudia kuimarisha viwanda vya kuunganisha magari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya kuzingatia maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge Serikali imefanya marekebisho ya viwango maalum yaani *specific rates* vya ushuru wa bidhaa zisizokuwa za mafuta non petroleum products ambazo ni vinywaji baridi, mvinyo, pombe na vinywaji vikali.

Mheshimiwa Spika, vinywaji baridi vimerekebisha kwa kiwango cha asilimia 5.0 badala ya asilimia 10. Aidha, mvinyo, pombe na vinywaji vikali sasa vitatozwa kwa kiwango cha asilimia 20. Bidhaa za sigara zitatozwa ushuru wa bidhaa wa asilimia 25 ili kutekeleza matakwa ya Mkataba wa Udhhibiti wa Matumizi ya Tumbaku Duniani yaani World Health Organization Frame

*Conventional Tobacco Control* wa Shirika la Afya Duniani ambayo ibara yake ya tano na sita inazitaka nchi zilizoridhia Mkataba huu kuweka utaratibu wa kisheria kikodi na kiutawala kwa ajili ya kuzuia na kupunguza matumizi ya tumbaku. Tanzania ni mionganoni mwa nchi zilizoridhia mkataba huo kwa lengo la kulinda afya za wananchi wake.

Tano, ni kuweka ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 25 kwenye vipuri chakavu vya magari na pikipiki pamoja na vifaa chakavu kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ikiwemo majokovu, mashine za kufulia, majiko ya umeme, majiko ya kupashia chakula, rejeta za umeme na vinginevyo vinahusiana na vyombo vya umeme vikiwemo runinga, wino wa kuchapishia, mashine za kuchapishia, mashine ya kutoa vivuli vya nyaraka, simu za mikononi na vinginevyo vinavyohusiana na hivyo vinavyoingizwa toka nje ya nchi. Aidha, kompyuta za mezani na kompyuta mpakato zilizotumika pamoja na baiskeli zimeondolewa katika orodha hii. (Makofii)

Sita, ushuru wa vinywaji baridi utapunguzwa kutoka sh. 91/= kwa lita hadi sh. 55/= kwa lita. Tunatarajia bidhaa hizi zitawafikia wananchi kwa bei iliyo nafuu sana. Hili ni lengo la Serikali. (Makofii)

Saba, ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi, yaani soda pamoja na kwenye maji ya matunda iliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini. Kumradhi, ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda yaliyotengenezwa kwa matunda ambayo yanayozalishwa hapa nchini utabaki kama ulivyo sasa ili kuimarisha viwanda vya ndani na pia kuimarisha uzalishaji wa maji ya matunda juice kwa kutumia matunda yanayozalishwa hapa nchini na hivyo na hivyo kuwatengenezea wakulima wa matunda hayo soko la ndani na kuiua hali zao za kiuchumi. (Makofii)

Nane, ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda yaliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini kutoka sh. 110/= kwa lita hadi Sh. 200/= kwa lita sawa na ongezeko la sh. 110/= tu kwa lita. Bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo hajaoteshwa yaani unmolted mfano Kibuku kutoka sh. 341/= kwa lita hadi sh. 375/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh. 34/= kwa lita. Bia nyiningine zote kutoka sh. 578/= kwa lita hadi sh. 694/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh. 116/= kwa lita.

Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu unaozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kisichozidi asilimia 75 kutoka sh. 160/= kwa lita hadi sh. 192/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh. 32/= tu kwa lita. Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu unaozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 kutoka sh. 1,775/= kwa lita hadi sh. 2,130/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh. 355/= kwa lita. Vinywaji vikali kutoka sh. 2,631/= kwa lita hadi sh. 3,157/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la sh. 526/= kwa lita.

Ushuru wa bidhaa kwenye samani zinazotoka nje kwa kiwango cha asilimia 15 ili kupanua wigo na kutoza ushuru kwenye samani zinazotambuliwa HS Code 9401.30 hadi HS Code 9401.80 ikiwemo viti vinavyotumika majumbani, maofisini na sehemu nyiningine zenye mkusanyiko wa watu. Mapendelekezo hayatahusu viti vya ndege pamoja na viti vya magari. Ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayozalishwa viwandani hautaongezeka. (Makofii)

Marekebisho ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara ni kama ifuatavyo:-

(a) Sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka sh. 9031/= hadi hadi sh. 11289/= kwa sigara 1,000. Hii ni sawa na ongezeko la sh. 2,258/= kwa sigara 1,000 au shilingi 2.25 kwa sigara moja.

(b) Sigara zenyе kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka sh. 21,351/= hadi sh. 26,698/= kwa sigara 1,000 ikiwa ni ongezeko la sh. 5,338/= au shilingi 5.30 kwa sigara moja.

(c) Sigara nyininge zenyе sifa tofauti na hizo nilizotajaji kwenye kifungu (a) na (b) kutoka sh. 38,628/= hadi sh. 48,285/= kwa sigara 1,000 ikiwa ni ongezeko la sh. 9,657/= sawa na shilingi 9.65 kwa sigara moja.

(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara yaani cut filler kutoka sh. 19,510/= hadi sh. 24,388 kwa kilo ikiwa ni ongezeko la sh. 4,878 kwa kilo.

Sehemu ya tano Mheshimiwa Spika yenyе vifungu 26 hadi 28. inapendekeza kufanya kufanya marekebisho katika Sheria ya Wakala wa Serikali Sura 245 kwa kuweka sharti kwamba Mashirika na Wakala wa Serikali na Mamlaka za Udhhibit yatawasilisha bajeti zao kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa uchambuzi na kupata kibali cha matumizi ya fedha zinazoombwua.

Mheshimiwa Spika, aidha, baada ya kuzingatia ushauri wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Serikali imerejesha utaratibu uliopo sasa Waziri wa Fedha kutangaza kuititia Gazeti la Serikali, Taasisi za Serikali zinazochangia Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kufanya uchambuzi wa Bajeti zao. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lengo la kurejesha hatua hii ni kutoa muda wa kupima matokeo ya utekelezaji wa Tangazo la Serikali ambalo lilichapishwa mwezi Aprili, 2014.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita yenyе vifungu 29 na 30 inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mauzo ya Nje, Sura 196 ili kupunguza kiwango cha ushuru wa mauzo ya nje unaotozwa kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi kutoka asilimia 90 na kuwa asilimia 60 au sh. 600/= kwa kilo moja ya ngozi. Marekebisho haya yanatarajiwu kuzuia biashara ya magendo ya ngozi ghafi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba yenyе vifungu 31 hadi 41, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha tatu cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 ili kutoa tafsiri ya maneno Director na Cooperation kwa lengo la kurahisha utozaji kodi kwenye ada ya mwaka ya Wakurugenzi na kujumuisha kwenye wigo wa kodi, mapato ya Taasisi na Mamlaka za Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada unapendekeza kurekebisha kifungu cha saba cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 na Jedwali la kwanza ili kutoza kodi katika ada ya mwaka wanaolipwa Wakurugenzi ili kuongeza wigo wa kodi. Vile vile inapendekezwa kurekebishiwa Jedwali la kwanza ili kupunguza kiwango cha chini cha kodi ya mapato yatokanayo na ajira kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12 ili kutoa nafuu ya kodi kwa wafanyakazi.

Pia inapendekezwa kuongeza kiwango cha chini cha kodi ya wafanyakabiashara wadogo (Presumptive Tax Payers) kutoka shilingi 100,000/= hadi shilingi 200,000/= kwenye mapato yanayozidi shilingi 400,000/= na yasiyozidi shilingi 7,500,000/=.

Kumradhi, kwenye mapato yanayozidi shilingi 4,000,000/= na yasiyozidi shilingi 7,500,000/= kwa mwaka ili kuongeza mapato ya Serikali na kuhamasisha uwekaji wa kumbukumbu za biashara na kurasimisha biashara za walipa kodi kwa ajili ya kutoza kodi kwenye faida halisi ya biashara badala ya kufanya makisio. Mapato haya yanayotajwa ni kuanzia yanayozidi shilingi 4,000,000/= na yasiyozidi shilingi 7,500,000/=.

kumbukumbu unaohamasishwa unatarajiwa kupunguza malalamiko ya kutozwa kodi kubwa mionganoni mwa wafanyabiashara wadogo na vilevile kupunguza mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kuzingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, imefanya marekebisho katika Jedwali la Pili kwa kurejesha msamaha wa kodi ya mapato yatokanayo na michezo ya kubahatisha kwa kuwa kodi hiyo hivi sasa inatozwa kwa kupitia Gaming Tax.

Aidha, msahamaha wa kodi ya mapato yatokanayo na ukodishaji wa ndege nje ya nchi umefutwa, ili kupunguza misamaha isiyokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yandalenga kutoza kodi, mapato yatokanayo na ukodishaji ndege nje ya nchi, badala ya kumsamehe kodi mlipa kodi asiye mkaazi ambaye hatimaye hulazimika kulipa kodi itokanayo na mapato hayo nchini kwake. Hii inamaanisha kwamba msamaha unaotolewa hivi sasa unasababisha uvujaji wa Pato la Taifa na kuzitajirisha Hazina za nchi za nje. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kimsingi na kwa kufuata Kanuni za Kimataifa za kodi ni kwamba, hata kama kodi hiyo ikilipwa hapa nchini, mapato hayo yaliyokatwa kodi yanatakiwa kupata punguzo la kodi katika nchi ambayo mwenye ndege ni mkaazi na kwa msingi huo msamaha unaotolewa hauhitajiki.

Kimsingi, kodi ya zuwio inayotozwa kwenye mapato yatokanayo na ukodishaji ndege nje ya nchi haiongezi gharama za biashara, kwani kisheria kodi hiyo hutozwa kwenye bei halisi walioyokubaliana. Aidha, mtindo unaotumiwa na walipa kodi kutokata kodi kwenye bei halisi na badala yake kuwalipia kodi wamiliki wa ndege hizo ni kinyume na sheria. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane yenyе vifungu 42 na 43, inapendekeza marekebisho katika Sheria za Fedha za Umma, Sura 348, kwa kuweka Sharti kwamba mashirika na wakala wa Serikali na Mamlaka za Udhibiti, watakiwe kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali Bajeti zao kwa ajili ya idhini kabla ya kuwasilishwa Bungeni ili kuimarisha udhibiti wa fedha za umma.

Aidha, utaratibu wa kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali 10% ya mapato ghafi utaendelea kutoa nafasi kwa utaratibu huu uliotangazwa kwa kupitia Gazeti la Serikali la Aprili, 2014 kutoa matokeo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa yenyе vifungu 44 na 45, inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura 220 kwa kuondoa mamlaka ya Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa ushuru wa mafuta kupitia Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura 220 isipokuwa misamaha inayotolewa kwenye mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali na washirika wa maendeleo, ili kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile miundombinu ya barabara, maji pamoja na mikataba iliyopo yaani existing agreements inayotoa misamahaka ya aina hii. Kwa sasa mamlaka hayo yako kwa Waziri wa Fedha tu na si mtu mwagine na hivyo, kuondolewa kwa mamlaka haya kunamaanisha kwamba hakuna mtu mwagine atakayeweza kutoa Misamaha hiyo. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 10, kama ilivyorekebishwa kwenye vifungu vya 46 hadi 48, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Uwezekozaji Tanzania, Sura 38, kwa kufanya marekebisho katika Kifungu cha Pili, ili kupandisha kiwango cha chini cha mtaji wa uwekezaji kutoka kiwango cha sasa cha dola za Kimarekani 300,000 kuwa Dola za Kimarekani 500,000 kwa

wawekezaji wa nje. Mtaji wa uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani unabaki kuwa dola za Kimarekani 100,000 kama ilivyo sasa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sambamba na marekebisho haya, inapendekezwa kurekebisha Kifungu cha 20 kwa kuongeza Kifungu kidogo cha nne (4), kinachoweka kiwango cha chini cha mtaji kwa wawekezaji mahiri. Kiwango kinachopendekezwa na Serikali ni dola za Kimarekani 20,000,000 kwa wawekezaji wa ndani, kiwango hiki ndicho kinachotumika kwa sasa. Aidha, inapendekezwa kuweka kiwango kipy cha dola za Kimarekani 50,000,000 kwa wawekezaji kutoka nje ya nchi. Kiwango cha dola za Kimarekani 20,000,000 kitaendelea kutumika kwa wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje kimepanda hadi dola 50,000,000. (Makof)

Mheshimiwa Spika, aidha, inapendekezwa kurekebisha Kifungu cha 19(3) ili kuondoa bidhaa za saruji, nondo na mabati katika orodha ya bidhaa zinazotfsiriwa kuwa ni bidhaa za mtaji (*deemed capital goods*) ambazo kwa sasa hupata msamaha wa kodi kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uzalishaji wa saruji, nondo na mabati pamoja na kulinda viwanda vya uzalishaji wa bidhaa hizo hapa nchini dhidi ya ushindani wa bidhaa za aina hiyo, zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Tunawahimiza wazalishaji wetu wa ndani kuchukua fursa hii kuzalisha na hivyo, bidhaa hii iwe inapatikana kutoka hapa hapa nchini kwa bei nafuu zaidi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sanjari na marekebisho haya inapendekezwa kuongeza Kifungu kidogo cha (3)(d) ili mtu ye yeyote asiruhusiwe kutoa misamaha yak di kwa miradi inayohusu upanuzi na ukarabati wa miradi inayofanywa na wawekezaji hao. Kwa sasa mamlaka hayo ya kutoa msamaha yapo kwa Waziri wa Fedha hivyo kuondolewa kwa mamlaka haya kuna maanisha kwamba hakuna mtui mwingine atakayeweza kutoa misamaha hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada unapendekeza kufuta misamaha ya kodi inayotolewa kwa makampuni ya simu isipokuwa kwa vifaa vya ujenzi wa minara ya simu. Misamaha inafutwa isipokuwa vifaa vya ujenzi wa minara ya simu, misamaha itaendela kutolewa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 11 yenye vifungu vya 48 na 49 inarejesha utaratibu uliopo hivi sasa chini ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, inayoweka sharti kwamba mashirika na wakala wa Serikali na mamlaka ya udhibiti watakiwe kuwasilisha Mfuko Mkuu wa Serikali 10% ya mapato yao ghafi ya mwaka.

Sehemu ya 12 na ya mwisho yenye vifungu vya 50 na 51 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundti Stadi, Sura ya 82 ili kuainisha katika Sheria taasisi mbalimbali zinazostahili kupata msamaha wa tozo ya ufundi stadi ambazo kwa sasa zimeainishwa katika Gazeti la Serikali Namba 15 la mwaka 1994. (Makof)

Mheshimiwa Spika, taasisi hizo ni Ofisi za Kidiplomasia, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na taasisi zake, mashirika na taasisi za nje zinazotoa misaada. Taasisi za kidini zenye watumishi walioajriwa mahsusni kuendesha ibada, mashirika yanayotoa misaada ya hiari, Serikali za Mitaa pamoja na wafanyakazi wanaofanya kazi mashambani.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Sheria inatoa msamaha kama huu kwa taasisi za umma au Idara za Serikali tu ambazo zinapata fedha 100% kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zilizobainishwa katika hotuba ya Bajeti zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia matangazo ya Serikali (*Government Notice*) kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika. Hatua hizo ni pamoja na:-

(a) Kufuta Hati Namba 21 ya mwaka 2014 inayoyataka Mashirika ya Umma, Taasisi na Mamlaka za Umma kuwasilisha 10% ya mapato ghafi (Gross Revenue) kwenye Mfuko Mkoo wa Hazina. Lengo la kufuta Hati hii ni kutokana na Marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 inayoyataka Mashirika ya Umma, Taasisi na Mamlaka ya Umma kuwasilisha kwenye Mfuko Mkoo wa Serikali malipo yote ya ziada yatakayokusanya, ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuboresha mapato ambayo sio ya kodi. (Makof)

(b) Kufuta Hati Namba 615 ya mwaka 1994 ambayo inatoa msamaha wa tozo ya Ufund Stadi kwa Ofisi za Kidiplomasia, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Tasidi zake, mashirika na taasisi za nje zinazotoa misaada, taasisi za kidini zenyet watumishi walioajiriwa mahsusui kuendesha ibada, Taasisi za Elimu na Mafunzo, Mashirika yanayotoa misaada ya hiari na Serikali za Mitaa.

Lengo la kufuta Hati hiyo ni kuwa msamaha husika, isipokuwa Taasisi za Elimu na Mafunzo imemainishwa katika Marekebisho ya Sheria ya Elimu na Ufund Stadi, Sura ya 82.

(c) Marekebisho ya Ushuru wa Forodha kwa bidhaa mbalimbali kama iliyotanganzwa kwenye Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 yatakelezwu kupitia Matangazo kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, naomba sasa Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu kwa kuupitisha ili kuhalalisha Kisheria hatua mbalimbali za kodi zilizobainishwa kupitia hotuba ya Bajeti kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaomba kutoa hoja. (Makof)

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa ijamuliwe)

**SPIKA:** Ahsante, Muswada huo umeungwa mkono. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti au mwakilishi wake atoe maoni ya Kamati ya Bajeti.

**MHE. ANDREW J. CHENG - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 88(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013 ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2014 (*The Finance Bill, 2014*).

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba tarehe 12 Juni, 2014 Waziri wa Fedha aliwasilisha Bungeni mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na alielezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali kwa madhumuni ya kuipa uwezo wa kupata mapato ya kugharamia Bajeti yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2014 pamoja na marekebisho yake una lengo la kubainisha kisheria hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ushuru kwa kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali. Hivyo, Bunge lako Tukufu linaombwa kuhalalisha kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali zitakazoanza kukusanya na Serikali kuanzia tarehe 01 Julai, 2014.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada, Kamati ya Bajeti imepokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu mapendekezo ya kuboresha Muswada huu. Kamati hii imepitia muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujelimisha maudhui ya kila kifungu.

Baada ya kujiridhisha na maudhui husika, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na mafuru na Waziri wa Fedha na watendaji wa Wizara yake kuhusu marekebisho ya Sheria kumi na moja zilizopo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchambua Muswada huo, Kamati imetoea maoni ya jumla ambayo yana lengo la kuishauri Serikali iweze kuyafikiria kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ili kuendelea kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mapato ya Serikali. Hivyo, taarifa hii ya Kamati ni matokeo ya mashauriano hayo na Serikali na ninaomba taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye Taarifa kwa ajili ya kumbukumbu yaani Hansard.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha Ya mwaka 2014, Marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara, Sura ya 25.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3, 4, 5, 6 na 7 cha Muswada ili kuweka utaratibu wa kutoa leseni za biashara zinazodumu kwa kipindi cha mwaka mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inapendekeza pia kuweka utaratibu wa kulipa ada ya leseni hiyo inapoisha muda wake. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuimarisha kumbukumbu za biashara na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii pia inapendekeza kurejesha ada kwa biashara za matawi (*Subsidiary Fee for Sub-Licence*) ambazo pindi mfanyakibashara atakapopanua biashara yake kwa kufungua tawi lingine la biashara yake, atalazimika kulipa pia ada ya leseni kwa kiwango kulingana na bidhaa anayouza na eneo tawi hilo lilipo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5 cha Muswada kinapendekeza kwamba leseni za biashara zitamaliza muda wake kila tarehe 30 Juni ya kila mwaka. Itakumbukwa kwamba, utaratibu wa kutoa leseni kwa mwaka uliwhi kutumika huko nyuma, lakini kwa kuwa ilionekana utaratibu huu unaleta usumbufu na vikwazo katika kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara nchini, Bunge lako Tukufu lilipendekeza na Serikali kuridhia kwamba ada za biashara zitolewe mara moja tu katika maisha ya biashara husika.

Hivyo, mapendekezo yanayoletwa sasa hivi yanaonesha kurejea katika utaratibu wa awali. Kamati imeishauri Serikali kwamba muda wa uhai wa leseni uwe mwaka mmoja, miaka miwili au mitatu kulingana na uamuzi wa mfanyakibashara. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Pili ni Sheria ya Ushuru wa Forodha, Sura 403. Sehemu ya Tatu ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha, Sura ya 403 kwa kurekebisha kifungu cha 194(4)(b) cha Sheria ya Ushuru wa Forodha, kwa lengo la kufuta misamaha ya kodi inayotolewa kwa makampuni ya simu isipokuwa kwa baadhi ya vifaa vya ujenzi wa minara ya simu kulingana na orodha itakayotolewa na Waziri wa Fedha baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo haya.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147. Kifungu cha 12 cha Muswada kinapendekeza kuifanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ili kuboresha adhabu

inayotolewa kwa mtu yejote atakayebainika kutengeneza bidhaa zinazotakiwa kutozwa ushuru wa bidhaa bila kibali cha mamlaka husika.

Kifungu kinapendekeza kwamba atakayebainika kufanya kosa hilo atahukumiwa kifungo cha miaka si chini ya mitatu au faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni tano ama vyote kwa pamoja. Kwa mtu anayetenda kosa mara ya kwanza na kwa mtu anayerudia kosa hilo hilo atapewa adhabu ya kifungo cha miaka isiyopungua mitano na faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni 10.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono pendekoz hili. Hata hivyo, kwa maana ya kuliboresha ili liendane na misingi ya kisheria ya kutoa adhabu, Kamati imependekeza kuwepo kwa ukomo katika kiwango cha miaka ya kifungo na faini ili kutompa Hakimu au Jaji wigo mpana wa kufanya maamuzi. Hivyo, Kamati ilipendekeza kuwepo na maneno “*isiyozi miaka...*” na pia “*isiyozi shilingi...*” fulani. Kiasi na idadi ya miaka ya ukomo inaachwa kwa Serikali na Bunge lako Tukufu kuamua.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ili kutoza ushuru wa bidhaa kwenye magari yasiyo ya uzalishaji (*non-utility motor vehicles*) na kuweka ukomo wa miaka minane kwa magari haya badala ya miaka 10. Inapendekezwa kuwa magari yenye umri wa zaidi ya miaka minane yatozwe ushuru wa bidhaa wa asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana pendekoz hili lilitewa na Serikali, lakini Bunge lako Tukufu lililikataa. Pamoja na sababu kadhaa zinazotolewa na Serikali kama kichocheo cha mabadiliko hayo, baada ya majadiliano na mashauriano na Serikali, Kamati imekubaliana na Serikali yafuatavyo:-

(i) Kwa magari yenye umri wa miaka kumi na zaidi tangu mwaka wa kutengenezwa gari, sasa yatatozwa ushuru wa bidhaa kwa uchakavu wa asilimia 30.

(ii) Kwa magari yenye umri kati ya miaka minane mpaka tisa, sasa yatatozwa ushuru wa bidhaa kwa uchakavu wa asilimia 15.

(iii) Magari yenye umri chini ya miaka minane, hayatatozwa ushuru wa bidhaa kwa uchakavu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti inatambua kuwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki Serikali zimekubaliana kupunguza uingizwaji wa magari yenye umri zaidi ya miaka minane.

Hivyo, Kamati inashauri kwamba huu ni wakati muafaka wa Serikali yetu kuangalia uwezekano wa kupunguza kodi kwa magari mapya ili Watanzania waweze kuumudu kununua magari mapya na kuachana na magari mitumba/magari chakavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 16 cha Muswada inapendekezwa kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 25 kwa bidhaa za nyumbani (*home appliances*) na maofisini zilizotumika (*used*) zinazoingizwa nchini kutoka nije ya nchi. Lengo la pendekoz hili ni zuri, hata hivyo, kwa kuwa nchi yetu haina viwanda vya kuzalisha baadhi ya bidhaa zinazolengwa na kifungu hiki, Kamati inapendekezwa kwamba vifaa vifutavyo viondolewe katika orodha ya tozo, navyo ni kompyuta mpakato (*laptops*, *monitors*, *pcs* na baiskeli kuukuu (*used*), kwa sababu ni vifaa hivi ni muhimu sana kwa shule zetu, vijana wetu, lakini pia kwa baiskeli wananchi wetu wengi hasa maeneo ya vijiji ndiyo chombo chao kikubwa cha usafiri. (*Makofii*)

Aidha, Kamati inapendekeza kuwa tozo ya ushuru wa bidhaa wa asilimia 25 kwa vifaa hivi ipunguzwe na kufikia asilimia 10. (Makof)

Mheshimiwa Spika, katika kifungu 16(6)(a), Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya ushuru wa bidhaa wa asilimia 0.15 uliokuwa unatozwa kwenye huduma ya uhaulishaji wa fedha (*money transfer*) na badala yake kutoza asilimia 10 kwenye tozo la ada ya huduma hiyo zinazotolewa na mabenki na makampuni ya simu katika uhawilishaji wa fedha. Kimsingi Kamati inakubaliana na kupongeza hatua hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 18 cha Muswada huu kinapendekeza kumwondolea mamlaka Waziri wa Fedha ya kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli isipokuwa tu misamaha inayotolewa kwenye mikataba iliyo sainiwa baina ya Serikali na washirika wa maendeleo (*Development Partners*) ili kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na kadhalika. Hatua hii ina maana kwamba hakutakuwa na mtu yeyote atakayekuwa na mamlaka ya kutoa misamaha ya kodi aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati inapongeza jithada za Serikali katika kupunguza misamaha ya kodi. Hata hivyo, kwa kutambua kuwa ipo mikataba ambayo Serikali tayari imeingia na baadhi ya makampuni, Kamati inaishauri Serikali kuheshimu mikataba hiyo ambayo ipo kabla ya sheria hii kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, sheria iliyopo sasa inampa Waziri wa Fedha mamlaka ya kuamua kutoa misamaha ya kodi ya mafuta akiona inafaa kwa manufaa ya Taifa. Kwa kuwa Serikali imeamua kufuta misamaha ya kodi, Kamati inapendekeza kwamba *discretion* ya Waziri isiondolewe kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya TRA kifungu cha 14, Bodi ya TRA ina wajibu wa kuandaa utaratibu wa kutekeleza misamaha ya kodi na kumshauri ipasavyo Waziri wa Fedha kuhusu misamaha ya kodi inayokusudiwa kutolewa. Kwa mantiki hii, Kamati ya Bajeti inapendekeza kuwa mabadiliko ya sheria yanayopendekezwa kwenye kifungu cha 18(2)(a) cha Muswada huu yafutwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mabadiliko yaliyotajwa katika vifungu vya 19, 20, 21, 22 na 24 vya Muswada huu. Hata hivyo inatoa angalizo kufanya marekebisho madogo madogo kwa upande wa maneno ya *spelling*, lugha ya uandishi na utenganisho wa aya ili kuleta maana sahihi inayokusudiwa katika marekebisho hayo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 25 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ambapo viwango mbalimbali vya ushuru wa bidhaa vinapendekezwa kubadilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Jedwali la Nne la Marekebisho, Kamati imekubaliana na Serikali kuridhia mapendekezo ya marekebisho yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Jitu Soni, Mbunge ambapo alipendekeza kufutwa kwa kiwango cha ushuru wa bidhaa kinachopendekezwa katika kichwa cha habari namba 20.09 cha shilingi 121 kwa lita kwa juisi zinazoingizwa kutoka nje ya nchi (*concentrate*) na badala yake kuweka kiwango kipywa cha shilingi 200 kwa lita. Hatua hii itasaidia kulinda wakulima wetu wa ndani wa matunda ili kutoa fursa kwa viwanda vya ndani vya usindikaji wa matunda, kununua matunda yanayolimwa na wananchi wetu kwa ajili ya usindikaji badala ya kuagiza juisi toka nje. (Makof)

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 25 cha Muswada kikisomwa pamoja na Jedwali Namba Nne la Muswada huu, kwa upande wa ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi (HS

code 22.02), Serikali inapendekeza kutoza shilingi 100 kwa lita ambalo ni ongezeko la shilingi tisa kwa lita ikilinganishwa na mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nchi za SADC ni nchi mbili tu Tanzania na Angola ndio wanatoza ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi. Hata hivyo, kwa upande wa Angola kiwango cha ushuru wa forodha kipo chini sana ni asilimia tatu tu.

Aidha, baada ya mashauriano kati ya Kamati na Serikali, Serikali imekubalina na ushauri wa Kamati wa kupunguza ushuru wa bidhaa katika vinywaji baridi kutoka shilingi 100 kwa lita hadi shilingi 55 kwa lita. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia kuongeza uwekezaji na ajira katika sekta hii muhimu, pia itatoa nafuu kwa watumiaji wa vinywaji hivi ambao wengi wao ni wananchi wa kipato cha chini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa na zabibu inayotambulika katika (HS code 22.04), Kamati inakubaliana na marekebisho ya kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo wa zabibu kutoka shilingi 1,775 hadi shilingi 1,952 kwa lita. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kufuatilia ulipwaji sahihi wa kodi kwa mvinyo wa zabibu unoagizwa kutoka nje ya nchi (concentrates) ya shilingi 1,952 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa marekebisho ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara ambavyo vimepanda kutoka asilimia 10 hadi 25, Kamati imeona kuwa ongezeko hilo ni kubwa mno, baada ya mashauriano na Serikali, Kamati imekubali Serikali iendelee na mapendekezo hayo kwa mwaka huu wa fedha kwa maelewano kwamba katika mwaka ujao wa fedha suala hili litatizamwa upya kwa madhumuni ya kushusha kiwango hiki ili kiendane na msingi uliowekwa na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa. Sheria hii ni sheria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Wakala wa Serikali (Sura ya 245) na Sheria ya Msajili wa Hazina (Sura ya 370) na Sheria ya Fedha za Umma (Sura ya 348), Kamati haijakubaliana na mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Wakala wa Serikali na Sheria ya Msajili wa Hazina kuhusu kuchukua kutoka mwenye mashirika mapato ya ziada yaani surplus. Kamati imekubaliana na Serikali kuongeza udhibiti wa mapato kutoka kwenye mashirika hayo kwa kuyataka mashirika yapeleke bajeti zao kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PayMaster General) kabla ya mwaka wa fedha kuanza ili kufanya uchambuzi na kupata kibali cha fedha zilizo kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuchukua mapato ya ziada (surplus) Kamati inashauri utaratibu wa kuchukua asilimia 10 ya mapato ghafi ya mashirika husika kama ilivyo sasa uendeleee, uimarishwe na usimamiwe kwa karibu.

Mheshimiwa spika, Sheria ya Kodi ya Mauzo ya Nje, Sura ya 196. Kamati inakubaliana na marekebisho yaliyowasilishwa na Serikali kwenye vifungu 29 na 30 kuhusu ushuru wa mauzo kwenye ngozi ghafi kutoka shilingi 900 hadi shilingi 600 kwa kilo. Kamati inaona hata hivyo, bado takwimu sahihi za uzalishaji, upatikanaji na mauzo kwa bidhaa ya ngozi hazijulikani vizuri. Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa kina kuhusu suala hili kwa kuongeza au kupunguza kiwango cha kodi sio kipimo sahihi cha kuzuia biashara ya magendo ya ngozi ghafi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332. Kwa kuwa nia ya Serikali ni kuongeza mapato, Kamati inakubaliana na marekebisho ya vifungu 31 hadi 39 vya Muswada huu. Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Kodi ya zuio ya asilimia 15 kwenye malipo ya Wakurugenzi wa Bodi kila mwisho wa mwaka (*Annual Director's Fees*) iangaliwe upya kwa kuwa kodi ya zuio (*Withholding Tax*) kwa washauri binafsi ni asilimia tano kwa kila mwisho wa mwaka.

(ii) Kwa upande wa kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12, Kamati hajjaridhika na pungozo hili, hivyo inaishauri Serikali kuendelea kupunguza kiwango hiki hadi kufikia tarakimu moja (*single digit*) kwa kuanzia mwaka ujao wa fedha.

(iii) Kwa upande wa michezo ya kubahatisha, Kamati haikukubaliana na pendekezo la Serikali la kutaka kufuta msamaha ya kodi kwenye michezo hiyo kutohaka na kuona kwamba sekta hii bado ni changa na inahitaji kulelewa na hatimaye ikue ili tuweze kupata mapato mengi. Hivyo, Kamati ilipendekeza Serikali kutohaka msamaha huo kwa michezo hiyo ili sekta hiyo iendelee kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria ya *Gaming Tax*.

(iv) Kwa upande wa ukodishaji wa ndege kwa walipa kodi wasio wakazi (*non-residents*), msamaha wa kodi ya zuio kwenye eneo hili umefutwa. Kamati inaona kuwa biashara ya usafiri wa ndege bado ni changa hivyo kuondolewa huduma hii kwa ukuaji wa sekta ya usafiri wa anga na upande wa utalii ni kupunguza uwekezaji katika sekta hii na kuongezeka kwa gharama za usafiri wa ndege.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Mafuta. Sheria iliyopo sasa inampa Waziri wa Fedha mamlaka ya kuamua kutoa msamaha wa kodi ya mafuta akiona inafaa kwa maslahi ya Taifa kwa kuzingatia ushauri atakaopewa na wataalamu wake ikiwemo Bodi ya TRA. Kamati inashauri mamlaka ya Waziri wa Fedha katika eneo hili yasiondolewe kama tulivyoshauri kwenye kifungu cha 18 cha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38. Kamati inakubaliana na marekebisho ya vifungu vya 44 hadi 47 vinavyopendekeza kupandisha kiwango cha chini cha mtaji wa uwekezaji kutoka kiwango cha sasa cha dola za Kimarekani 300,000 hadi kufikia dola za Kimarekani 500,000 kwa wawekezaji kutoka nje.

Kwa upande wa wawekezaji wa ndani kiwango kilichopendekezwa na Serikali yaani kupanda kutoka dola za Kimarekani 100,000 hadi kuwa dola za Kimarekani 300,000, Kamati ilishauriana na Serikali kiwango hicho kiendelee kubaki dola za Kimarekani dola 100,000 kama ilivyo. Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na kiwango kinachopendekezwa na Serikali cha dola za Kimarekani 20,000,000 kwa wawekezaji mahiri wa ndani na kwa wawekezaji mahiri wa nje kuwa dola za Kimarekani 50,000,000.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bidhaa za nondo na mabati ambazo hazikuwekwa kwenye orodha ya mapendekezo ya bidhaa zinazochukuliwa kuwa ni bidhaa za mtaji (*deemed capital goods*) ambazo zinazondolewa msamaha wa kodi kama ilivyofanyiwa mabadiliko saruji ambayo ilipendekezwa kuondolewa katika kundi hilo, Kamati ilishauriana na Serikali kuhusu kujumuisha bidhaa za nondo (*steel*) na mabati katika kundi la bidhaa ambazo zitaondolewa msamaha huo. Hatua hii ni muhimu katika kulinda viwanda vya ndani ambavyo vinazalisha bidhaa hizo. Hata hivyo, Kamati inapendekeza kuwa ushuru wa forodha kwenye nondo uongezwe kutoka kiwango cha asilimia 10 kilichopo sasa hadi kufikia asilimia 25, lengo ni kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani na kuongeza ajira. Nchi jirani na mwanachama mwenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imepandisha ushuru wa forodha kwenye bidhaa za nondo kutoka

asilimia 10 hadi asilimia 25 katika mwaka ujao wa fedha kwa nia ya kulinda viwanda vyake vya ndani dhidi ya uingizaji wa bidhaa za aina hiyo zinazoingizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi, Sura ya 82. Kamati inakubaliana na marekebisho ya vifungu 50 na 51 vya Muswada ambavyo vinatoa msamaha wa tozo ya ufundji stadi kwa taasisi za Kidiplomasia, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na taasisi zake, Mashirika na taasisi za nje zinazotoa misaada, taasisi za kidini zenyne watumishi walioajiriwa mahsus ikuendesha ibada na mashirika ya misaada ya hiari na Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, Kamati bado inasisisita Serikali kuendelea kupunguza kiwango cha tozo hii hadi kufikia asilimia mbili kama Serikali ilivyoahidi kwa lengo la kupunguza ghamra za uendeshaji lakini pia kuchochea ajira hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya uchambuzi wa kina wa Muswada huu na kutoa maoni kama yanavyoonekana kwenye taarifa hii, naomba kuwasilisha maoni ya jumla ambayo Serikali inaweza kuyafikiria kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa kodi za mafuta ya petroli yanayoingia nchini, Serikali inapendekeza kufuta utaratibu wa ulipaji wa kodi ya mafuta ya petroli ambao hufanyika katika siku 45 baada ya mafuta kuingizwa nchini. Hatua hii Kamati inatoa tahadhari utaleta athari zifuatazo:-

(i) Kuwaondoa katika soko kampuni za Kitanzania ndogo na zile za katika biashara ya mafuta;

(ii) Hatua hii itasababisha upungufu wa mafuta ya petroli na dizeli hasa kwa mikoa ya pembezoni;

Mheshimiwa Spika, kutohana na athari hizo, Kamati inashauri utaratibu uliopo sasa uendelee lakini usimamiwe kwa karibu. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, Kodi ya Usafirishaji Nje (*export levy*) ya mashudu na mbegu za alizeti. Katika maoni ya Kamati yaliyotolewa mwaka jana kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha, Kamati yangu ililijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania inapokea wastani wa dola za Kimarekani milioni 8.2 kila mwaka kwa kusafirisha mashudu yenye mafuta kiasi cha asilimia nne na mbegu za alizeti nje ya nchi bila ushuru wowote.

Mheshimiwa Spika, bidhaa hizi husafirishwa nje ya nchi na hutengenezewa mafuta ambayo huuzwa tena hapa nchini. Ikilinganishwa fedha inayopatikana kwa kuza nje na kununua tena bidhaa itokayo nje bidhaa hizo zikiingizwa tena nchini ni kwamba Tanzania imekuwa ikipunjika sana.

Mheshimiwa Spika, kutohana na hali hii, Kamati ilipendekeza kuanzishwa kwa kodi ya usafirishaji nje yaani *export levy* ya kiasi cha dola za Marekani 100 kwa tani ya mbegu za alizeti yenye HS Code 260630 na dola 100 kwa tani ya mashudu (*oil cake mill*) yenye HS Code 23063010 ambayo yana kiasi cha mafuta cha zaidi ya asilimia nne. Hatua hii ilikadiriwa kuingizia Serikali kiasi cha shilingi bilioni 16. Aidha, Kamati pia ilipendekeza kutenganishwa kwa HS Code ya mashudu na mbegu ili kurahisisha udhibiti wa bidhaa hizi kwa kuzuia mashudu kusafirishwa katika Code ya meal yenye mafuta chini ya asilimia nne.

Mheshimiwa Spika, Kamati ililijulisha na Serikali kwamba wangefanya utafiti suala hili na kulitumia kama chanzo cha mapato ikionekana inafaa. Kwa kuwa Kamati bado haijapokea

taarifa rasmi za matokeo ya utafiti huo, naomba kuchukua fursa hii kuiomba tena Serikali kuiangalia eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi katika bahari kuu, ni eneo mojawapo ambalo Serikali inapoteza mapato mengi kwa kutolifirkiria katika kulitumia kama chanzo cha mapato. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kulifanyia kazi kwa haraka sana eneo hili. (Makof)

Mheshimiwa Spika, shukrani, napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Napenda kumshukuru kwa dhati Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, mtoto wangu na Mheshimiwa Mwigulu Mcchemba, Mbunge kwa ushirikiano wao walioutoa katika Kamati. (Makof)

Aidha, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi hatua hii. Kamati pia inawashukuru wadau wote wa Muswada huu kwa kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati. (Makof)

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Mheshimiwa Jitu Soni, Mbunge na Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mbunge kwa mawasilisho ya majedwali ya marekesho ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kwenye maboresho ya Muswada huu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua maoni yao tumeambatisha maoni yao kwenye taarifa hii kwa ajili ya rejea ya Bunge lako Tukufu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua vifungu vya Muswada huu na kuweza kufanya maamuzi sahihi. Wamefanya kazi nzuri, kwa muda mrefu na kwa kujituma sana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah kwa namna walivyohudumia Kamati hii katika kipindi chote ambacho imekuwa ikitekeleza majukumu yake. (Makof)

Aidha, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati hii iliyongozwa na Ndugu Theonest Ruhilabake na Makatibu wa Kamati Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Kadebe na Ndugu Michael Chikokoto kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. (Makof)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante.

**TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2014 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2014 (THE FINANCE ACT, 2014)**

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 88 (1) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2013 niweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2014 (The Finance Act, 2014).

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kwamba tarehe 12 Juni, 2014, Waziri wa Fedha aliwasilisha Bungeni Mapendelekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, na kuelezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali kwa madhumuni ya kuipa uwezo wa Kupata Mapato ya kugharamia Bajeti yake kwa Mwaka ujao wa Fedha.

## **2.0. MADHUMUNI YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2014 pamoja na marekebisho yake una lengo la kubainisha kisheria hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ushuru kwa kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali. Hivyo Bunge lako Tukufu linaombwa kuhalalisha kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali zitakazoanza kukusanywa na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2014.

## **3.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti, imepokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu mapendelekezo ya kuboresha muswada huu. Kamati pia imepitia muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu. Baada ya kujiridhisha na maudhuhi husika, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Watendaji wa Wizara yake kuhusu marekebiso ya **Sheria Kumi na Moja** zilizopo kwenye Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuchambua Muswada huu, Kamati imetoa maoni ya jumla ambayo yanalengo la kuishauri Serikali iweze kuyafikiria kwa mwaka wa fedha 2015/16 ili kuendelea kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mapato kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo, taarifa hii ya Kamati ni matokeo ya mashauriano hayo na ninaomba taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye Hansard kwa ajili ya kumbukumbu.

## **4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MWAKA 2014.**

### **4.1 Marekebiso ya Sheria ya Leseni za Biashara , SURA 25.**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya Pili ya muswada inapendekeza kurekebisha **kifungu 3,4,5,6** na **7** cha Muswda ili kuweka utaratibu wa kutoa leseni za biashara zinazodumu kwa **kipindi cha mwaka mmoja tu**. Sehemu hii inapendekeza pia kuweka utaratibu wa kulipa ada ya leseni hiyo inapoisha muda wake. Madhumuni ya marekebiso haya ni kuimarisha kumbukumbu za biashara na kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii pia inapendekeza kurejesha ada kwa biashara za matawi (subsidiary fee for sub-Licence) ambapo pindi mfanyakibashara atakapopanua biashara yake kwa kufungua tawi jingine la biashara yake, atalazimika kulipa pia ada ya leseni kwa kiwango kulingana na bidhaa anayouza na eneo tawi hilo lilipo.

**Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5** cha Muswada kinapendekeza kwamba leseni za biashara zitamaliza muda wake kila tarehe 30 Juni ya kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kwamba, utaratibu wa kutoa leseni kila mwaka uliwhali kutumika miaka iliyopita, lakini kwa kuwa ilionekana utaratibu huu unaleta usumbufu na vikwazo katika kuimarisha ufanyaji biashara nchini, Bunge lako tukufu lilipendekeza na Serikali kuridhia kwamba ada za biashara zitolewe mara moja tu katika maisha ya biashara husika. Hivyo, mapendekezo yanayoletwa sasa hivi yanaonesha kurejea katika utaratibu wa awali. Kamati imeishauri Serikali kwamba, muda wa uhai wa leseni uwe mwaka mmoja, miwili au mitatu kulingana na uamuji wa mfanyabiashara.

#### **4.2 Sheria ya Ushuru wa Forodha, SURA 403**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya Tatu ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria ya Ushuru wa Forodha, Sura ya 403 kwa kurekebisha kifungu cha 194(4)(b) cha Sheria ya Ushuru wa Forodha, SURA 403, kwa lengo la kufuta misamaha ya kodi inayotolewa kwa makampuni ya simu isipokuwa kwa baadhi ya vifaa vyta ujenzi wa minara ya simu kulingana na orodha itakayotolewa na Waziri wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na mapendekezo haya.

#### **4.3 Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

**Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12** cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ili kuboresha adhabu itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayebainika kutengeneza bidhaa zinazotakiwa kutozwa ushuru wa bidhaa bila kibali cha mamlaka husika. Kifungu kinapendekeza kwamba, atakayebainika kufanya kosa hilo atahukumiwa kifungo cha miaka si chini ya mitatu au faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni tano ama vyote kwa pamoja, kwa mtu atakayetenda kosa mara ya kwanza, na kama mtu mtu huyo atarudia kosa, atafungwa kifungo cha miaka isiyopungua mitano na faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni 10.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono pendeleko hili. Hata hivyo, kwa maana ya kuliboresha ili liendane na misingi ya kisheria na haki ya binadamu, Kamati imependekeza kuwepo kwa ukomo katika viwango vyta miaka ya kifungo na faini ili kutompa Hakimu wigo mpana wa kufanya maamuzi. Hivyo Kamati ilipendekeza kuwepo na maneno " isiyozidi miaka..." na pia " isiyozidi shilingi...". Kiasi na idadi ya miaka ya ukomo inaachwa kwa Serikali kuamua.

**Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16** cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ili kutoza ushuru wa bidhaa kwenye magari yasiyo ya uzalishaji (*non-utility Motor vehicles*) na kuweka ukomo wa miaka Minane kwa magari hayo badala ya miaka 10. Inapendekezwa kuwa magari yenye umri wa zaidi ya miaka Minane yatozwe ushuru wa bidhaa wa asilimia 25.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka jana pendeleko hili lililetwa na Serikali, lakini Bunge lako tukufu liliilikataa. Pamoja na sababu kadhaa zinazotolewa na Serikali kama kichocheo cha mabadiliko haya. Baada ya majadiliano na mashauriano na Serikali, Kamati imekubaliana na Serikali yafuatayo:-

- Kwa magari yenyé umri wa miaka Kumi (10) na zaidi tangu mwaka wa kutengenezwa gari, sasa yatatozwa ushuru wa bidhaa kwa uchakavu wa asilimia 30;
- Kwa magari yenyé umri kati ya miaka Minane (8) mpaka Tisa (9), sasa yatatozwa ushuru wa bidhaa kwa uchakavu asilimia Kumi na Tano (15)
- Magari yenyé umri chini ya miaka Minane (8), hayatatozwa ushuru wa bidhaa kwa uchakavu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti inatambua kuwa katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wamekubaliana kupunguza uingizwaji wa magari yenyé umri zaidi ya miaka minane. Hivyo, Kamati inashauri kwamba huu ni wakati muafaka wa kupunguza kodi kwa magari mapya ili watanzania waweze kuumudu kununua magari mapya na kuachana na magari chakavu.

**Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 16** cha Muswada inapendekezwa kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 25 kwa bidhaa za nyumbani (*home appliances*) na maofisini zilizotumika (*used*) zinazoingizwa nchini toka nje ya nchi. Lengo la pendekezo hili ni zuri, hata hivyo, kwa kuwa ni dhahiri kwamba nchi yetu haina viwanda vya kuzalisha baadhi ya bidhaa zinazolengwa na kifungu hiki. Kamati inapendekezwa kwamba vifaa vifutavyo viondolewe katika orodha ya tozo:- Kompyuta Mpakato (*laptops*), Monitors, PCs na balskeli kuukuu (*used*), kwa sababu ni vifaa muhimu vinavyotumika katika mashule na wananchi hasa wa maeneo ya vijijini. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa tozo ya ushuru wa bidhaa wa asilimia 25 kwa vifaa hivi ipungue na kufikia asilimia 10.

**Mheshimiwa Spika, katika kifungu 16(6A),** Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya ushuru wa bidhaa wa asilimia 0.15 uliokuwa unatozwa kwenye huduma za uhaulishaji wa fedha (*money transfer*) na badala yake kutoza asilimia 10 kwenye tozo na ada ya huduma hiyo zinazotolewa na mabenki na makampuni ya simu katika uhawilishaji wa fedha. Kimsingi Kamati inakubaliana na kupongeza hatua hii.

**Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 18 (2A)** cha muswada huu kinapendekeza kumwondolea mamlaka Waziri wa Fedha ya kutoa msamaha wa Ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya Petroli isipokuwa tu misamaha inayotolewa kwenye mikataba iliyo sainiwa baina ya Serikali na washirika wa maendeleo (*Development Partners*) ili kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji nk. Hatua hii ina maana kwamba hakutakuwa na mtu yoyote atakayekuwa na mamlaka ya kutoa misamaha ya kodi aina hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati inapongeza jitihada za Serikali katika kupunguza misamaha ya kodi. Hata hivyo, kwa kutambua kuwa ipo mikataba ambayo Serikali tayari imeingia na baadhi ya makampuni, Kamati inashauri Serikali kuheshimu mikataba hiyo ambayo ipo kabla ya sheria hii kuanza kutumika.

**Mheshimiwa Spika,** sheria iliyopo sasa inampa Waziri wa Fedha Mamlaka ya Kuamua kutoa misamaha ya kodi ya mafuta akiona inafaa. Kwa kuwa Serikali imeamua kufuta misamaha ya kodi, Kamati inapendekeza kwamba discretion ya Waziri isiondolewe, kwa kuwa kwa mujibu wa sheria ya TRA,(kifungu cha 14) Bodi ya TRA ina wajibu wa kuandaa utaratibu wa kutekeleza misamaha ya kodi na kumshauri ipasavyo Waziri wa Fedha kuhusu misamaha ya kodi inayokusudiwa kutolewa. Kwa mantiki hii, Kamati ya bajeti inapendekeza kuwa mabadiliko ya sheria yanayopendekezwa kwenye **kifungu cha 18 (2A)** cha Muswada huu yafutwe.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mabadiliko yanayofanywa katika **kifungu 19,20,21,22 na 24** vya Musawda huu. Hata hivyo inatoa angalizo kufanya marekebisho madogo

madogo kwa upande wa maneno (*spelling*), lugha ya kiuandishi na utenganisho wa aya ili kuleta maana sahihi inayokusudiwa katika marekebisheso hayo.

**Mheshimiwa Spika, kifungu cha 25** cha Muswada, kinapendekeza kufanya marekebisheso katika jedwali la nne la Sheria ya Ushuru wa bidhaa ambapo viwango mbalimbali vya ushuru wa bidhaa vinapendekezwa kubadilishwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika jedwali la nne la marekebisheso, Kamati imekubaliana na Serikali kuridhia mapendekezo ya marekebisheso yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Jitu Soni, Mb, ambapo alipendekeza kufutwa kwa kiwango cha ushuru wa bidhaa kinachopendekezwa katika kichwa cha habari **namba 20.09** cha shilingi 121 kwa lita kwa juisi zinazoingizwa toka nje ya nchi (concentrate) na badala yake kuweka kiwango kipywa cha shilingi 200 kwa lita. Hatua hii itasaidia kulinda wakulima wetu wa ndani wa matunda, ili kutoa fursa kwa viwanda vya ndani vya usindikaji wa matunda kununua matunda yanayolimwa na wananchi kwa ajili ya usindikaji badala ya kuagiza juisi toka nje.

**Mheshimiwa Spika**, katika **kifungu cha 25 cha** muswada kikisomwa pamoja **na jedwali namba Nne (4) la Muswada**; Kwa upande wa ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi (HS code 22.02), Serikali inapendekeza kutoza shilingi 100 kwa lita, ambalo ni ongezeko la shilingi tisa kwa lita ikilinganishwa na mwaka jana. **Kwa upande wa nchi za SADC, Tanzania na Angola tu ndio wanatoza ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi**. Aidha, baada ya mashauriano kati ya Kamati na Serikali, Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati wa kupunguza ushuru wa bidhaa katika vinywaji baridi kutoka shilingi 100 kwa lita hadi shilingi 55 kwa lita. Hatua hii itasaidia kuongeza uwekezaji na ajira katika sekta hii, pia itatoa nafuu kwa watumiaji wa vinywaji hivi ambaeo wengi wao ni wananchi wa kipato cha chini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa na zabibu (**HS code 22.04**), Kamati inakubaliana na marekebisheso ya kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo wa zabibu kutoka shilingi 1775 hadi shilingi 1952 kwa lita. Hata hivyo Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kufuatilia ulipwaji sahihi wa kodi kwa mvinyo wa zabibu unaoagizwa kutoka nje ya nchi (concentrates) ya shilingi 1952 kwa lita.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa marekebisheso ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara ambavyo vimepanda kutoka asilimia 10 hadi 25, Kamati imeona kuwa ongezeko hilo ni kubwa mno. Baada ya mashauriano na Serikali, Kamati imekubali Serikali iendelee na mapendekezo hayo kwa mwaka huu wa fedha kwa maelewano kwamba katika mwaka ujao wa fedha suala hili litatizamwa upya kwa madhumuni ya kushusha kiwango hiki ili kiendane na msingi uliowekwa na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa.

#### **4.4 Sheria ya Wakala wa Serikali (SURA 245); Sheria ya Msajili wa Hazina (SURA 370) na Sheria ya Fedha za Umma (SURA 348)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijukubaliana na mapendekezo ya mabadiliko ya **Sheria ya Wakala wa Serikali (SURA 245)** na **Sheria ya Msajili wa Hazina (SURA 370)** kuhusu kuchukua kutoka mwenye mashirika mapato ya ziada (*surplus*). Kamati imekubaliana na Serikali kuongeza udhibiti wa mapato kutoka kwenye mashirika haya kwa kuyataka mashirika yapeleke bajeti zao kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kabla ya mwaka wa fedha kuanza ili kufanya uchambuzi na kupata kibali cha fedha zilizo kwenye bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu kuchukua mapato ya ziada (*surplus*) Kamati inashauri utaratibu wa kuchukua asilimia 10 ya mapato ghafi ya mashirika husika uendelee na uimarishwe.

#### **4.5 Sheria ya Kodi ya Mauzo ya Nje, SURA 196**

**Mheshimiwa spika**, Kamati inakubaliana na marekebisho yaliyowasilishwa na Serikali kwenye **vifungu 29 na 30** kuhusu ushuru wa mauzo kwenye ngozi ghafi kutoka shilingi 900 hadi 600 kwa kilo. Kamati inaona hata hivyo, bado takwimu sahihi za uzalishaji, upatikanaji na mauzo kwa bidhaa ya ngozi hazijulikani vizuri. Kamati inashauri Serikali kufanya utafiti wa kina kuhusu suala hili kwa kuwa kuongeza au kupunguza kiwango cha kodi sio kipimo sahihi cha kuzuia biashara ya magendo ya ngozi ghafi.

#### **4.6 Sheria ya Kodi ya Mapato , SURA 332**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa nia ya Serikali ni kuongeza mapato, Kamati inakubaliana na marekebisho ya **vifungu 31 hadi 39** vya Muswada huu. Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

- i) Kodi ya zuio ya asilimia 15 kwenye malipo kwa wakurugenzi wa bodi kila mwisho wa mwaka (*Annual Director's Fees*) iangaliwe upya kwa kuwa, Kodi ya zuio (WHT) kwa washauri binafsi ni asilimia 5 kwa kila mwisho wa mwaka.
- ii) Kwa upande wa kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12. Kamati haijaridhika na pungozo hili, hivyo inashauri Serikali kuendelea kupunguza kiwango hiki hadi kufikia tarakimu moja (single digit) kwa mwaka ujao wa fedha.
- iii) Kwa upande wa michezo ya kubahatisha, Kamati haikukubaliana na pendekoz la Serikali la kufuta msamaha wa kodi kwenye michezo hiyo kutokana na kuona kwamba sekta hii ni changa na inahitaji kukua. Hivyo, Kamati ilipendekeza Serikali kutofuta msamaha huo kwa michezo hiyo ili sekta hiyo iendelee kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria ya Gaming tax.
- iv) Kwa upande wa ukodishaji wa ndege kwa walipa kodi wasio wakazi (*non residents*), msamaha wa kodi ya zuio kwenye eneo hili umefutwa. Kamati inaona kuwa biashara ya usafiri wa ndege bado ni changa hivyo kuondolewa kudumaa kwa ukuaji wa sekta ya usafiri wa anga, kupunguza uwekezaji katika sekta hii na kuongezeka kwa ghamama za usafiri wa ndege.

#### **4.7 Sheria ya Ushuru wa Mafuta, SURA 220**

**Mheshimiwa Spika**, sheria iliyopo sasa inampa Waziri wa Fedha mamlaka ya kuamua kutoa msamaha wa kodi ya mafuta akiona inafaa kwa maslahi ya Taifa kwa kuzingatia ushauri atakaopewa na wataalamu wake ikiwemo Bodi ya TRA. Kamati inashauri mamlaka ya Waziri wa Fedha katika eneo hili yasiondolewe kama tulivyoshauri kwenye Kifungu cha 18 cha Muswada huu.

#### **4.8 Sheria ya Uwekezaji Tanzania, SURA 38**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na marekebisho ya **vifungu vya 44 hadi 47** vinavyopendekeza kupandisha kiwango cha chini cha mtaji wa uwekezaji kutoka kiwango cha sasa cha Dola za kimarekani laki tatu (USD 300,000 ) hadi kufikia Dola za Kimarekani laki tano (USD 500,000) kwa wawekezaji kutoka nje. Kwa upande wa wawekezaji wa ndani kiwango kilichopendekezwa na Serikali kupanda kutoka Dola za Kimarekani laki moja hadi kuwa Dola za Kimarekani laki tatu, Kamati ilishauriana na Serikali kiwango hicho kiendelee kubaki Dola za Kimarekani laki moja (USD 100,000) kama ilivyo sasa. Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na kiwango kinachopendekezwa na Serikali cha Dola za Kimarekani milioni ishirini (USD 20,000,000) kwa wawekezaji mahiri wa ndani na kwa wawekezaji mahiri wa nje kuwa Dola za Kimarekani milioni hamsini (USD 50,000,000).

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa bidhaa za nondo na mabati ambazo hazikuwekwa kwenye orodha ya mapendekezo ya bidhaa zinazochukuliwa kuwa ni bidhaa za mtaji, (deemed capital goods) ambazo zinazondolewa msamaha wa kodi kama ilivyofanyiwa mabadiliko saruji ambayo ilipendekezwa kuondolewa katika kundi hilo, Kamati ilishauriana na Serikali kuhusu kujumuisha bidhaa za nondo (*steel*) na mabati katika kundi la bidhaa ambazo zitaondolewa msamaha huo. Hatua hii ni muhimu, katika kulinda viwanda vya ndani ambavyo vinazalisha bidhaa hizo. Hata hivyo, Kamati inapendekeza kuwa, ushuru wa forodha kwenye nondo uongezwe kutoka kiwango cha **asilimia 10** kilichopo sasa hadi kufikia **asilimia 25**, lengo ni kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani na kuongeza ajira. Nchi jirani ya Kenya imepandisha ushuru wa forodha kwenye bidhaa za nondo kutoka **asilimia 10** hadi **asilimia 25** kwa nia ya kulinda viwanda vyake vya ndani dhidi ya uzalishaji wa bidhaa za aina hiyo zinazoingizwa kutoka nje.

#### **4.9 Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, SURA 82**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na marekebisho ya vifungu 50 na 51 vya Muswada huu ambavyo vinatoa msamaha wa tozo ya ufundu stadi kwa taasisi za Kidiplomasia, mashirika ya Umoja wa Mataifa na taasisi zake, Mashirika na taasisi za nje zinazotoa misaada, taasisi za kidini zenye watumishi walioajiriwa mahsus ikuendesha ibada na mashirika ya misaada ya hiari na Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, Kamati bado inasitisiza Serikali kuendelea kupunguza kiwango cha tozo hii hadi kufikia asilimia 2 kama Serikali ilivyoahidi kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji kwa wanaostahili kulipa tozo hii. Hatua hii itaongeza kukubalika (*compliance*) kwa tozo hii.

### **5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Muswada huu na kutoa maoni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa hii, naomba kuwasilisha maoni ya jumla ambayo Serikali inaweza kuyafikiria kwa siku zijazo.

#### **5.1 USIMAMIZI WA KODI ZA MAFUTA YA PETROLI YANAYOINGIZWA NCHINI**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapendekeza kufuta utaratibu wa ulipaji wa kodi ya mafuta ya petroli ambao hufanyika katika siku 45. Hatua hii italeta athari zifuatazo:-

- (i) Kuwaondoa katika soko makampuni madogo na ya kati katika biashara ya mafuta;
- (ii) Upungufu wa mafuta hasa kwa mikoa ya pembezoni;

Kutokana na athari hizo, Kamati inashauri utaratibu uliopo sasa uendelee.

#### **5.2 KODI YA USAFIRISHAJI NJE (*EXPORT LEVY*) YA MASHUDU NA MBEGU ZA ALIZETI**

**Mheshimiwa Spika**, katika maoni ya Kamati yaliyotolewa mwaka jana kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha, Kamati yangu ililijulisha Bunge lako kwamba Tanzania inapokea wastani wa dola za Kimarekani milioni 8.2 kila mwaka kwa kusafirisha mashudu yenyе mafuta kiasi cha

asilimia 4 na mbegu za alizeti nje ya nchi bila ushuru wowote. Bidhaa hizi husafirishwa nje ya nchi na hutengenezewa mafuta ambayo huuzwa tena nchini. Ikilinganishwa fedha inayopatikana kwa kuza nje na kununua tena bidhaa itokanayo na bidhaa hizo zikiingizwa tena nchini, ni kwamba Tanzania imekuwa ikipunjika sana.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hii, Kamati ilipendekeza kuanzishwa kwa kodi ya usafirishaji nje (*export levy*) ya kiasi cha dola za Marekani 100 kwa tani ya mbegu za alizeti (*sunflower seed*) yenye HS Code 260630 na dola 100 kwa tani ya mashudu (*oil cake mill*) yenye HS Code 23063010 ambayo yana kiasi cha mafuta cha zaidi ya asilimia 4. Hatua hii ilikadiriwa kuiingizia Serikali kiasi cha **shilingi bilioni 16**.

Aidha Kamati pia ilipendekeza kutenganishwa kwa HS Code ya Mashudu na Mbegu ili kurahisisha udhibiti wa bidhaa hizi kwa kuzuia mashudu (Cake) kusafirishwa katika Code ya Meal yenye mafuta chini ya asilimia nne.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa na Serikali kwamba wangefanyia utafiti suala hili na kulitumia kama chanzo cha mapato ikionekana inafaa. Kwa kuwa Kamati bado haijapokea taarifa rasmi za matokeo ya utafiti huo, naomba kuchukua fursa hii kuiomba tena Serikali kuiangalia fursa hii.

### 5.3 UVUVI KATIKA BAHARI KUU

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu uvuvi katika bahari kuu, ni eneo mojawapo ambalo Serikali inapoteza mapato mengi kwa kutolifirkiria katika kulitumia kama chanzo cha mapato. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufanya kazi eneo hili.

### 6.0 SHUKRANI

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Fedha, Mhe. Saada Mkuya Salum, Mb Naibu Mawaziri wake Mhe. Kigoma Malima, Mb na Mhe. Mwigulu Mchemba, Mb kwa ushirikiano wao waliloutoa kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi hatua hii. Kamati pia inawashukuru wadau wote wa Muswada huu kwa kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa namna ya pekee napenda kuwashuru Mhe. Jitu V. Soni (Mb) na Mhe. Murtaza A. Mangungu (Mb) kwa mawasilisho ya majedwali ya marekesho ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kwenye maboresho ya Muswada huu. Kwa kutambua maoni yao tumeambatisha maoni yao kwenye taarifa hii kwa ajili ya rejea ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua vifungu vya Muswada huu na kuweza kufanya maamuzi sahihi. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo.

- |                              |   |              |
|------------------------------|---|--------------|
| 1. Mhe. Andrew J. Chenge, Mb | - | Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Dr Festus Limbu, Mb  | - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Amina Amour, Mb      | - | Mjumbe       |
| 4. Mhe. Dr. Cyril Chami, Mb  | - | "            |
| 5. Mhe. Mansoor Hiran, Mb    | - | "            |

6. Mhe. Josephat Kandege, Mb	-	"
7. Mhe. Christina M. Lissu, Mb	-	"
8. Mhe. Dr. Goodluck Ole Medeye	-	"
9. Mhe James Mbatia, Mb	-	"
10. Mhe Assumpter Mshama, Mb	-	"
11. Mhe. Hamad Rashid, Mb	-	"
12. Mhe. Kidawa Saleh, Mb	-	"
13. Mhe. Joseph Selasini, Mb	-	"
14. Mhe. Saleh Pamba, Mb	-	"
15. Mhe Godfrey Mgimwa, Mb	-	"
16. Mhe Beatrice Shelukindo, Mb	-	"
17. Mhe Ritha Mlaki, Mb	-	"
18. Mhe John Cheyo, Mb	-	"
19. Mhe Peter Serukamba, Mb	-	Mjumbe Mshiriki

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah kwa namna mlivyoihudumia Kamati hii katika kipindi chote ambacho imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Aidha, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati hii iliyoongozwa na Ndugu Theonest Ruhilabake, na Makatibu wa Kamati ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Kadebe na Ndugu Michael Chikokoto kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Muswada huu.

Andrew J. Chenge, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

**27 Juni, 2014**

**JEDWALI LA ORODHA YA MAPENDEKEZO YA MABADILIKO YA SHERIA YALIYOWASILISHWA NA WAHESHIMIWA WABUNGE  
KWA KAMATI YA BAJETI NA NAMNA YALIVYOSHUGHULIKIWA**

S/N	Mto a Hoja	Sehemu ya Muswada inayopendekezwa Kubadilishwa	Mababiliiko yanayopendekezwa	Jinsi ya lillyo shughuli kwa												
1.	Mhe. Jitu Soni, Mb	Clause 7 is amended in the First Schedule by:-	<p>1. Adding another S/N 38 which will be as follows;</p> <table border="1"> <thead> <tr> <th>S/N</th><th>COLUMN 1</th><th>COLLU MN 11</th><th>PRIN CIPAL</th></tr> </thead> <tbody> <tr> <td></td><td>BUSINESS CATEOGORY</td><td>DESCRIPTION OF THE BUSINESSES</td><td>FEE FOR PRINCIPAL LICENSE</td></tr> <tr> <td>38</td><td>Agriculture Business</td><td>For all registered agriculture farms</td><td>50,00 0/=</td></tr> </tbody> </table> <p>2. Deleting S/N 31 describes as "1. Motor vehicle 2. Motor cycle and 3. Bicycle" and substituting for it "Auto Spare and hardware"            (a) City Municipal            (b) District            (c) Minor settlement and village"</p> <p>3. Deleting The new fee for principal licence and fee for sub-liscence finance described "10 Silver and gold Smith dealer and Substituting for it the following new fees            (a) City/Municipal fee for principal licence 200,000/= instead of 300,000/=, fee for Sub-liscence finance 150,000/= instead of 200,000/-            (b) District/town fee for principal license 150,000/= instead of 250,000/=, fee for sub-liscence finance 100,00/= instead of 200,000/=            (c) Minor settlement and village 100,000/= and fee for sub-license finance 50,000/= instead of 80,000/=</p>	S/N	COLUMN 1	COLLU MN 11	PRIN CIPAL		BUSINESS CATEOGORY	DESCRIPTION OF THE BUSINESSES	FEE FOR PRINCIPAL LICENSE	38	Agriculture Business	For all registered agriculture farms	50,00 0/=	Pendekezo hili halikuchukuliwa
S/N	COLUMN 1	COLLU MN 11	PRIN CIPAL													
	BUSINESS CATEOGORY	DESCRIPTION OF THE BUSINESSES	FEE FOR PRINCIPAL LICENSE													
38	Agriculture Business	For all registered agriculture farms	50,00 0/=													
				Serikali ilieleza kwamba pendekezo hili linajibowi katika eneo la general merchanising. Hata hivyo Kamati ilipendekeza kuwa mababiliiko yanayopendekezwa yafanyiwe kazi siku zijazo.												
				Pendekezo hili halikubaliwa. Hata hivyo Serikali imehidi kulichukua na itafanya kazi.												
		Clause 25 is amended in the Fourth Schedule by:-	Deleting the new excise rates of Tshs. 121 per litre describe as "Imported fruit juices (including grape must) and vegetable and not containing added spirit, whether or not containing added sugar or other sweetening matters" under Heading 20.09 and substituting for it the excise rate of "Tshs 200 per litre".	Pendekezo hili illikubaliwa na imewekwa katika muswada												
		Clause 16 (5C)	deleting the words "PCs, Monitors, Laptops, Cartridges, Printers and Photocopiers" appearing on the last line from the bottom	Pendekezo hili illipokelewa, na Serikali imeshauriwa kulfanya kazi.												
2.	Mhe. Jitu Soni, Mb	Clause 45 (b) is amended by	deleting " not less than Tanzanian shillings equivalent to three hundred thousand US dollars ( USD 300,000)" and substituting for it immediately after capital " is not less than Tanzanian Shillings equivalent to two hundred thousand US dollars ( USD 200,000)	Pendekezo hili illiboreshwana na Kamati kwa kushauriana na Serikali kama inavyoonekana kwenye Muswada sasa.												

3.	Mhe. Jitu Soni, Mb	Clause 51	Adding immediately after Clause 19(e)(ii) the following : (iii) administer education services (iv) administer Health Services		Pendekazo limeoneshwa kuwepo katika kifungu cha 19(f)cha Sheria inayofanyiwa marekebisho.		
4.	Mhe. Murtaza Mangungu, Mb	Clause 25	In clause 25 in the fourth Schedule by inserting the following HS CODES immediately after the item 8523, HS CODE 8423.40.90 and amend the inserted HS CODES as follows:-		Kamati ilijulishwa na Serikali kwamba LABSA ni raw material na hivyo katika hali ya kawaida haitozwi ushuru wa torodha. Kamati pia ilijulishwa na mtoa hoja kwamba LABSA inayozalishwa hapa nchini inatosheleza mahitaji ya ndani. Kamati ilishauri Serikali kwa ujumla wake ilifanyie kazi suala hili.  Mto a hoja aliondoa sehemu ya pili ya hoja ya mabadiliko		
			HEADING	HS CODE	DESCRIPTION	UNIT	EXCISE RATE
				HS CODE 3402.11 .00 3402.12 .00 3402.19 .00	LABSA		10 percent per
				3808.91 .39	Insect pesticides made by petrol eum oil	litre	15 percent per
5	Mhe. Jitu Soni, Mb	Anapendekiza kuongewa kwa sehemu mpya ya XIII kurekebisha Sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa ( <b>THE LOCAL GOVERNMENT FINANCE ACT, CAP (290)</b> )	<p>"This part shall be read as one with the local Government finance Act, hereafter referred as the "Principal Act"</p> <p>1. Section 35 is amended by adding the words "except unprocessed Agriculture products" immediately after the words "excise duty"</p>		Hoja hii halikuafikiwa. Serikali imeshauri mto a hoja kuwa suala hili litaathiri moja kwa moja mapato ya halmashauri. Kwa sababu hiyo Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na mto a hoja walishughulikie suala hili kwa pamoja na TAMIEMI ili kufanya mabadiliko katika mwaka wa fedha unaofuata.		
			<p>2. Section 47 is amended in the third Schedule.</p> <p>A. In Item 31 by adding the word "tube" between the words "supply of" and "factors"</p> <p>B. In Item 30 by adding the words "dealers" and "Suppliers" immediately after the word farms</p>		Hoja hii halikuafikiwa. Serikali imeshauri mto a hoja kuwa suala hili litaathiri moja kwa moja mapato ya halmashauri. Kwa sababu hiyo Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na mto a hoja walishughulikie suala hili kwa pamoja na TAMIEMI ili kufanya mabadiliko katika mwaka wa fedha unaofuata.		

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu Serikali imependekiza kurekebisha Sheria mbalimbali, nimezitaja kwa ajili ya muda sitazisoma.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu linatunga Sheria ya Fedha ya mwaka 2014 ikiwa imebaki mwaka mmoja tu kwa Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Nne kumalizia kipindi chake cha pili cha uongozi.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa miaka yote minne ya kipindi cha pili cha Awamu ya Nne, imekuwa ikiishauri Serikali kuachana na kasumba ya kuleta Miswada ya Fedha Bungeni inayopendekeza vyanzo vilevile vya kijadi vya mapato ya Serikali. Vyanzo hivyo vya kijadi vya mapato yaani *traditional sources of revenue* ni pamoja na kutoza ushuru katika vinywaji baridi na vikali kama vile soda, juisi na pombe za cina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kugandamiza tabaka la wafanyakazi kupitia kodi ya mapato yaani Pay As You Earn ambayo inatozwa kwa kiwango kikubwa kuliko nchi zote za Afrika Mashariki huku utozaji huo wa kodi ukiwa hauendani na kupanda kwa gharama za maisha, upatikanaji wa huduma za msingi kwa Watanzania walio wengi ikiwemo huduma duni za afya, mfumo dhaifu wa elimu, viwango duni vya miundombinu, ukosefu wa ajira na kadhalika. Athari za hali hii ni kuendelea kuwabebesha Watanzania walio wengi mzigo mkubwa wa kodi ili kukidhi matumizi makubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa miaka takribani tisa iliyopita yaani tangu mwaka 2005 hadi sasa imekuwa ikipendekeza kwa Serikali vyanzo mbadala vya mapato ambavyo havimkandamizi mwananchi wa kawaida. Jambo la kushangaza ni kwamba Serikali mara zote imekuwa ikisita kuchukua mapendekezo hayo na kuendelea na vyanzo vilevile ambavyo ni kandamizi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ulioiunda ya kuisadia Serikali kubuni vyanzo vipyta vya mapato na kutoa taarifa yake kwako maarufu kama *Chenge I Report* na ripoti ya wataalam wa Serikali ya Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa yaani *Big Results Now* iliyohusu kubuni vyanzo vipyta vya mapato, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza ripoti zote mbili ziletwe hapa Bungeni ili ziweze kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge na kuazimia namna bora ya utekelezaji wake. (*Makofii*)

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuna mapungufu ya Kikatiba ambayo yanayozua chombo chochote, isipokuwa Mamlaka ya Rais kutoza kodi, hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 99 na Ibara ya 138(1). Ibara hizo zimelifunga mikono Bunge lako Tukufu, kwani mapendekezo yote ambayo yapo kwenye ripoti ya *Chenge I* ingekuwa ni rahisi kuyahalalisha kisheria na Bunge lako Tukufu.

Katiba tuliyo nayo sasa imetufunga mikono na huu ni mmojawapo wa udhaifu mkubwa wa mgawanyo wa madaraka. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliomba Bunge lako Tukufu kuangalia udhaifu huu wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu vyanzo mbadala vya mapato ambavyo havijafanyiwa kazi kikamilifu ni kama ifuatavyo:-

Moja, kodi ya majengo yaani *Property tax*. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tulipendekeza kuwa Serikali ianzishe Mamlaka ya Udhibiti wa Majengo (*Real Estate Regulatory Authority*) ili sekta ya nyumba iweze kuratibiwa vizuri na kuiingizia Serikali mapato. Kwa makisio ya chini Sekta Ya Nyumba ikisimamiwa vizuri, Serikali inaweza kukusanya zaidi ya shilingi trilioni moja kwa mwaka.

Mbili, Usimamizi wa makusanyo katika bandari zetu, hususan Bandari ya Dar es Salaam, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikishauri mara kwa mara kwamba, ikiwa vigezo vya ufanisi na kuaminika vitazingatiwa kwa uboreshaji wa asilimia 50 tu ya Bandari ya Dar es Salaam, basi Serikali itawenza kuongeza mapato yake kwa kiasi kinachokadirwa shiliini trilioni 1.44 kwa mwaka. Hii ni kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia ya mwaka 2013.

Tatu, kodi kutokana na uvuvi katika Bahari Kuu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipendekeza kuwa Serikali itoze angalau mrabaha wa asilimia tano katika mapato yanayotokana na uvuvi wa samaki katika bahari kuu. Inakadiriwa kwamba Serikali inaweza kupata mapato ya zaidi ya shilingi trilioni moja kwa mwaka ikiwa sekta hii kwa ujumla wake itasimamiwa kikamilifu.

Nne, kupunguza misamaha ya kodi kama njia ya kuongeza mapato ya Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri Serikali kupunguza misamaha ya kodi isiyokuwa na tija hadi kufikia angalau asilimia moja ya pato la taifa. Kwenye eneo hili la misamaha ya kodi isiyokuwa na tija ya kukuza na kuendeleza uchumi wetu Serikali inaweza kuongeza mapato yake hadi kufikia takribani shilingi trilioni 1.386 kwa mwaka.

Tano, kudhibiti ukwepaji wa kodi na udanganyifu. Takwimu zilizofanyiwa utafiti na taasisi mbalimbali zinaonesha kwamba takribani shilingi trillioni 1.9 kwa mwaka hupotea kutokana na udanganyifu na ukwepaji wa kodi.

Sita, vyanzo vingine vya mapato kwa mfano, utalii, uwindaji wa kitalii pekee unachangia mapato ya shilingi takribani shilingi bilioni 70 kwa mwaka. Mauzo ya mazao ya misitu yanachangia mapato ya shilingi bilioni 220.4.

Mheshimiwa Spika, (b) kuongeza ufanisi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kutaongeza mapato ya Serikali yanayokadiriwa kuwa shilingi bilioni 708.1 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, (c) kodi ya asilimia moja kwa manunuzi yote ya nje na tozo ya asilimia 0.5 ya mauzo yote ya nje kwa ajili ya ukarabati wa reli kutachangia mapato ya Serikali kwa takribani shilingi bilioni 226.1.

Mheshimiwa Spika, aidha, vipo vyanzo vingine vya mapato kwa mfano tozo mbalimbali na mirabaha katika sekta ya uchimbaji wa madini, michango ya kisheria ya taasisi na makampuni ya kibiashara ya Serikali kama vile TANAPA, EWURA, TCRA, Ngorongoro Conservation Area Authority na kadhalika.

(b) Kuongeza thamani madini yote ya vito hapa nchini badala ya kuuza madini hayo yakiwa ghafi. Taasisi hizi zinatakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha namba 13 ya mwaka 2008 pamoja na Waraka wa Hazina namba 8 wa mwaka 2008/2009 kuchangia mapato yao katika Mfuko Mkuu wa Serikali (*Consolidated Fund*). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu ni taasisi ngapi zilitimiza sharti hili la kisheria la kuchangia asilimia 10 ya mapato yake ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuondoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali katika Muswada huu wa Sheria wa mwaka 2014 yanayolenga kutoza kodi katika vyanzo vilevile vya mapato na badala yake tunawaomba Waheshimiwa Wabunge walete majedwali ya marekebisho katika Jedwali la Marekebisho la Serikali ili kutoa mapendekezo ya vyanzo vipyta vya mapato tulioainishwa hapo juu na vyanzo vingine watakavyo viona kwa kutumia busara zao.

Mheshimiwa Spika, inakuwa vigumu kwa Waheshimiwa Wabunge kuelewa kiasi halisi kitakachopatikana kwa kila kifungu kinachofanyiwa marekebisho, mfano, kwa marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147 inahusisha bidhaa nyingi lakini imetolewa jumla kuu tu kuwa Serikali itakusanya shilingi bilioni 124.292. Kwa utaratibu huu unasababisha Waheshimiwa Wabunge kushindwa kukidhi matakwa ya Kanuni ya 109(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2013.

Mheshimiwa Spika, sera za kodi na ukuaji wa uchumi. Lengo kuu la kodi mahali popote kwanza ni kuchochea maendeleo endelevu kwa walipa kodi wake, kukuza uchumi na kukuza utu wa mlipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali hutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa kutumia fedha hususani za walipa kodi wake. Ni jambo la kusikitisha kuwa sera za kodi hapa Tanzania kwa kiasi kikubwa zinakusudia zaidi ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya muda mfupi, hususan mwaka mmoja. Mfumo huu kwa kiasi kikubwa unaondoa dhamira na kufisha utashi wa kila mlipa kodi katika ufuatiliaji wa matumizi sahihi ya kodi yake.

Mheshimiwa Spika, katika Dira ya Taifa ya mwaka 2025, Tanzania imejiwekea malengo ya kuwa na uchumi wa kipato cha kati, kuongeza kiwango cha maendeleo ya watu, kuwa na

uchumi wa kati wa viwanda, maisha bora kwa kila M<sup>t</sup>anzania, utawala bora pamoja na kujenga uchumi imara na shindani ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, ili malengo tajwa hapo juu yaweze kutekelezwa ipasavyo, ni wajibu wa Serikali kutengeneza mazingira shirkishi na rafiki hususan kwa sekta binafsi kwa kuwa ndiyo engine ya ukuaji wa uchumi wetu. Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2014 inaonesha kwamba katika Kanda hii ya Afrika Mashariki, Tanzania haijaweza kutekeleza ipasavyo kwa vitendo sera zake zinazosimamia sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kufungua milango yake kwa uwazi zaidi katika ushiriki wa sekta binafsi, asasi za kiraia, wasomi na watu mbalimbali katika jamii kwenye maandalizi ya upatikanaji wa mapato yake na pia uwazi katika matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya vifungu mbalimbali katika Muswada. Sasa naomba kupitia baadhi ya vifungu ambavyo tunaona vinatakiwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara Sura ya 25. Leseni hizi zinajulikana kama leseni za manyanyaso (*nuisance tax*) ambazo zilifutwa tangu tarehe 29 Septemba, 2004. Naomba nifanye masahihisho ya uchapaji, hotuba mtakayopewa imeandikwa 29 Septemba, 2014 ni kosa la kiuchapaji ni Septemba 29, 2004 na Serikali ya Awamu ya Tatu. Je, Serikali ya Awamu ya Nne mmekosa ubunifu wa vyanzo vipyta vya mapato, mpaka mnaamua kurudisha leseni hizi za manyanyaso kwa Watanzania? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe takwimu katika Bunge hili Tukufu kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 ni kiasi gani cha mapato kilichopatikana kutokana na ada hizi za leseni. Aidha, chanzo hiki cha mapato kwa Serikali licha ya kuwa ni chanzo cha manyanyaso kwa wafanyabiashara pia ni kichocheo kikubwa cha rushwa kutokana na urasimu uliopo wa kupata leseni hizi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kuachana kabisa na aina hii ya chanzo cha mapato yake ambacho kwa kiasi kikubwa kinakiuka misingi ya kuendeleza uchumi endelevu kwa wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, (b) marekebisho ya sheria ya ushuru wa bidhaa Sura ya 147. Kifungu cha 16 cha Muswada tuliokuwa nao, huu mpya tuliopewa hapa Bungeni kitasomeka 17 kuna marekebisho yalifanywa na Serikali, cha Muswada kinachoifanyia marekebisho kifungu cha 124 cha sheria mama, kifungu kidogo cha 16(b), kwa sasa kitasomeka 17(b) kinafuta vifungu vidogo vya 5(a), 5(b) na 5(c) na kuviardika upya.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba gari linaloingizwa nchini litozwe kodi kulingana na taarifa za ukaguzi utakaofanywa nje (*pre-inspection*) na ukaguzi wa ndani (*verification*) na kuoanisha taarifa hizo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba uchakavu wa gari unatokana na matumizi ya gari husika na si mwaka wa kutengenezwa. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iangalie upya sera zake za mfumo wa kodi hasa ushuru wa forodha, VAT, ushuru wa bidhaa na kadhalika kwenye uingizaji wa magari mapya nchini. Jumla ya kodi zote kwenye manunuvi ya magari mapya kwa sasa ni takriban asilimia 63 ya gari jipya husika. Tunapendekeza kodi zote kwenye ununuvi wa magari mapya ziwe chini ya asilimia 30.

Narudia, tunapendeleza kodi zote kwenye ununuzi wa magari mapya ziwe chini ya asilimia 30. Hii itasaidia pamoja na mambo mengine usalama wa wananchi wetu, uhifadhi wa mazingira, kuongeza ubora wa maisha, kupunguza umaskini na vigezo vingine vya kuongeza utu wa mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la bidhaa ambazo ni mpya lakini ubora wake ni wa kiwango cha chini kulingana na bidhaa zilizokwisha kutumika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuangalia aina ya bidhaa hasa zilizotumika ambazo ni ukweli ulio wazi kuwa bidhaa zilizokwishatumika zinasaidia Watanzania walio wengi na hasa wale wenye kipato cha chini ambaao hutumia bidhaa hizo kuongeza utu wao.

Aidha, ushuru huo ungekuwa na manufaa kwa Taifa kama Tanzania ingelikuwa na viwanda vya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa husika na zenyenye ubora tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 cha Muswada wa zamani, ulioletwa leo kitasomeka kifungu cha 20 cha Muswada kinachorekebisha kifungu cha 137 cha Muswada kinachomtaka mzalishaji wa bidhaa (*manufacturer*) kuwa kwa muda wa siku 21 baada ya kuanza uzalishaji na kuanza kulipa ushuru wa bidhaa, kinyume na hapo anatakiwa kulipa faini ya shilingi 100,000/= au asilimia moja ya kiasi cha kodi ambacho hakikulipwa kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kifungu hiki kinawakatisha tamaa wazalishaji wa ndani, je, kwa siku 21 toka uanze kuzalisha bidhaa ni kweli bidhaa hizo zitakuwa zimeingia sokoni na kukubalika? Na je, ni muda gani usambazaji utakuwa umefanyika?

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kukiangalia upya kifungu hicho kwani badala ya kuwakatisha tama wazalishaji wa ndani iwe ni motisha kwa wajasiriamali wadogo wadogo na hasa wale wa ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya mwaka 2014/2015 katika Ibara ya 30 ya aya ya mwisho inaeleza kuhusu mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji. Naomba kunukuu; "Dhamira ya Serikali ni kuboresha mazingira ya uwekezaji na kupunguza gharama za kufanya biashara nchini ili kukabiliana na ushindani mkubwa kutoka nchi nyingine zilizotekeleza maboresho ya mifumo yao ya udhibiti wa biashara." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imenukuu sehemu hiyo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni kwenye Bunge hili la Bajeti kutokana na ukweli kwamba Serikali yenyewe kutokutekeleza kwa vitendo.

Narudia, Serikali yenyewe kutokutekeleza kwa vitendo kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji hapa nchini, aidha, imejengeka dhana kuwa; na hii ni ripoti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, imejengeka dhana kuwa sekta binafsi zinaendesha kazi yao kijanja janja na kwa upande mwingine sekta binafsi inaiona Serikali kuwa kazi yake ni kupunguza viwango vya faida kwa kupanua uititiri wa kodi na ushuru mkubwa visivyoingatia ukuaji wa biashara zao na shughuli zao za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano hai. Ni kodi na tozo mbalimbali katika sekta za utalii zinafikia 32 kwa sekta moja. Baadhi ya kodi hizo na tozo hizo naomba nizitaje TALA license, EWURA tax, charged by REA, Corporate tax, Withholding tax, Stamp duty, OSHA, PARK fees, Annual motor vehicle and road license fee, Safety fee, Land rent, Property tax, NSSF, Skill and Development Levy, Municipal Service Levy, Bedding Levy-Hotels, Import duty, Camping fee to

TANAPA, Bar licensed-Hotel, Excise duty of 0.15 percent, Tourism Development Levy, Rescue Fees, Business License Fee, Resident Permit Fee, Wildlife Management na kadharika, yaani mtu mmoja mfanyabiashara mmoja kwenye sekta hii analipa kodi zaidi ya 32. Hii ni kero na fedheha kubwa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya biashara yenye kodi na tozo hizo je, ni rafiki kwa biashara? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kodi au tozo zote hizo zihuishwe kwa pamoja yaani harmonization ili mazingira rafiki na yenye motisha kwa wawekezaji yafanyike kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Mauzo ya nje Sura ya 196. Kifungu cha 30 cha Muswada kinarekebisha ushuru wa mauzo ya nje ya ngozi ghafi kutoka asilimia 90 au shilingi 900 kwa kilo hadi asilimia 60 au shilingi 60 kwa kilo. Kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri lengo la kufanya hivyo ni kuzuia biashara ya magendo ya ngozi ghafi. Huu ni udhaifu wa Serikali kiutendaji kushindwa kudhibiti biashara ya magendo kwenda nje kiwe ni kitendo cha kulifanya Bunge litunge sheria ambayo pamoja na athari nyingine ni kupunguza ajira za Watanzania. Hoja hii ni dhaifu na haikubaliki. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona sababu hii ni dhaifu sana na inasababisha Watanzania kukosa ajira kwani kitendo cha kusafirisha ngozi ghafi ni kusafirisha ajira pia. Sambamba na hilo viwanda vyetu vya ngozi ambavyo ni *Himo Tanneries* kule Kilimanjaro, *Morogoro Tanneries*, *Moshi Lather Industry*, *Lake Trade and Company – Pwani*, *Arusha Tanneries*, *Tanmbuzi Limited* na kadhalika kuna uwezekano mkubwa wa kupunguza wafanyakazi wake kutokana na kukosa malighafi ya ngozi.

Mheshimiwa Spika, kanuni za uchumi zinaweka wazi kuwa nguzo za uchumi wa kijamii zinaeleza kuwa Serikali inatakiwa kujikita katika shughuli zozote za uwekezaji ambazo zinalenga katika kukuza uchumi bila ya kuathiri wengine, *The principles of welfare economics indicates that the Government should venture into any investment that makes its better off without making other worse of.*

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo ni dhahiri kuwa viwanda vya ndani vitakosa malighafi kutokana na kitendo cha Serikali kupunguza ushuru wa mauzo ya nje na kuchocheara biashara ya kuuza ngozi nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka au inashauri ushuru wa asilimia 90 au Shilingi 900 kwa kilo uendelee kuwepo kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato sura ya 332. Kifungu cha 38 kwa Muswada wa leo tulipewa hapa ni kifungu cha 40 cha Muswada kinachofanya marekebisho ya Kodi ya Mapato ya Ajira (*Pay As You Earn*) kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12. Kwa mujibu wa kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge Kambi Rasmi ya Upinzani iliishauri Serikali kupunguza kiwango cha kodi hiyo kutoka asilimia 14 mwaka wa fedha 2012/2013 hadi kufikia asilimia tisa. Lakini Serikali ikapunguza kuka asilimia 14 hadi 13 kwa mwaka. Aidha kwa mwaka ujao wa Fedha Serikali imetangaza kusudio la kupunguza kutoka asilimia 13 hadi 12.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza tena Serikali ishushe kodi hiyo hadi asilimi tisa kama tulivyoshauri mara kwa mara ndani ya Bunge lako Tukufu na nje ya Bunge, kwani kitendo hiki cha Serikali cha kushusha kwa tarakimu moja kila mwaka ni dhahiri inaweza kuchukua hadi mwaka wa 2017/2018 kuweza kufikia asilimia tisa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, takwimu za mapato ya Serikali kutokana na kodi hii kwa mwaka 2012/2013, ilipokuwa asilimia 14 ilikuwa ni bilioni 425.96 mwaka 2013/2014 ilivyokuwa asilimia 13 ilikuwa bilioni 509.997 na mwaka ujao wa fedha kwa asilimia 12 itafikia bilioni 568.45.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi ni dhahiri kwamba kwa kadri ya asilimia ya PAYE inavyozidi kushuka ndivyo mapato yanavyoongezeka. Hapa kuna dhana kuu tatu kubwa kwamba kuongezeka huko kunasababisha ajira kuongezeka, mishahara kuongezeka, kuongezeka kwa uhiari wa waajiri kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, dhana ya tatu ya hapo juu ni kwamba makampuni na viwanda hasa ya sekta binafsi vimeshindwa kutoa ajira za kudumu na hivyo kusababisha wafanyakazi walio wengi kuwa vibarua tu. Hatua hii itaisababishia Serikali kukosa mapato. Kushushwa hadi tarakimu moja kutaisababishia Serikali kupata mapato zaidi na hivyo kuweza mfanyakazi siku za mwishoni anapostaafu aweze kupata pensheni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kuongoza mabadiliko ni kuongoza wanyonge. Katika historia ya hapa Tanzania hakuna mahali popote wanyonge wamekaidi mabadiliko ya kuboresha maisha yao. Mara nyingi wanaokaidi ni walio nacho, hofu na woga wa wanyonge ni hadaa ya viongozi kutokuwa wakweli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukutakia matashi mema wewe pamoja na uongozi wa Bunge kwa utumishi wenu kwa Taifa la Tanzania, hekima na busara ziwaongoze katika kusimamia misingi ya haki na kukuza utu wa binadamu.

Aidha, napenda kuwashukuru wote walioshirikiana nami kuandaa maoni ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa unyenyekevu naomba kutumia fursa hii adhimu kuwatakia waislamu wote mfungo mwema wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika naomba kuwasilisha. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana na Mungu awasamehe hao viongozi waongo. Haya, ahsante sana.

#### **HOTUBA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2014 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHE. JAMES FRANCIS MBATIA (MB) KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2014 (THE FINANCE ACT, 2014)**

*(Kanuni ya 109(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013)*

#### **I. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia, kwa mara nyingine kusimama mbele ya Bunge lako tukufu nikiwa na siha njema.

Pili, napenda kumshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha, Mhe. Christina Lissu Mughwai na viongozi wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa ushauri na maoni yao wanayoendelea kuniwezesha kusimamia vyema wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeleta Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2014 kuliomba Bunge lako tukufu kuidhinisha mabadiliko katika sheria mbali mbali ili kuiwezesha Serikali kutoza kodi kwa ajili ya kutekeleza bajeti yake ya mwaka wa fedha 2014/2015, iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 24 Juni, 2014.

**Mheshimiwa Spika**, katika muswada huu, Serikali inapendekeza kurekebisha Sheria zifuatazo: Sheria ya Leseni za bidhaa Sura ya 25, Sheria ya Ushuru wa Forodha Sura ya 403, Sheria ya Ushuru wa bidhaa sura ya 147, Sheria ya Wakala wa Serikali Sura ya 245, Sheria ya Mauzo ya Nje Sura ya 196, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332, Sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348, Sheria ya Uwekezaji Tanzania Sura ya 38, Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 418 na Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Sura ya 82.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lako Tukufu linatunga Sheria ya Fedha ya mwaka 2014 ikiwa imebaki mwaka mmoja tu, kwa Serikali inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya awamu ya nne kumalizia kipindi chake cha pili cha uongozi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa miaka yote minne ya kipindi cha pili cha awamu ya nne, imekuwa ikiishauri Serikali kuachana na kasumba ya kuleta miswada ya fedha Bungeni inayopendekeza vyanzo vilevile vya kijadi vya mapato ya Serikali. Vyanzo hivyo vya kijadi vya mapato (traditional sources of revenue) ni pamoja na kutoza ushuru katika vinywaji baridi na vikali kama vile soda, jusi na pombe za aina mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Serikali imeendelea kukandamiza tabaka la wafanyakazi kupitia kodi ya mapato yaani PAYE ambayo inatozwa kwa kiwango kikubwa kuliko nchi zote za Afrika Mashariki, huku utozaji huo wa kodi ukiwa hauendani na; kupanda kwa gharama za maisha, upatikanaji wa huduma za msingi kwa Watanzania walio wengi ikiwemo huduma duni za afya, mfumo dhaifu wa elimu, viwango duni vya mundombini, ukosefu wa ajira nk. Athari za hali hii ni kuendelea kuwabebesha Watanzania walio wengi, mzigo mkubwa wa kodi ili kukidhi matumizi makubwa ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa miaka takriban tisa iliyopita yaani tangu mwaka 2005 hadi sasa, imekuwa ikipendekeza kwa Serikali vyanzo mbadala vya mapato ambavyo havimkandamizi mwananchi. Jambo la kushangaza ni kwamba Serikali mara zote imekuwa ikitiba kuchukua mapendekezo hayo na kuendelea na vyanzo vilevile ambavyo ni kandamizi kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati uliyounda ya kuisadia Serikali kubuni vyanzo vipyta vya mapato na kutoa taarifa yake, maarufu kama 'CHENGE I REPORT' na ripoti ya wataalam wa Serikali ya 'Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa' (Big Results Now-BRN) iliyohusu kubuni vyanzo vipyta vya Mapato; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza ripoti zote mbili ziletwe rasmi hapa Bungeni ili ziweze kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge na kuazimia namna bora ya utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuna mapungufu ya kikatiba ambayo yanayouzia chombo chochote, isipokuwa Mamlaka ya Rais kutoza kodi, hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 99 na Ibara ya 138(1). Ibara hizo zimelifunga mikono Bunge lako Tukufu, kwani mapendekezo yote ambayo yapo kwenye ripoti ya 'CHENGE I' ingekuwa ni rahisi kuyahalalisha kisheria na Bunge lako Tukufu. Katiba tulio nayo sasa imetufunga mikono na huu ni mmojawapo wa udhaifu mkubwa wa mgawanyo wa madaraka. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliomba Bunge lako Tukufu kuangalia udhaifu huu wa kisheria.

**Mheshimiwa Spika**, mionganoni mwa mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu vyanzo mbadala vya mapato ambavyo havijafanyiwa kazi kikamilifu ni kama ifuatavyo:

- i. Kodi ya majengo (Property tax); Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tulipendekeza kwa Serikali ianzishe Mamlaka ya Udhibiti wa Majengo (Real Estate Regulatory Authority) ili Sekta ya

Nyumba iweze kuratibiwa vizuri na kuiingizia Serikali mapato. Kwa makisio ya chini Sekta ya Nyumba ikisimamiwa vizuri, Serikali inaweza kukusanya zaidi ya shilingi triliioni 1 kwa mwaka.

ii. Usimamizi wa makusanyo katika bandari zetu, hususan bandari ya Dar es Salaam; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikishauri mara kwa mara kwamba, ikiwa vigezo vya **Ufanisi na Kuaminika** vitazingatiwa kwa uboreshaji wa asilimia 50 tu, ya bandari ya Dar es Salaam, basi Serikali itaweza kuongeza mapato yake kwa kiasi kinachokadiriwa shiinigi triliioni 1.44 kwa mwaka. Hii ni kwa mujibu wa taarifa ya benki ya Dunia ya mwaka 2013.

iii. Kodi kutokana na Uvuvi katika Bahari Kuu; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipendekeza kuwa Serikali itoze angalau mrabaha wa asilimia 5 katika mapato yanayotokana na uvuvi wa samaki katika bahari kuu. Inakadiriwa kwamba Serikali inaweza kupata mapato ya zaidi ya shilingi triliioni 1 kwa mwaka ikiwa sekta hii itasimamiwa kikamilifu.

iv. Kupunguza misamaha ya kodi kama njia ya kuongeza mapato ya Serikali; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri Serikali kupunguza misamaha ya kodi isiyokuwa na tija hadi kufikia angalau asilimia 1 ya pato la taifa. Kwenye eneo hili la misamaha ya kodi isiyokuwa na tija ya kukuza na kuendeleza uchumi wetu Serikali inaweza kuongeza mapato yake hadi kufikia takriban shilingi triliioni 1.386 kwa mwaka.

v. Kudhibiti ukwepajji wa kodi na udanganyifu; Takwimu zilizofanyiwa utafiti na taasisi mbalimbali zinaonesha kwamba takriban shilingi triliioni 1.9 kwa mwaka hupotea kutokana na udanganyifu na ukwepajji wa kodi.

vi. Vyanzo vingine vya mapato; kwa mfano:

(a) Utalii

➤ Uwindaji wa kitalii pekee unachangia mapato ya shilingi takriban shilingi bilioni 70 kwa mwaka

➤ Mauzo ya mazao ya misitu yanachangia mapato ya shilingi bilioni 220.4

(b) Kuongeza ufanisi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kutaongeza mapato ya Serikali yanayokadiriwa kuwa shilingi bilioni 708.1 kwa mwaka.

(c) Kodi ya asilimia 1 kwa manunuzi yote ya nje na tozo ya asilimia 0.5 ya mauzo yote ya nje kwa ajili ya Ukarabati wa Reli kutachangia mapato ya Serikali kwa takriban shilingi bilioni 226.1

**Mheshimiwa Spika**, aidha, vipo vyanzo vingine vya mapato; kwa mfano:

(a) Tozo mbalimbali na mirabaha katika sekta ya uchimbaji wa madini, michango ya kisheria ya taasisi na makampuni ya kibiashara ya Serikali kama vile TANAPA, EWURA, TCRA, Ngorongoro Conservation Area Authority nk.

(b) Kuongeza thamani madini yote ya vito hapa nchini badala ya kuuza madini hayo yakiwa ghafi.

Taasisi hizi zinatakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha No. 13 ya mwaka 2008 pamoja na Waraka wa Hazina namba 8 wa mwaka 2008/9 kuchangia mapato yao katika Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu ni taasisi ngapi zilitimiza sharti hili la kisheria la kuchangia asilimia 10 ya mapato yake ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuondoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali katika muswada huu wa fedha wa 2014 yanayolenga kutoza kodi katika vyanzo vilevile vya mapato na badala yake tunawaomba Waheshimiwa wabunge walete majedwali ya marekebisho katika jedwali la Marekebisho la Serikali ili kutoa mapendekezo ya vyanzo vipyta vya mapato yaliyoainishwa hapo juu na vyanzo vingine.

**Mheshimiwa Spika**, inakuwa vigumu kwa Waheshimiwa wabunge kuelewa kiasi halisi kitakachopatikana kwa kila kifungu kinachofanyiwa marekebisho, mfano: kwa marekebisho ya sheria ya ushuru wa bidhaa sura 147 inahusisha bidhaa nyingi lakini imetolewa jumla kuu tu, kuwa serikali itakusanya **shilingi bilioni 124.292**. Kwa utaratibu huu, unasababisha Waheshimiwa Wabunge kushindwa kukidhi **matakwa ya kanuni ya 109(2) ya kanuni za Bunge toleo la 2013**, inayosema

*“Marekebisho au mabadiliko ya kupunguza kiwango cha kodi katika ibara yoyote ya muswada wa Sheria ya fedha yatakayopendekezwa na Mbunge ye yeyote hayatakubaliwa iwapo hayatatoa mapendekezo mbadala yanayoziba pengo linalotokana na punguzo linalopendekezwa.”*

## II. SERA ZA KODI NA UKUAJI WA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika**, Lengo kuu la kodi ni:

- Kuchochea maendeleo endelevu;
- Kukuza uchumi; na
- Kukuza Utu wa mlipa kodi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali hutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa kutumia fedha hususani za walipa kodi wake. Ni jambo la kusikitisha kuwa sera za kodi hapa Tanzania kwa kiasi kikubwa zinakusudia zaidi ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya muda mfupi, hususan mwaka mmoja. Mfumo huu, kwa kiasi kikubwa unaondoa dhamira na kufisha utashi wa kila mlipa kodi katika ufuatiliaji wa matumizi sahihi wa kodi yake.

**Mheshimiwa Spika**, katika Dira ya Taifa ya mwaka 2025, Tanzania imejiwekea malengo ya kuwa na uchumi wa kipato cha kati, kuongeza kiwango cha maendeleo ya watu, kuwa na uchumi wa kati wa viwanda, maisha bora kwa kila Mtanzania, utawala bora pamoja na kujenga uchumi imara na shindani ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili malengo tajwa hapo juu yaweze kutekelezwa ipasavyo, ni wajibu wa serikali kutengeneza mazingira shirikishi na rafiki hususan kwa sekta binafsi kwa kuwa ndiyo injini ya ukuaji wa uchumi wetu. Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2014 inaonesha kwamba katika Kanda hii ya Afrika Mashariki, Tanzania haijaweza kutekeleza ipasavyo kwa vitendo sera zake zinazosimamia sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri serikali kufungua milango yake kwa uwazi zaidi katika ushiriki wa sekta binafsi, asasi za kiraia, wasomi na watu mbalimbali katika jamii, kwenye maandalizi ya upatikanaji wa mapato yake na pia uwazi katika matumizi yake.

## III. MAPITIO YA VIFUNGU MBALIMBALI KATIKA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, sasa naomba kupitia baadhi ya vifungu ambavyo tunaona vinatakiwa kurekebishwa

**a. Marekebisheso ya Sheria ya Leseni za Biashara Sura 25**

**Mheshimiwa Spika**, Leseni hizi zinajulikana kama leseni za manyanyaso (Nuisance Tax) ambazo zilifutwa tangu tarehe 29 Septemba, 2014 na Serikali ya awamu ya tatu. Je, Serikali ya awamu ya nne mmekosa ubunifu wa vyanzo vijpya vya mapato, mpaka mkaamua kurudisha leseni hizi za manyanyaso kwa Watanzania?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali itoe takwimu katika Bunge hili Tukufu kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 ni kiasi gani cha mapato kilichopatikana, kutokana na ada hii za leseni? Aidha, chanzo hiki cha mapato kwa Serikali licha ya kuwa ni cha manyanyaso kwa wafanyabiashara pia ni kichocheo kikubwa cha Rushwa, kutokana na urasimu uliopo wa kupata leseni hizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali hii inayoongozwa na CCM, kuachana kabisa na aina hii ya chanzo cha mapato yake. Ambacho kwa kiasi kikubwa kinakiuka misingi ya kuendeleza uchumi endelevu kwa Wananchi wa kipato cha chini.

**b. Marekebisheso ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147**

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 16 cha muswada kinachokifanya marekebisheso kifungu cha 124 cha sheria mama, kifungu kidogo cha 16(b) kinafuta vifungu vidogo vya (5A),(5B) na (5C) na kuvianidika upya. Naomba nirejee Vifungu vya (5A) na (5B);

"(5A) There shall be charged in addition to any other rates imposed under the law, a duty at a rate of 25% in respect of the imported vehicle aged more than eight years from the year of its manufacture excluding buses under HS Code 8702.10.22, 8702.10.29, 8702.10.99, 8702.90.29, 8702.90.99 (5B) There shall be charges in addition to any other rates imposed under the law, a duty at a rate of 10% in respect of the imported buses under HS Code 8702.10.22, 8702.10.29, 8702.10.99, 8702.90.29, 8707.90.99 aged more than five years from the year of its manufacture"

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza kwamba gari linaloingizwa nchini litozwe kodi kulingana na taarifa ya ukaguzi utakaofanyika nje (Pre-Inspection) na ukaguzi wa ndani (Verification) na kuoanisha taarifa hizo mbili. Hili ni kutokana na ukweli kwamba uchakavu wa gari unatokana na matumizi ya gari husika na sio mwaka wa kutengenezwa (**Year of Manufacture**).

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali iangalie upya sera zake za mfumo wa kodi hasa ushuru wa forodha, VAT, ushuru wa bidhaa nk, kwenye uingizaji nchini wa magari mapya. Jumla ya kodi zote kwenye manunuzi ya magari mapya ni takriban asilimia 63 ya gharama za gari husika.

Tunapendekeza kodi zote kwenye ununuzi wa magari mapya uwe chini ya asilimia 30. Hii itasaidia pamoja na mambo mengine usalama wa wananchi wetu, uhifadhi wa mazingira, kuongeza ubora wa maisha, kupunguza umaskini nk.

**Mheshimiwa Spika**, Kuna tatizo la bidhaa ambazo ni mpya lakini ubora wake ni wa kiwango cha chini kwa kulinganisha na bidhaa zilizokwishatumika.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuangalia aina ya bidhaa hasa zilizotumika, ambazo ni ukweli ulio wazi kuwa bidhaa zilizokwishatumika zinasaidia Watanzania walio wengi na hasa wale wenye kipato cha chini, ambao hutumia bidhaa hizo kuongeza Utu wao.

Aidha, ushuru huo ungelikuwa wa manufaa kwa Taifa, kama Tanzania ingelikuwa na viwanda vya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa husika na zenyenye ubora tofauti na ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 19 cha muswada kinacho rekebisha kifungu cha 137 cha muswada, kinachomtaka mzalishaji wa bidhaa (manufacturer) kuwa kwa muda wa siku 21 baada ya kuanza uzalishaji na kuanza kulipa ushuru wa bidhaa. Kinyume na hapo atatakiwa kulipa faini ya shilingi laki moja au asilimia moja kwa kiasi cha kodi ambayo haikulipwa kwa kipindi husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaona kifungu hiki kinawakatisha tamaa wazalishaji wa ndani. Je, kwa siku ishirini na moja toka uanze kuzalisha bidhaa ni kweli bidhaa hizo zitakuwa zimeingia sokoni na kukubalika? Na je, Ni muda gani usambazaji utakuwa umefanyika? Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kukiangalia upya kifungu hicho kwani badala ya kuwakatisha tamaa wazalishaji wa ndani iwe ni motisha kwa wajasiriamali wa ndani.

**Mheshimiwa Spika**, hotuba ya makadirio ya ofisi ya Waziri Mkuu ya mwaka 2014/2015, katika ibara ya 30 aya ya mwisho, ilieleza kuhusu mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji,

**“Dhamira ya Serikali ni kuboresha mazingira ya uwekezaji na kupunguza gharama za kufanya biashara nchini ili kukabiliana na ushindani mkubwa kutoka nchi nyingine zilizotekeleza maboresho ya mifumo yao ya udhibiti wa biashara”.**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, imenkuu sehemu hiyo ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutokana na ukweli kwamba, Serikali yenye kutokontaktekeleza kwa vitendo kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji hapa nchini. Aidha, imejengeka dhana kuwa Sekta binafsi zinaendesha kazi zao kijanja janja, na kwa upande mwingine Sekta Binafsi inaiona Serikali kuwa kazi yake ni kupunguza viwango vyao vya faida kwa kupanga uitiri wa kodi na ushuru mkubwa visivyozingatia ukuaji wa biashara na shughuli zao za uzalishaji1.

**Mheshimiwa Spika**, mfano hai; ni kodi na tozo mbali mbali zipatazo 32 zinazotozwa kwenye sekta ya Utalii. Baadhi ya kodi hizo na tozo ni: TALA license, EWURA Tax 1% charged by TANESCO, REA tax 3%, VAT, Corporate tax, Withholding Tax, Stamp Duty, OSHA,PARK Fees, Annual Motor Vehicle and Road License Fee, Safety week stickers, Land Rent,Property Tax, NSSF, Skills & Development Levy, Municipal Service Levy, Bedding Levy-Hotels, Concession Levy-Hotels, Import Duty, Camping fees to TANAPA, Bar license-Hotel, Excise duty of 0.15%, Tourism development levy, Rescue Fees, Business License fee, Resident permit fees, Wildlife Management fees, n.k

**Mheshimiwa Spika**, katika mazingira ya biashara yenyeye kodi na tozo hizo, je ni rafiki kwa biashara? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kodi na au tozo zote hizo zihuishwe (Harmonized) pamoja ili mazingira rafiki na yenyeye motisha kwa wawekezaji wafanyike kwa vitendo.

### c. Marekebisho ya Sheria ya Mauzo ya Nje sura ya 196

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 30 cha muswada kinarekebisha ushuru wa mauzo ya nje ya nchi ya ngozi ghafi, kutoka asilimia 90 au shilingi 900 kwa kilo moja hadi asilimia 60 au shilingi 600 kwa kilo. Kwa mujibu wa Mhe. Waziri, lengo la kufanya hivyo ni kuzuia biashara ya magendo ya ngozi ghafi. Huu ni udhaifu wa Serikali kiutendaji, kushindwa kudhibiti biashara ya magendo kwenda

nje kiwe ni kigezo cha kulifanya Bunge litunge sheria ambayo pamoja na athari nyingine ni kupunguza ajira za Watanzania. Hoja hii dhaifu na haikubaliki!

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaona sababu hii ni dhaifu sana na inasababisha Watanzania kukosa ajira, kwani kitendo cha kusafirisha ngozi ghafi ni kusafirisha ajira pia. Sambamba na hilo viwanda vyetu vya ngozi ambavyo ni: Himo Tanneries and Planters Ltd (Kilimanjaro - Himo); Morogoro Tannery (Morogoro – Kihonda Industrial Area); Moshi Leather Industries Ltd (Kilimanjaro – Moshi Vijijini); Lake Trade Co. Ltd (Pwani – Kibaha); SAK Tannery; (Arusha) na Tanmbuzi Ltd. Kuna uwezekano mkubwa wa kupunguza wafanyakazi wake kutokana na kukosa malighafi.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni za uchumi zinaweka wazi kuwa, 'Nguzo za uchumi wa kijamii, zinaelezea kuwa Serikali inatakiwa kujikita katika shughuli zozote za uwekezaji ambazo zinalenga katika kukuza uchumi wake bila ya kuathiri wengine' - (**The principles of welfare economics indicates that, the Government should venture into any investment that makes it better off without making others worse off**).

Kwa misingi hiyo ni dhahiri kuwa viwanda vya ndani vitakosa malighafi kutokana na kitendo cha Serikali kupunguza ushuru wa mauzo nje na kuchochea biashara ya kuza ngozi nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka ushuru wa asilimia 90 au shilingi 900 kwa kilo uendelee kuwepo kama ilivyokuwa awali.

#### d. Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 38 cha muswada kinachofanya marekebisho ya kodi ya mapato ya ajira (PAYE) kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12. Kwa mujibu wa kumbukumbu za taarifa rasmi za Bunge (Hansard) ni kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, iliishauri Serikali kupunguza kiwango cha kodi hiyo kutoka asilimia 14 mwaka wa fedha 2012/13 hadi kufikia asilimia 9. Lakini Serikali ikapunguza kutoka asilimia 14 hadi 13 kwa mwaka 2013/14. Aidha, kwa mwaka ujao wa fedha Serikali imetangaza kusudio la kupunguza kutoka asilimia 13 hadi 12.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inasisitiza tena Serikali ishushe kodi hiyo hadi asilimia 9 kama tulivyokuwa tunashauri mara kwa mara ndani ya Bunge hili Tukufu na nje ya Bunge. Kwani kitendo hiki cha Serikali cha kushusha kwa tarakimu moja moja kila mwaka ni dhahiri inaweza kuchukua hadi mwaka wa 2017/2018 kuweza kufikia asilimia 9.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu za mapato ya Serikali kutokana na kodi hii kwa mwaka 2012/13 PAYE ilikuwa asilimia 14, mapato yake yalikuwa shilingi bilioni 425.960. Mwaka 2013/14 PAYE ilikuwa asilimia 13, mapato yake yalikuwa shilingi bilioni 509.997. Na mwaka ujao wa fedha 2014/2015 matarajio yanaonesha kuwa PAYE itakuwa asilimia 12, mapato yake yatakuwa ni shilingi bilioni 568.451.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takwimu hizi ni dhahiri kwamba kwa kadri asilimia ya PAYE inavyoshuka ndivyo mapato yake yanavyoongezeka. Hapa kuna dhana kuu tatu kubwa kwamba kuongezeka huko kumesababisha:

- Ajira rasmi kuongezeka
- Mshahara umeongezeka
- Kuongezeka kwa uhiari kwa waajiri kulipa kodi hiyo (**Increase in Compliance rate**).

**Mheshimiwa Spika**, dhana ya tatu hapo juu ni kwamba, makampuni na viwanda hasa vya sekta binafsi, vimeshindwa kutoa ajira za kudumu na hivyo kusababisha wafanyakazi wao kuwa

vibarua tu, hatua hii inasababisha Serikali kukosa mapato. Kushushwa kwa kodi hadi asilimia 9 kama tunavyoshauri, itasaidia kushawishi makapuni na viwanda hivyo kutoa ajira za kudumu kwa watumishi wake na hivyo PAYE italipwa kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ilikwishatoa ushauri wa kima cha chini cha Mshahara cha **shilingi 350,000**. Kwa maana kwamba kwa kiwango hiki PAYE ikiwa asilimia 9, mapato ya Serikali yataongezeka na mishahara kwa watumishi itakuwa na hakikishio la kulipwa pensheni. Tukumbuke kwamba pensheni inalipwa kulingana na kiwango cha mshahara ambao mtumishi alikuwa analipwa kabla ya kustaafu.

#### **IV. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, kuongoza mabadiliko ni kuongoza wanyonge. Katika historia hapa Tanzania, hakuna mahali ambapo wanyonge wamekaidi mabadiliko ya kuboresha maisha yao. Mara nydingi wanaokaidii ni walio nacho (hasa mafisadi), hofu na woga wa wanyonge ni hadaa ya viongozi.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kukutakia matashi mema, wewe pamoja na Uongozi wa Bunge kwa utumishi wenu kwa Taifa la Tanzania. Hekima na Busara ziwaongoze katika kusimamia misingi ya haki na ya kukuza Utu wa Binadamu.

Aidha, napenda kuwashukuru wote walioshirikiana nami kuandaa maoni ya muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa unyenyekevu, naomba kutumia fursa hii adhimu, kuwatachia Waislam wote mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

.....  
**James Francis Mbatia (Mb)**  
**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni-Wizara ya Fedhha**  
**27 Juni, 2014**

**SPIKA:** Waheshimiwa kwa mujibu wa taratibu zetu dakika tulizo nazo kuweza kujadili hoja hii ni kama dakika 60. Kwa hiyo nitakuwa na wachangiaji wachache sana.

Nianze na Mheshimiwa Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni, atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage na atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Mheshimiwa Ndassa yupo?

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na naomba niunge mkono mawasilisho ya Serikali lakini pia niunge mkono mawasilisho ya Kamati ya Mzee Chenge.

Nianze labda na upande wa magari ambayo kwa kweli upande wa Serikali imefanya jambo jema sana kwa kupokea na kukubali mapendekezo ya Kamati ya Chenge. Lakini pia upande, Mheshimiwa Spika kwa sababu sikujandaa...

**SPIKA:** Unaweza kukataa kama hujajiandaa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Sorry!

**SPIKA:** Unaweza kukataa kama hujajiandaa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, hapana, naunga mkono mapendekezo ya Mzee Chenge lakini pamoja na mapendekezo ya Serikali. Nashukuru. (Kicheko)

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia nishukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hapa leo.

Kwanza nilikuwa na ombi, wakati tunajaribu kupitia hizi sheria mbalimbali tunapata tatizo kubwa kwa kupata hizi sheria zile copy halisi.

Sasa tulikuwa tunaomba Ofisi yako Mheshimiwa Spika kama inaweza kutuandalia DVDs au CDs zenye sheria zote ambazo *zipo up to date* labda kila mara moja kwa mwaka ili wakati tunapotaka kufanya marejeo tuweze kupitia sheria ambayo tunataka kuzibadilisha ili iwe rahisi kwa Wabunge kupitia sheria mbalimbali na pia kuleta mapendekezo ambayo Serikali labda hajajaleta lakini sisi kama Wabunge tunaona imepitwa na wakati au inataka marekebisho kwa kuboresha uchumi wa nchi yetu basi tuweze kutumia hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini muhimu pia nilikuwa naomba Serikali izingatie kwa sehemu kubwa, sasa hivi *informal sector* (sekta isiyo rasmi) ni kubwa. Tulikuwa tunapendekeza kwamba iangalie namna ya kuondoa kodi, tozo na ushuru mbalimbali ambao unafanya watu ambao wako kwenye *informal sector* waweze kurudi kwenye *formal sector*.

Leo hii ukiangalia mtu kwa mfano katika lile Jedwali la Kodi ya Mapato, kwa yule ambaye haweki *records* na yule ambaye anaweka *record* tofauti ni ndogo sana na ukiangalia tofauti ni kama shilingi 100,000/= kwa yule ambaye anaweka *record*, utampata wapi mhasibu ambaye atakutoza hiyo shilingi 100,000/= kwa mahesabu ya mwaka mzima. Utakuta yule ambaye haweki *record* anakuwa na unafuu, lakini kwa yule ye yeyote ambaye atakuwa na leseni ya biashara au amekuwa registered anapata mlolongo wa kodi na ushuru mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwagine ni kwamba kuna sheria nyingi ambazo tunapitisha halifu wakati wa utekelezaji haitekelezwi na Idara ya TRA wakati wa kukusanya yale mapato, inakuwa pia ni kero. Lakini muhimu kuliko yote asilimia 80 ya Watanzania ambayo ajira kubwa ipo huko ni katika sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi ambayo haikuzingatiwa kabisa katika sheria hii ya mabadiliko yote haya yaliyokuja. Tunashukuru hiyo moja ambayo kwa sasa hivi sasa itafanya yale matunda au concentrates inayotoka nje ule ushuru uwe juu ili sekta ya kilimo humu ndani ipate unafuu, matunda hapa yaweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, lakini bado katika ile sheria tulitegemea kwamba tungekuwa na mabadiliko katika sheria ya zana za kilimo, bado zinaendelea kutozwa kodi, matairi ya trekta, trela na bado tumeambiwa kwamba itakuja kujitokeza katika sheria mpya ya VAT. Lakini hiyo sheria mpaka tuje tuijishe bado itachukua muda mrefu na inawezekana pia ikawa kama ilivyotokea kwa miaka mitatu mfululizo, hii ya nyuma ambapo tumepitisha na huo ushuru bado unaendelea kutozwa.

Inawezekana pia ikawa kama ilivyotokea kwa miaka mitatu mfululizo hii ya nyuma ambapo tumepitisha na ushuru huo bado unaendelea kutozwa. Naishukuru Kamati ya Bunge ya Bajeti na Serikali, safari hii maoni mengi ambayo tuliyafanya kazi vizuri, wameyakubali na tayari yameonekana katika Jedwali lao la Marekebisho; tunashukuru kwa hilo. Tunaendelea kuwaomba Wataalam kwamba, badala ya sisi kusubiri mpaka dakika za mwisho, tuwe tunapata muda wa kutosha ili hizi sheria na haya marekebisho tuyaelewe vizuri. Tuweze pia kuishauri Serikali mahali ambapo inataweza kupata mapato mengi zaidi, ili kodi ambayo

anabebeshwa mtu mmoja, yaani *formal sector*, iweze kupungua na *compliance*, yaani ule ulipaji wa kodi utaongezeka.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru wamekuja na vigezo vingi vya kuondoa misamaha ya kodi. Tunawaomba Wataalam wakati tunakuja kwenye hiyo Sheria mpya ambayo tunaitegemea ya VAT Bill, wahakikishe kwamba, lengo hapa siyo kuondoa msamaha kwa ujumla wake. Lengo ni kwamba, yale maeneo muhimu ambayo yanahitajika, hiyo kodi iendelee kupata msamaha, ili uchumi wetu uendelee kukua, yasije yakaachwa na hasa katika Sekta hiyo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, jana tulipopeleka hoja yetu kuhusu Skill Development Levy (SDL), kulikuwa kuna utata kidogo katika suala la tafsiri yake. Tunaomba hata hizi tafsiri, kama inawezekana hizi sheria zote ambazo zinapitishwa zifkishwe katika ngazi zote kuanzia ngazi ya Wilaya na Mkoa kwa upande wa TRA, ili baadaye isilete mkanganyiko wakati wa kukusanya, iendelee kukusanya kile ambacho ni halali. Yale ambayo yamesamehewa, basi yasiendelee kutozwa kodi, kuondoa kero kwa Watanzania na kwa wafanyabiashara na wale wote ambao wanalazimishwa kulipa kodi ambayo wanajua tayari haipo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ambayo nilikuwa ninaomba ifafanuliwe vizuri kwa uwazi na sheria hiyo tafsiri yake iwekwe ni kwenye SDL, ambapo hata Mheshimiwa Waziri alipotamka zile taasisi za kidini, ambazo wafanyakazi wake au watumishi watasamehewa kulipa hiyo SDL, ni pale wanapofanya kazi ya dini tu au masomo ya dini au kutekeleza shughuli za kidini. Tulipendekeza hilo liwekwe wazi ili baadaye tusipate usumbu na hata taasisi zao ambazo ni za elimu na zinazotoa huduma za afya pia iwekwe wazi kwamba nazo pia hazitakuwa zinatozwa kwa sababu tayari kuna malalamiko ambayo tumeyapokea huko na ndiyo maana tulileta hayo mapendeleko ya mabadiliko ili iwe wazi ile kero baadaye isijitokeze.

Mheshimiwa Spika, muhimu kuliko yote kwa upande wangu, bado ninaisubiri, jana nilileta mabadiliko hata hii Sheria ya VAT, kabra hatujasubiri hilo la mabadiliko mapya. Nilileta mabadiliko ya vipuri vya matrekti, lakini nimekubaliana nao ya kwamba, tutasubiri na tutaiboresha hiyo Sheria ya VAT. Ninashukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, wametoa ushirikiano mkubwa na ndiyo maana yale mengine ambayo wametuambia, tumekubaliana nao na tutawaunga mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsanteni na ninashukuru. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa ninamwita Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninaunga mkono hoja iliyoko mbele yetu, ila kuna mambo mawili, matatu, ambayo ningelipenda kutoa angalizo kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwenye ushuru wa sigara, inaonekana ushuru wa sigara umeongezeka nchini kwetu. Ninaishauri Serikali, ifanye malinganisho na nchi ambazo tunashirikiana kwenye Region moja. Kuwekeza kwa wenzetu kuzalisha isije ikawa rahisi na Tanzania ikawa *distribution centres*.

Mheshimiwa Spika, nzungumze hilohilo kuhusu suala la nondo. Ninachelea kama wenzetu wanaweka ushuru mkubwa kwenye nondo zinazotoka nje kuingia kwao na sisi tunaweka ushuru mdogo, ina maana nondo za kuagiza zitaingia kirahisi hapa na kuzinyima Kampuni za hapa nchini *competitive advantage*. Kwa hiyo, itapelekea viwanda vyetu

vitadhoofu, wale jirani zetu waliozuia viwanda vyao vitaimarika na Common Market ya East inapoanza, sisi tutageuka soko. Kwa hiyo, waangalieni wale wenzetu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, huo ulikuwa ni utangulizi, nizungumzie suala la mafuta. Mheshimiwa Waziri, amekuja na utaratibu mpya wa kwamba, mafuta yatakapofika nchini yatalipa ushuru mara moja.

Mheshimiwa Spika, niseme kuwa, sina masilahi katika hili, lakini napenda kutamka kwamba, karibu nusu ya kampuni zote za kati na chini za Kitanzania, nilihuksika kwa namna moja katika kuzianzisha. Nusu ya makampuni yote haya ya kati na madogo, nusu yake, nilihuksika kwa namna moja kuyaanzisha zama zile kabla zijaanza biashara hii ya maneno.

Mheshimiwa Spika, utaratibu aliouanzisha Mheshimiwa Waziri, kama alivyosema Mheshimiwa Andrew Chenge, una madhara. Sisi Tanzania tunaagiza meli moja yenye ujazo wa tani 100,000. Hakuna utaratibu wa namna hiyo katika nchi za Rwanda, Burundi na Uganda, unakochukulia mfano. Kitakachotokea ili mtu akulipe ushuru *upfront*, itabidi aende Benki akope. Katika *price structure* ya EWURA, hakuna provision, hakuna kiasi kilichotengwa cha ile *cost of borrowing*, ile gharama ya kukopa haipo. Maana yake ni nini?

Kama hakuna gharama ya kukopa, itabidi sasa mtu akakope ili akupe pesa wewe kwa mafuta ambayo hajayalipa. Waheshimiwa Wabunge, kampuni za mafuta, ile pesa wanayolipa ni Wakala, wanakusanya wanamlipa TRA na hawa watu wanakusanya karibu asilimia 16 ya makusanyo ya TRA.

Mheshimiwa Spika, kinachoweza kufanyika hapa ni kwamba, Serikali ikae na EWURA na makampuni, ikubali ile *cost of borrowing* nani ataiibeba. Mkiweka kwenye *price structure*, ina maana Mwananchi ataumia na mimi nisingelipenda kushauri Wananchi waumie. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kilichopaswa kufanyika, Serikali kama mnataka kuchukua mapato yenu mwanzoni, mlipaswa mchukue ile Hifadhi ya TIPPER, mchukue asilimia zote ili TIPPER iwe ya Serikali. Mnunue ile 50%, halafu eneo lile la TIPPER ambalo kuna ekari 30 mjenge matanki makubwa ya ujazo wa tani kama 500,000 ili Tanzania iwe hifadhi kubwa ya mafuta; halafu mafuta katika eneo lile iwe sehemu iliyozuiliwa, Bonded Warehouse.

Mheshimiwa Spika, kabla ya utaratibu wa sasa, zamani tulikuwa na maeneo yaliyozuiliwa, Bonded Warehouse, ili mtu atakayekuwa anaagiza au anatoa kiasi anachokihitaji, anakulipa ushuru wako mara moja.

Mheshimiwa Spika, utaratibu anaouleta Mheshimiwa Waziri, una madhara yafuatayo: Tumepigana sana hapa kuanzia mwaka 2008 mliokuwepo, tukaanzisha Bulk Procurement katika kipindi chetu. Makampuni sasa yanayoagiza tani 10,000, katika mfumo wa kulipa Bulk Procurement, watakuja kushindwa kuagiza kiasi hicho mara moja. Wataanza kuagiza vipande vidogo vidogo, ndiyo maa Mtemi Chenge akasema, kutakuja kutokea tatizo la mafuta. Mtemi Chenge, ambacho hakukisema, matatizo ya ukosefu wa mafuta yatatokea kwetu sisi wa mikoa ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, yatatokea mikoa ya pembezoni kwa sababu mafuta yanaposhuka Dar es Salaam, kuja kufika Bukoba yanachukua siku saba. Sasa kama mtu analipa *upfront*, hizi siku saba zinakwenda wapi? Kwa hiyo, kuna mambo ambayo hayajawekwa sawa.

Mheshimiwa Spika, nami nikueleze, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, si kweli kwamba, ulipaji wa siku 15, 15 unakoshesha mapato. Hakuna, meli inapofika, mafuta

yanapopimwa huwa kunatolewa kitu kinachoitwa *tax liability*. Ukiwa na Watendaji makini kama hawa ninaowafahamu wa TRA, especially huyu Commissioner General mpya; ukishapata *tax liability*, ukaweka kwenye computer, ni suala la kufuatilia. Mimi nilishaweeleza hapo mwanzoni zamani wakati ninaandika kwenye magazeti kwamba, kwa sababu 15% ya collection ya TRA, inatokana na segment hii, wekeni watu makini ambao wanajua *they have to do, otherwise they will be fired*. Unamuweka mtu, unampa mamlaka, anakosea asubuhi, kabla ya saa nne ameshafukuzwa kazi. Suala lililopo ni kwamba, sisi tunaogopa wasije wakaumia wale watu wadogo. Kwa nini ninayatetea makampuni madogo na makampuni ya kat?

Mheshimiwa Spika, kwa makampuni makubwa yenye *financial muscles* watakwenda kwa ndugu zao huko Ulaya, wataleta pesa watakeleza kile unachokitaka.

Mheshimiwa Spika, niwaambie jambo moja; makampuni yanayoitwa makubwa hakuna ambayo ina kituo Kigoma, hakuna ambayo ina kituo Bukoba, hakuna ambayo ina kituo kule kwetu Bunda. Kwa hiyo, makampuni yote yamejibana mjini. Puma ana vituo 33 na ukubwa wake. Hizi Kampuni zote zimejibana mjini. Kwa hiyo, ili kutufaidisha sisi ambao tunakaa kule vijijini mwishoni, lazima Makampuni haya ya Kitanzania yalelewe; na ndiyo maana ninapendekeza na ninarudia kupendekeza tena, lazima tuanzishe National Oil Company, ambayo wakati wote itaweza kuhimili mtikisiko, kwa sababu haitakuwa na mahali pa kwenda. Nimekuwa nikilisema hapa, nimelisema kwenye Kamati na kila siku mnani puuza. Utakapotokea mtikisiko, ndipo mtakuja kujuu kwamba, tulipaswa kuwa na watoto wetu wenyewe badala ya kuwa na watoto wa kufikia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, *multinational companies*, hali ikiwa mbaya wanaondoka. Imeondoka Caltex, Esso imeondoka, BP imeondoka na Shell itaondoka; na hawa wengine wataondoka kwa sababu hapa wamekuja kuchuna. Ndiyo maana mimi nilipoteza muda wangu kuziandaa Kampuni za Kitanzania, kusudi ziweze kuja, ni watoto wetu wenyewe. Hatima ya yote ni kuanzisha National Oil Company, ambayo vijana wanaotoka Vyuo Vikuu, wataingia tuwafundishe kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iwalete hao vijana niwafundishe kazi mimi wakati bado nina nguvu, halafu tunapoondoka tunaweza kuendelea. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaishauri Serikali mkae na Wadau na Wizara ya Nishati, hili jambo litakuja kuleta mtikisiko. Kwa sababu katika biashara ya mafuta, tunaangalia upatikanaji wa mafuta, kama mafuta hayapatikani, yatapanda bei, hata ungekuja na Polisi wangapi. Yanapoanza kukosekana yanauzwa kwenye madumu na ndiyo yanapoteza ile *quality*. Mafuta ni *availability, reliability* na *quality*. Yakishauzwa kwenye vidumu, hakuna *quality* tena, utawekewa maji, matope na vitu vingine vichafu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikiwa na imani kwamba, Mheshimiwa Waziri, atanikaribisha nimpe ushauri wa bure, ninaunga mkono hoja. (Kicheko/Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilisema baada ya Mheshimiwa Charles Mwijage kuzungumza, nitamwita Mheshimiwa John Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Awali ya yote, kabla ya kujielekeza kwenye vifungu vya Muswada, naomba kutumia fursa hii kutoa pole kwa msiba wa Sister aliyeuwawa pale Ubungo kwa kupigwa risasi. Mwenyezi Mungu, amlaze mahali pema na nitaomba Serikali kwa kweli, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mambo ya Ndani, ifanyie kazi kwa kuwa kumejitokeza mara kwa mara matukio ya watu kuawa; siyo Sister tu, wapo wengine

waliouwawa wakitoka kwenye Benki za jirani na maeneo ya Ubungo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linahitaji Serikali kulichunguza na kuchukua hatua ili kunusuru maisha ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza kwenye kuchangia vifungu kadhaa kutokana na muda huu mchache vya Muswada ulioletwa hapa mbele yetu pamoja na marekebisheso yake.

Mheshimiwa Spika, tunaifanya kazi hii tukiwa tunafungwa Kikatiba nje ya kazi hii kufanya marekebisheso ya kikodi. Kifungu hiki cha Kikatiba kiko kwenye Ibara ya 99 (1) ya Katiba inasema, Bunge halitashughulikia jambo lolote kati ya mambo yanayohusika na Ibara hii, isipokuwa kama Rais amependekeza jambo hilo lishughulikiwe na Bunge na Bunge na pendekeso hilo la Rais, liwe limewasilishwa kwenye Bunge na Waziri. Mambo yanayohusika na Ibara hii ni pamoja na Muswada wa Sheria kwa ajili ya jambo lolote yafuatayo: (i) Kutoza kodi au kubadilisha kodi kwa namna yoyote nyingine isipokuwa kupunguza.

Mheshimiwa Spika, ubovu huu wa Katiba unafanya nje ya Muswada wa Sheria ya Fedha, Bunge kuititia kwa Wabunge Binafsi, ama Wabunge kwa ujumla wao, lisiwe na uwezo wa kufanya maamuzi yoyote ya kuongeza kodi kama Rais kuititia kwa Waziri hajaleta Muswada Bungeni.

Mheshimiwa Spika, udhaifu huu wa Kikatiba ni muhimu urekebisheswe ili tuwe na uhuru zaidi katika masuala yanayohusiana na kodi wakati wa kujadali Muswada wa Sheria ya Fedha na nje.

**SPIKA:** Basi litakapokuja Bunge la Katiba turudi tufanye hizi kazi. (Makofii)

Mheshimiwa Mnyika, endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, niseme tu, kama maoni ya Wananchi hayatazingatiwa, hatutarudi kufanya hiyo kazi; kwa kuwa hayatazingatiwa hata haya mambo mengine ya msingi. (Kicheko/Makofii)

Mheshimiwa Spika, nirejee kwenye vifungu mahususi, nitaanza na Kifungu cha 17 cha Marekebisheso ya Sheria. Ninashukuru baada ya kazi ya Kamati, Serikali imeondokana na lengo la awali lililokuwepo juu ya Kifungu hiki, ambacho awali kilikuwa Kifungu cha 16.

Mheshimiwa Spika, bado lipo tatizo, uamuzi wa kuongeza viwango vya tozo la kodi kwenye magari hasa kwenye magari ya umri wa kati yasiyozidi miaka kumi ni kitanzu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeliunga mkono pendekeso hili kama kungeletwa hapa Jedwali la Serikali, kupunguza kodi kwa magari mapya, ili watu wanunue magari mapya. Kama pendekeso la kupunguza kodi kwenye magari mapya haliji, kwa vyovyote vile pendekeso la kuongeza kodi kwa asilimia 15 lisikubalike, lifanyiwe marekebisheso na nitaleta Jedwali la Marekebisheso kwenye eneo hili, kwa ajili ya marekebisheso. Kwa hiyo, kama Serikali inataka kusiwe na marekebisheso, kwa lengo la kulinda hayo ambayo Waziri ameyaeleza na Serikali imeyaeleza, basi ilete hapa Jedwali la kupunguza kodi kwenye magari mapya, ili watu waelekee kwenye kununua magari mapya na waache kununua magari yenye umri wa miaka isiyozidi kumi kama ambavyo ninaelezwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nitachangia kwenye eneo linalofuata, Kifungu cha 30 cha Sheria, kinachohusiana na masuala ya kodi kwenye bidhaa ghafi za ngozi. Katika jambo hili, ninaungana mkono na mapendekeso ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake ya Bajeti alisema kwamba, lengo la pendkelezo hili na jambo hili limerudiwa tena, ni kuzuia utoroshaji wa ngozi ghafi kupelekwa nje ya nchi. Sasa kama kuna utoroshaji kwa njia za magendo za ngozi ghafi, maana yake kuna udhaifu wa Serikali katika kudhibiti mipaka ya nchi. Udhaifu huo wa Serikali wa kudhibiti mipaka ya nchi, wa kudhibiti ngozi hizi kutoroshwa kwa magendo, haupaswi kuzibwa kwa kuathiri Sekta ya Ngozi hapa nchini, kwa kupunguza kodi na hatimaye kusababisha viwanda vya ndani kukosa malighafi ya kutosha na hatimaye kusababisha ajira kutoroshwa nje. (Makofii)

Unapopeleka ngozi ghafi ambazo bado hazijachakachuliwa ndani ya nchi, unasababisha Vijana wa Tanzania kukosa ajira katika kazi hii ya viwandani ya kuzibadili ngozi ghafi kuwa ngzi ambazo tayari zimeshachakatuliwa. Vilevile kuwa bidhaa za ngozi ambazo kimsingi zina soko kubwa Kimataifa na Tanzania tuna uwezo wa kusafirisha bidhaa hizi nje.

Mheshimiwa Spika, jambo hili sikubaliani nalo bado. Ibara ya 30 ya Muswada huu, Serikali bado imeendelea na uamuvi wake wa kuziba udhaifu wa Serikali wa kuzuia magendo kwa kuathiri ajira na kuathiri viwanda vya ndani; jambo hili halikubaliki. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kifungu kingine ambacho ningelipenda kuchangia katika Muswada huu ni Ibara ya 40 ya Muswada wa sasa na hapo awali ilikuwa Ibara ya 38 ya Muswada, juu ya kodi ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa mara kwa mara hapa Bungeni na Kambi ya Upinzani na Wabunge wengine kwamba, kodi ya Wafanyakazi ishushwe na iwe tarakimu moja. Ninaungana mkono na Kambi ya Upinzani na kwa sababu ya muda, sitazungumza kwa kirefu, namna ambavyo Serikali mara kwa mara imewaaahidi Wafanyakazi, lakini ikiwahadaa bila utekelezaji. Sasa kama wote tunazungumza lugha moja ya kwamba, kodi kwa wafanyakazi ishushwe, basi jambo hili lijadiliwe na liamuliwe kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nitaleta Jedwali la Marekebisho kwenye eneo hili, nimekwishapeleka Jedwali ya Marekebisho kwa Katibu na ninaomba niliweke tu Mezani kama kumbukumbu, kwa sababu tayari limeshapelekwa kwa Katibu. Pamoja na Jedwali hili, tumeainisha, Serikali inaposema ukipunguza kodi ya Wafanyakazi kuwa tarakimu moja au kuwa asilimia 10 au 11, badala ya 12 inayopendekezwa na Serikali, Serikali inavyosema tatizo ni vyanzo vya mapato. Kimsingi, Serikali inakwepa tu kutekeleza jambo hili na safari hii mapendekezo ya vyanzo mbadala, tumeyakokotoa kutoka taarifa ya Kamati yako. Taarifa ya Kamati ya Spika, juu ya mapendekezo ya Serikali, iliyoongozwa na Mheshimiwa Andrew Chenge. (Makofii)

Nimeweka kwa muhtasari, ninaomba niweke Mezani, baadhi ya mapendekezo ya Taarifa hii, mapato ya mapendekezo ya Kamati. Kwa mwaka wa fedha huu peke yake, Kamati hii iliainisha mapato yanayozidi shilingi trilioni 1.7, ambayo utekelezaji unawezekana kabisa.

Ninaomba jambo hili liingie kwenye kumbukumbu kwa sababu ya muda, lakini ninaamini, Waheshimiwa Wabunge wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, ambaye aliongoza Kamati hii ya Spika, Mheshimiwa Andrew Chenge na Wabunge wengine, watafanya kazi ya Kibunge kwa pamoja ya kuisimamia Serikali. Badala ya sisi Wabunge kulalamika na badala ya Kamati kulalamika kwamba, Serikali haitekelezi mapendekezo ya Kamati, basi mapendekezo hayo ya Kamati, Bunge liisimamie Serikali yatekelezwe. Safari hii tupunguze gherama za maisha badala ya kila siku kuongeza kodi katika maeneo ambayo yanaongeza ugumu wa maisha kwa Watanzania maskini.

Mheshimiwa Spika, nilitarajia safari hii tuletewe Muswada wa Sheria ya Fedha, ajali za bodaboda zimekithiri, kuondoa kodi kwenye kofia za bodaboda ili Wananchi wapate kofia za bodaboda kwa gharama nafuu tupunguze ajali. Nilitarajia safari hii Serikali italeta Sheria ya kuondoa kodi na kupunguza kodi kwenye vifaa vya uzalishaji wa maji ili kupunguza gharama za uchimbaji wa visima, kupunguza gharama za Miradi ya Maji na kupunguza gharama za kuhakikisha Wananchi wanapata huduma ya maji. Mapendekezo haya hayapo kwenye mapendekezo. Nilitarajia safari hii Serikali baada ya kuahidi mara nydingi, italeta pendekezo la kuondoa kodi katika uuzaaji wa nyumba za gharama nafuu ili Watanzania wanunue nyumba kwa gharama nafuu za National Housing na nyumba nydingine za umma. Ukipitia Miswada hii ya Sheria, Muswada wa kwanza na wa pili, yote haina mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba, pamoja na kazi nzuri sana iliyofanywa na Kamati, bado tuna nafasi kwa mujibu wa ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka marekebisho yafanyike. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Haya ahsante, lakini zingatia Kifungu cha 109(2).

Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, nikiamini kuna baadhi ya mambo naona yanahu su vijana na yale ambayo waliji-commit kwenye Bunge lako Tukufu mbele yako Mheshimiwa Spika, wakati nakamata shilingi, yatapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hii asilimia 17 ya kodi ya bidhaa za simu, ambapo asilimia 2.5 inaenda katika Mfuko wa Elimu ya Juu kwa ajili ya kusaidia mikopo ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, hilo naliunga mkono nikiamini vijana wengi hasa amba wanatoka katika familia maskini kule vijijini, wanaopata fursa ya kuijunga na Elimu ya Juu, watapata mikopo. Sasa tuna chanzo maalum kwa ajili ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, uzuri wa chanzo hiki, hata kukiwa na ongezeko la wanafunzi mwaka hadi mwaka, Serikali haitakuwa na mzigo mkubwa wa kufikiria gharama kubwa kwa ajili ya kutafuta fedha za Mikopo ya Elimu ya Juu, itakachofikiria ni kuongezea, kwa sababu tayari kuna chanzo maalum. Naliunga mkono hilo asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna asilimia 17, wakati nikichangia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, nilizungumzia suala zima la Mfuko wa Vijana kwa ajili ya kuwasaidia vijana ili wajajiri wenyewe. Ninapozungumzia hili, natambua changamoto ya ajira ya vijana wenzangu, amba mimi ni wapiga kura wangu kama wengine mna Majimbo yenu.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe nilikubali kurudisha shilingi, kwa sababu Naibu Waziri alisema kutakuwa na utaratibu maalum. Baada ya kupitia Muswada, nimeona fedha hizi, asilimia 2.5 zinaenda kwa ajili ya mikopo ya juu. Kwa nini msitoe asilimia nydingine zikaenda katika Mfuko wa Vijana kwa ajili ya kuwakopesha vijana?

Leo hii tunazungumzia Mifuko ya Vijana na Akina Mama katika wilaya yetu, fedha haziendi na changamoto kubwa ni upatikanaji wa fedha. Mbali na kwamba, kila mwaka tunaongeza bajeti katika Wizara ya Vijana, lakini fedha haziendi kutokana na sungura mdogo ambaye hanenepi. Sasa mmetafuta chanzo cha fedha, asilimia 2.5 inaenda kwa ajili ya mikopo ya Elimu ya Juu; kwa nini asilimia 2.5 nyine nyingine isiende katika Mfuko wa Vijana ili tuwe na uhakika a hundred percent vijana watapata mikopo kuliko na ahadi hewa?

Leo hii kwanza, nashukuru Waziri amesema mmetuongezea bilioni mbili, lakini nina uhakika kwa sababu hazipo katika *ring-faced*, hizi fedha hazitakuja. Hii ni kwa sababu nina experience hiyo, miaka minne ndani ya Bunge nikizungumzia suala moja. Leo mmetafuta chanzo, asilimia 2.5 inakwenda katika elimu ya juu; kwa nini asilimia 2.5 nyine msipeleke katika Mfuko wa Vijana ili vijana wawe na uhakika wa kupata mikopo?

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ulinibembeleza nikarudisha shilingi, ukasema tusubiri *Finance Bill*, ndiyo hii sioni, naona katika upande mmoja tu. Mimi naunga mkono hii hoja, lakini naomba Mheshimiwa Waziri nendeni mkajifungie, asilimia 2.5 nyine iende katika Mfuko wa Vijana na wao wapate mikopo. Kila siku tumechoka kusimama hapa tunapewa ahadi halafu hakuna, hata mwezi haujaisha Naibu Waziri ameji-commit, leo hii hakuna, kuna eneo moja tu. Kwa hiyo, mimi naomba, vijana wana tatizo la ajira na wala *mindset* siyo kwamba wanajua eti fedha zipo tu Serikalini watapata, hapana. Kwa sababu ya ukosefu wa ajira, wapo vijana graduate wamemaliza wanataka ku-invest hawana mitaji. Kwa hiyo, hizi fedha ndizo zitakazowasaki hata na wale ambao wanafanya biashara ndogondogo. Ninaomba majibu katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naipongeza Serikali kwa kuja na *idea* ya kutoa adhabu na faini kwa wale wote watakaogundulika na bidhaa feki. Taifa letu limekuwa likipata matatizo, kuna watu wamekuwa wakidhurika kutokana na watu wanaouza bidhaa feki. Hii mimi naiunga mkono na tena naungana na Kamati kwamba, kuwekwe kiwango maalum cha faini pamoja na adhabu ya kutumikia kifungo kama ambavyo Kamati imesema.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naunga mkono kuondoa kwa ushuru kwenye bidhaa kama *laptop* pamoja na balskeli ambazo ndiyo usafiri wa Watanzania walio wengi vijiji. Ni jambo zuri kwa Serikali kuangalia masilahi ya Wananchi.

Ningepata ufanuzi katika suala zima la kodi ya mafuta, nilidhani Mheshimiwa Waziri alikuwa na dhamira njema kwamba, eneo hili kwenye kodi ya petrol ndiko fedha nydingi zinapotea na ndiko kwenye mianya ya rushwa. Nampongeza Waziri, inahitaji uzalendo kusema nijivue mamlaka ya kutoa msamaha wa kodi. Huyu ni Waziri wa kwanza kumwona na mimi kwa kweli niwapongeze, mmeonesha uzalendo wa hali ya juu. (*Makofii*)

Baada ya kusikia mchango wa babu yangu hapa, naona kuna haja ili kusije kukaleta madhara kwa upande mwingine kwa Watanzania maisha kupanda kutokana na kuwepo kodi kwenye mafuta. Dhamira ya Serikali naiona ni nzuri kwamba, lazima pia mtafute ni vitu gani ambavyo mnawenza mkafanya ili tuondokane na mzigo wa kuwepo misamaha ya kodi kwenye madini na kwenye mafuta. Ninaamini kwamba wanaofanya biashara hii wana uwezo wa kulipa kodi. Kwa hiyo, cha msingi tuangalie pande zote mbili kusiwe na athari; kusiwe na athari kwa Wananchi kutokana na kufuta huu msamaha na vilevile tuangalie ni mianya gani ya rushwa. Hapa kuna challenge ya Waziri kupima nani amfutie msamaha wa kodi na nani amwachie. Kwa kweli ni challenge kubwa hata mimi ningejivua. Sasa kujivua pia siyo solution, lazima mkae na wadau muangalie njia gani mwafaka ya kwenda ili Wananchi wasipate madhara kutokana na hiki ambacho Serikali mmeamua kutuletea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuhakikisha wanaongeza mtaji kwa wawekezaji wa nje kutoka USD 300,000 mpaka 500,000. Hii tutaepukana na wawekezaji wanaokuja na *briefcase* hapa na kututapeli. Kwa hiyo, naunga mkono jambo hili, lakini pia nina-support kuacha hiki kiwango cha 100,000 kwa ajili ya kuwashamasisha wawekezaji wa ndani. Jambo hili ni jema na ninali-support asilimia mia moja. (*Makofii*)

Vilevile katika suala zima la kuondoa kodi kwenye makampuni ya simu, ni mionganoni mwa makampuni ambayo yamekuwa yakinata faida na yamekuwa yakiachiwa misamaha ya kodi bila sababu za msingi. Naunga mkono kuondoa msamaha wa kodi kwenye minara, kwa sababu bado nchi yetu ina tatizo la kutokuwa na wigo mpana wa mawasiliano hasa maeneo ya mijini. Naamini msamaha huu utasaidia maeneo ya mikoa mbalimbali na hasa vijijini, kuhakikisha kwamba, wanapata mawasiliano na n chi yetu inaendelea kutanuka katika Sekta ya Mawasiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri, ningependa utoe ufanuzi, mwaka jana tuliondoa kodi ya bodaboda kwa vijana, ambao ni wapiga kura wangu mimi. Leo hii kuna maeneo mengine wanatozwa shilingi 200. Hawa watu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu na wajiatatufua kipato na tunajua zile bodaboda siyo zao. Sasa je, ni nani mkubwa hapa Halmashuri au Bunge ambalo limesema kodi kwa vijana wanaoendesha bodaboda ziondolewe?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi nilikuwa sijajiandaa vizuri, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ungejiaandaa ingekuwaje? Ninadhani kodi walisema ile ya kulipa *afront*, nadhani ndiyo hasa iliyokuwa inasumbua.

Mheshimiwa Hamad Rashid, atafuatiwa na Mheshimiwa Betty Machangu na Mheshimiwa Mustapha Akunaay.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami niungane na wenzangu, kumpongeza Waziri, Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa Hotuba zao nzuri, zinahitaji kufanyiwa kazi. Nina maoni yafuatayo naomba niyaelekeze:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, naishukuru sana Serikali kwa kukubali kuwa *engaged* vizuri na Kamati ya Bajeti na kwa kina kabisa tukaupitia Muswada, tukauchambua kwa pamoja, kwa mashirikiano makubwa. Naamini kabisa, tutakapokuwa na *Budget Act* mbele ya safari, kazi hiyo itafanya vizuri zaidi na kwa ufanisi zaidi na matunda ya kazi ya Bunge hili yatakuwa yanaonekana. Naomba nikushukuru sana kwa kuanzisha Kamati ya Bajeti, ambayo sasa inaonekana matunda yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, niishukuru vilevile Serikali kwa kukubali maeneo muhimu sana ya kuweza kuyafanya kazi na kukuza uchumi wetu. Area hii ya *soft drink* ambayo Serikali imekubali ushauri wa Kamati, madhumuni yake makubwa hasa ni kuvisaidia hivi viwanda viweze kukua.

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo nataka tuelekeze katika Serikali, ni sera ya kulinda viwanda vyetu vya ndani. Hatujakuwa na sera nzuri ya kusimamia ulinzi wa viwanda vyetu vya ndani na ndiyo maana kila wakati, tunakuja zaidi na *measures* za kodi lakini hakuna sera na mkakati hasa kuona hivi viwanda tunavilinda vipi na *vita-survive* vipi na *vitashindana* vipi katika soko na hatimaye viweze kutoa ajira zinazokubalika.

Kwa hiyo, tumekuwa na hizi hatua za kifedha, yaani za kikodi, lakini ile sera proper hasa za kulinda viwanda hakuna na ndiyo maana bado leo tuna tatizo la uagizaji wa sukari, viwanda vyetu bado havijatoa sukari ya kutosha. Ukienda kwenye viwanda vingine vya vinywaji vilevile vinakufa, vya nguo vinakufa, bado hatujakuwa na sera nzuri za kulinda. Naiomba Serikali ije na sera nzuri sana ya kulinda viwanda vyetu vya ndani ili tuingie kwenye soko la ushindani na tutumie Soko la Afrika Mashariki vizuri zaidi. Hilo ndiyo ombi langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, nashukuru katika Sheria hii tumekubaliana kwamba, wawekezaji wa ndani na wa nje, watakuwa na tofauti kubwa. Vilevile tunahitaji kutofautisha kitu kimoja; kwa mfano, mwekezaji anakuja na dola milioni 500, utaweza kumlinganisha na mwekezaji anayekuja na dola milioni 20? Kwa hiyo, *treatment* yake lazima iwe tofauti. Huwezi huyu ukaja kumpangisha foleni siku tatu hajapata kibali au miezi miwili hajapata kibali ukafikiri atakaa, hawezi kukaa. Hizi ndiyo *investments* ambazo tunazitafuta, ambazo zitakuza uchumi wetu kwa haraka na opportunity hiyo ipo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano; Mheshimiwa Mbatia ameligusia na Kamati yetu imeligusia sana suala la deep sea. Juzi Waziri alizungumza vizuri akanisifusifu kidogo, lakini bado sijaridhika na sijaridhika kwa sababu moja ya msingi. Ukitosha Sheria ya leo ya Deep Sea, hii Sheria iliyopo hivi sasa, ikisimamiwa vizuri yenye we inaingiza mapato. Kwa hiyo, huhitaji utafiti wala taaluma yoyote ni kuisimamia sharia. Sheria inasemaje?

Sheria inasema, meli yoyote inayokuja kufanya *registration* inalipa kwanza *registration fee*. Ikihamaliza inatakiwa kila mwezi ipige *report* kwenye bandari za Tanzania ama ya Dare es Salaam, Zanzibar, Mtwara, Tanga na kadhalika. Isipofanya hivyo ni dola milioni moja faini. Sheria toka 1998 imepitishwa, hakuna hata meli moja iliyopigwa faini na hakuna hata meli moja *ime-report* kwenye bandari; ni usimamizi wa sheria tu! (Makofii)

Kwa hiyo, ukichukua average ya meli 50 zinakuja hapa kuvua zikapewa leseni zikaondoka bila kupiga *report* ni faini. Ukienda kwenye Convention ya *Law of The Sea*, zinatakiwa kama wameshindwa kuikamata waambie wale ambaao ni nchi yao kwamba meli yenu imeingia katika nchi yangu na haikufanya hiki na hiki, zinachukuliwa hatua; hakuna! Kwa hiyo, usimamizi wa sheria ndiyo tatizo. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, meli ambazo ziko pale bandarini zinazovua prones, hawa samaki kwanza watu wamekwambia kwamba, hawa hivi sasa wataondoka. Samaki wenye we ni mobile, investors wenye we ni mobile, kwa hiyo, hakuna investor anayekuja ku-*invest* kwenye *Tanzania Investment Centre*. Anachukua leseni akijua miezi mitatu atavua ataondoka, kwa sababu na samaki lazima wawafuate wanakwenda mkondo gani hawakai. Kwa hiyo, anayekwambia kwamba lazima investor aje a-*invest*, no, anakudanganya! Hakuna dunia nzima, wataalamu wamekwambia hakuna nchi ambayo inatoza *royalty*, ni kweli kwa sababu wenzetu wamejitayarisha namna ya kulinda rasilimali zao.

Namibia wamejenga viwanda vya samaki. Namibia wamehakikisha kwamba. meli ya nje inapokuja. 50% ni Serikali na Wafanyakazi ni lazima 50% watoke Namibia. Kuna haja tena ya kutoza *royalty*? Huna! Ukienda Sierra Leone ni hivyo hivyo, ukienda Maldives ni hivyo hivyo. Sisi kwa sababu hatukuitayarisha katika kuchuma rasilimali zetu, ndiyo maana meli zinachukua samaki zinaondoka. Are *licensing them to loot*? Sawasawa na mtu unampa leseni ya mgodi achimbe, kwa sababu wewe huna kiwanda cha kusafisha dhahabu basi achukue dhahabu? Akili ya wapi?

Sheria ya 2003, *Fisheries Act* inasema hivi; chombo chochote cha uvuvi kikiwa cha ndani ya nchi, kinatakiwa kitozwe dola 2.4 ya gross weight ya meli yake. Cha nje dola 108, ikiwa

kitakuja kwenye bandari, hakiji kwenye bandari dola 106; sheria ipo! Haitaki utafiti sheria ipo, go and read these lectures na zote nimezi-forward kwenu; is paining!

Wanasema kama meli hizi 26 zilizoko bandarini ingekuwa 13 zinavua ni dola 64 milioni zinapatikana. *The laws are there, haitaki utafiti.* Hizi ninazokuletea zote ninazozi-forward ni tafiti za Watanzania. Tafiti zao ndiyo ninazozisoma, sisomi nyingine na report za FAO na kadhalika, *that is all.* Hizi ni pesa za bure, tunakuja hapa tunang'ang'ania kwenye bia na kadhalika, kuna mapato kwenye non tax revenue areas. Ukienda kwenye misitu hali ni hiyohiyo, ukienda kwenye ngozi hali ni hiyohiyo, ukienda kwenye wanyamapor hali ni hiyohiyo, ukienda kwenye utalii hali ni hiyohiyo!

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano mwengine; wenzetu wanafanya sports fishing. *Sport fishing* kwa Marekani inaingiza 30 billion. Maldives, sport fishing ukiingia kwenye boti kwa saa tano unalipa dola 2,000. 2,000 dollars five hours kwenye sport fishing. Hapa wenzetu wa Kenya wanakuja kufanya sport fishing kwenye Pemba channel, tupo hapa tunatazama. Hayataki stadi kubwa, yanataka watu kudhamiria kutumia sheria tulizonazo na taratibu tulizonazo ili tuweze kuvua haya mafuno makubwa.

Mheshimiwa Spika, baya zaidi, tani 2500 za samaki zilizopo zinajulikana kwenye Ziwa Victoria na sehemu nyingine. Kwenye Ukanda wa Bahari hatujui resources tulizonazo mpaka leo! We don't know the resources zilizopo, hakuna research iliyofanywa, hakuna sensa ya Samaki iliyofanywa mpaka leo! Matokeo yake, kwenye GDP ya 1.2% basi 75% inatokana na uvuvi wa maziwa, kwenye bahari yote hii tuliyonayo 25%; akili gani hii? What are we doing?

Tunakuja hapa ndiyo tunagombana, mfanyakazi unampunguzia asilimia moja na kadhalika, hizi resources funaziacha bure. Hawa wafanyakazi tungerudi na 5% wacha 10%, we could do that! Ng'ombe tulionao, viwanda vya Kenya vinafanya kazi, viwanda vyetu havifanyi kazi. (Makofisi)

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana, nashukuru sana ulipoanzisha hii Kamati ya Bajeti, tumejifunza vitu vingi sana, tunahitaji kusimamia non tax revenue area tupate kodi ya uhakika na kodi zipo. Ukienda kwenye misitu, ukienda kwenye utalii, ukienda kwenye wanyamapor, kuna a lot of money hazijakuwa collected. Nawaomba sana, Afisa Masuuli na Wizara, Sectoral Ministries, zisimamie jambo hili na Kamati za Kisika za Bunge zisimamie watu wakusanye mapatoya Serikali ili wafanyakazi wapate mishahara mizuri, Serikali ipate rasilimali za kujenga miundombinu na ili investors waendelee ku-invest katika nchi yetu. Bila ya hiyo tutapiga kelele tu hapa, tutaendelea na soda na vibiriti hatutamaliza.

*Let us go kwenye non tax revenue, kuna a lot of money hazijakuwa collected, only ten percent ndiyo inachangia kwenye kodi; siyo sahihi hata kidogo!* Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali na sisi Wabunge wenye katika maeneo yetu, tusimamie non tax revenue zikusanywe na zitumike vizuri. Hayo mambo mawili ni lazima tuyafanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. (Makofisi)

**SPIKA:** Ahsante. Kamati ya Bajeti inatakiwa ifuatilie on a daily basis katika maeneo hayo. Mheshimiwa Betty Machangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mustapha Akunaay.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Jamani ninavyotaja mimi ni hiari yangu, isipokuwa ninawaweka hapa wasiondoke wajue kwamba wamo; ndiyo hivyo. Haya Mheshimiwa Betty. (Kicheko)

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba nitoe pongezi kwa Kamati ya Bajeti, wamefanya kazi vizuri. Pia timu iliyopo Serikalini ya Wizara ya Fedha ni nzuri na makini, nina imani haya yaliyosemwa yatafanyika. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ninaomba ni-comment very briefly kwenye mambo matatu; jambo la kwanza, kwenye Kifungu cha 16(6)(a), Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya ushuru wa bidhaa wa 0.5%, uliokuwa unatozwa kwenye huduma ya uhaulishaji wa fedha (*money transfer*) na sasa hivi wanataka kutoza 10% kwa ile ada ambayo inalipwa.

Mheshimiwa Spika, hofu yangu kubwa ni kwamba, hii tozo itakuwa *indirectly transferred to customers*. Sasa naiomba Serikali kwamba, sasa hivi M-Pesa na Tigo Pesa ni mkombozi kwa Wananchi wa Tanzania, hata yule mtu mdogo kabisa. Wengine wanafanya ni benki zao. Hii tozo ikirudishwa kwao itakuwa ni matatizo makubwa kabisa. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ifuatilie ni namna gani hizi benki hazitaongeza hiyo tozo ya akina M-Pesa na Tigo Pesa kwa ajili ya kumsaidia Mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la pili nilikuwa nataka ni-comment kuhusu Sura ya 403 inayohusu msamaha wa kodi kwenye Kampuni za Simu. Mwaka jana tuliweka kodi kwenye Sim-card, ilikuwa ni matatizo na kelele nyngi kweli kutoka kwa Wananchi. Hii tunayoifanya ya kuondoa kodi kwenye Kampuni za Simu itakuwa ni vilevile.

Mheshimiwa Spika, siyo si-support kwamba waendelee kupewa exemption, hapana, ni vizuri kabisa tulivyofanya. Serikali iangalie ni namna gani itatusaidia kwa sababu hii kodi waliyoondolewa hapa maana yake ni kwamba, itarudi kwa mlaji na kama itarudi kwa mlaji, ninakwambia hata message siku nyngine zitakuwa vigumu kutuma. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iangalie itasaidiaje. Kuanzia mwaka huu wa fedha Serikali inaweza ikahamasisha makampuni mengine mengi yakaja.

Mahali kama Uingereza au Amerika, unachagua mtando gani unakupa units nyngi kwenye vocha ununua hiyo vocha yake. Kwa hiyo, na hapa pengine tuweke makampuni mengi zaidi kwa mtazamo kwamba competition ikiwa kubwa na rates zitapungua.

Mheshimiwa Spika, kifungu kingine cha mwisho ninachotaka ku-comment ni cha 147, ambacho Mheshimiwa Waziri amesema juu ya kutengeneza bidhaa zinazotakiwa kutozwa ushuru wa bidhaa bila kibali cha mamlaka husika. Katika kifungu hiki, Serikali imekuja na pendekezo kwamba, mtuhumiwa afungwe si chini ya miaka mitatu au aliye faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni tano ama vyote kwa pamoja, na kwa mtu atakayetenda kwa mara nyngine, afungwe miaka mitano na aliye faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni kumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ika-comment kwamba, inaona kama hivi iliyosemwa na Serikali siyo sawa. Kamati ikapendekeza kuwepo na ukomo katika viwango vya miaka ya kifungu na faini ili kutokumpa Hakimu wigo mpana wa kufanya maamuzi. Hivyo, Kamati imependekeza kuwepo na maneno "isiyozidi miaka" na "isiyozidi shilingi."

Mhesimiwa Spika, ninaona Serikali ilikuwa sawa, kwa sababu nafikiria tukisema "isiyozidi miaka" jinsi ambavyo hatujaweza kuikomesha rushwa tuliyonayo, kama mtu alikuwa afungwe miaka mitano, anaweza akatoa rushwa akafungwa miezi Sita. Kwa hiyo, ninadhani twende na hii ya Serikali kwamba, iwekwe definite years na definite amount of money. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Akunaay!

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nguvu leo nije hapa kuzungumza juu ya hoja iliyopo mbele yetu. Kabla sijaanza kuchangia hoja, ninawatachia Waislam wote Ramadhan njema.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, niwapongeze Kamati ya Bajeti pamoja na Kambi ya Upinzani, kwa utafiti wao na jinsi walivyochambua Sheria hii. Kwa hakika kabisa, Kamati ya Bajeti imefanya kazi kubwa, ninawapongeza sana. Ninaomba wapewe muda wa kutosha katika bajeti inayokuja na wapate resource ya watu watakaowasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie kwa jumla sheria hii ilivyokaa bila kwenda kwenye vifungu. Ninaomba kuzungumzia juu ya Sheria inayohusu Kodi ya Mapato, Sheria inayohusu Uwekezaji na Sheria ya Leseni.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mapato imeendelea kuzungumzia juu ya kodi ya zuio la kukodi ndege. Mheshimiwa Waziri, amesema hapa kwamba, kodi hiyo ikilipwa bila kukatwa nchi ya nje kule inafaidi na ikitatwa hapa tunapata sisi mapato. Mimi sina ubishi juu ya hilo, lakini ninachosema ni kama alivyosema Msemaji wa Upinzani kwamba, athari itakayotokea wakati waendesha biashara wa nchi hii hawana ndege. Nayo ni kwamba, watapandisha bei kwa sababu wao wakati wa mapatano yao hawakuzungumzia juu ya hiyo *withholding tax*. Sasa je, ninyi mliona mapatano yao yamekuwaje?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili katika kodi ya mapato. Kama nilivyozungumza; wale wakubwa katika collection sheria imewekwa na sisi tutapitisha sheria hapa, tunawapa Serikali enforcement itakwenda kuchukua kodi. Sasa ninazungumzia juu ya wale wadogo ambao hawaweki hesabu. Kinachofanyika ni kwamba, TRA wanakwenda wanampa makadirio ya juu ili waweze kum-squeeze. Kwa mfano; mtu ambaye labda kodi yake ni shilingi milioni mbili, wao wanamkadiria shilingi milioni kumi ili aweze kutoa shilingi milioni saba, wanamwambia toa shilingi milioni sita, lakini tunakupa risiti ya shilingi milioni tatu utupe shilingi milioni mbili. Kwa hiyo, imetoka shilingi milioni tano na ye ye ataona ilikuwa shilingi milioni saba ame-save mbili.

Mheshimiwa Spika, ninachozungumzia hapa ni kwamba, iwapo rushwa haitaondokana na watu wa TRA, ukandamizaji utakuwa mkubwa na fedha nyingi sana zinakusanywa lakini haziendi TRA. Kule nje wanachozungumza watu ni kwamba, ya nini kulipa kodi mbona zinaliwa huko acha sisi tule, kama ni posho tunalipana huko huko; ndiyo maana treasury imefilisika, sisi kila siku tunapitisha bajeti lakini haitoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama hazitafanywa taratibu zingine ambazo tutahakikisha watu wetu hapa nchini wanaondokana na tabia za rushwa au kutopenda nchi hii, tutaendelea kupitisha bajeti, lakini haitatosha hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya leseni. Kwa hakika leseni inatolewa kama kibali, lakini inaelekea Serikali yetu (Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa), sasa imebadilisha madhumuni ya leseni badala ya kutumika kama kibali inakuwa ni chanzo cha mapato, maana yake inapigiwa bajeti. Kwa hiyo, watakwendwa Mgambo wa Halmashauri, Polisi, nani na kila mtu, kusaka watu na watu wataondoka mijini na fedha haitapatikana. Sisi tunaomba leseni kiwango chake kiwe kidogo, iwe ni permit, kama ni record kama wanavyosema hapa kwamba, wanataka kuweka kumbukumbu, basi tujue watu wanaangaliwa kiwango gani na siyo kwamba Serikali inapata kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili hiyo, kama ni kutafuta vyanzo vya mapato ina maana sasa kodi ya mapato imetozwa mara mbili, yaani watu wamekuwa *double taxed*, kwa majina tofauti; *income tax* na leseni.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, ninataka kuzungumzia juu ya Sheria ya Uwekezaji (*TIC*). Hapa Serikali imependekeza kwenye sheria kuondoa msamaha ambao hauna tija. Sasa ninashauri kwamba, kweli iwe ni msamaha ambao hauna tija, isije ikawa msamaha unaondolewa katika sehemu ambayo baadaye itatusababishia nchi ishindwe kuwekeza. Hakuna nchi Duniani ambayo imeendelea bila kuwa na uwekezaji. Ninaelewa Waheshimiwa Wabunge wana uchungu juu ya misamaha ambayo imekuwa abused. Nami pia ninakubali.

Vilevile ninaona Wawekezaji ambao wamekuja hapa, wamechukua mikopo kutoka benki mbalimbali, kwa hiyo, na wao wanataka hiyo mikopo ilipwe na wapate faida. Kwa hiyo, tuangalie huko tuna-create jobs maana sisi wenyewe hatuna viwanda na nchi ambayo haina viwanda haitaendelea. Basi waachwe waje watutengenezee viwanda na sisi tuanze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliopo hauwezi kutosha kuwataja wengine, tutaendelea kesho. Sasa nina maelezo ya aina mbili; kwanza kabisa, Muswada wa Fedha ni sehemu ya Bajeti. Kwa hiyo, kutokana na maamuzi yetu wenyewe, tutaendelea kufanya kazi hii kesho ili tumalizie Muswada huu. Kama nilivyosema, Miswada ile mingine tumeiondoa kwa sababu ya kufanya kazi zaidi kuliko kuiharakisha halafu kazi isifanyike vizuri.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(8), ninamwita Mheshimiwa Susan Lyimo!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO – MJUMBE WA UMOJA WA MABUNGE DUNIANI (IPU):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa taarifa kuhusiana na Maadhimisho ya Miaka 125 ya Umoja wa Mabunge Duniani (*Inter Parliamentary Union*).

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Mabunge Dunia (*Inter Parliamentary Union - IPU*) ni Chombo cha Kimataifa cha Mabunge kilichozaa Juni, 1889 huko Ufaransa. *IPU* ni kati ya Taasisi za Kimataifa iliyoanza zamani sana na ilisaidia kuanzhishwa kwa Taasisi nyingine katika ngazi ya Kimataifa (*Intergovernmental Level*), ambayo baadaye ilijulikana kama Umoja wa Mataifa. Vilevile *IPU* ilichangia sana uanzishwaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Hague (*The Permanent Court of Arbitration in the Hague*).

Mheshimiwa Spika, mwezi huu wa Juni, 2014, Umoja huu unaadhimisha miaka 125 toka kuzaliwa kwake. Umoja wa Mabunge Duniani ulianzhishwa kwa *Article of the Statutes of the IPU* na Katiba yake inaelezea ni nani wanapaswa kuwa Wajumbe wa *IPU*, maeneo ya kufanya kazi, malengo yake, makao makuu, muundo wake na vikao vyake. Umoja huu ni kitovu cha mijadala ya Mabunge Duniani na vilevile huimarisha amani, ushirikiano na kuhakikisha uwepo wa demokrasia shirkishi.

Mheshimiwa Spika, kwa muda wote wa uhai wake, *IPU* imejitahidi kufanya yafuatayo:-

- i. Kuratibu na kubadilishana uzoefu kati ya Mabunge na Wabunge Washirika;
- ii. Kushiriki katika masuala yote ya Kimataifa ili kujenga umoja na amani;

- iii. Kusaidia kulinda na kutetea haki za binadamu ambalo ni jambo la msingi katika demokrasia ya Mabunge na maendeleo;
- iv. Kujenga uelewa mzuri wa taasisi zinazowakilishwa, kuboresha na kuendeleza malengo yake; na
- v. Kusaidia juhudhi na kufanya kazi kwa karibu sana na UN ambayo malengo yake yanafanana.

*IPU* pia inashirikiana na Kanda na Mashirika ya Kimataifa ya Kiserikali na Yasiyo ya Kiserikali yenyé malengo ya kufanana.

Mheshimiwa Spika, *IPU* ina Wanachama kutoka nchi 164 Duniani, vilevile ina Mabunge ya Kikanda 10 ambayo ni Wanachama Washiriki (*Associate Members*). Hawa ni pamoja na Bunge la Afrika Mashariki, Bunge la Ulaya, Bunge la Amerika ya Kati, Bunge la Jumuiya ya Uchumi ya Afrika Magharibi (*ECOWAS*), Bunge la Uarabu, Bunge la Afrika na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wajumbe hawa, *IPU* ina hadhi ya uangalizi wa kudumu wa Umoja wa Mataifa na vilevile hadhi ya ushauri kwenye Baraza la Uchumi na Kijamii la Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa utendaji bora wa Bunge letu kuongozwa na Kamati za Kudumu, ni hivyo hivyo kwa *IPU*. *IPU* ina Kamati za Kudumu nne, Kamati za Kawaida nne na Makundi kazi manne, ambayo yote yanasaidia utendaji kazi mzuri wa mikutano yake. Kamati hizi za kudumu ni pamoja na Amani na Usalama wa Kimataifa (*Standing Committee on Peace and International Security*), Maendeleo Endelevu, Fedha na Biashara (*Standing Committee on Sustainable Development, Finance and Trade*) na Mheshimiwa Hamad Rashid ni mmoja wa Wajumbe katika Kamati hii. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, Kamati nyingine ni Demokrasia ya Haki za Binadamu (*Standing Committee on Democracy and Human Rights*) na Mahusiano ya Umoja wa Mataifa (*Standing Committee on United Nations Affairs*).

Mheshimiwa Spika, *IPU* ina wafanyakazi 37 walioko Jeneva na watatu walioko New York. Wajumbe wake hukutana mara mbili kila mwaka na huwa na mada mbalimbali hususan zihusuzo amani, demokrasia, haki za binadamu, maendeleo endelevu, usawa wa kijinsia na utawala bora. Mada kuu huwa zinapendekezwa na Sekretarieti na kipelekwa kwenye Baraza la Uongozi wa *IPU* (*Governing Council*), chini ya Uenyekiti wa Rais wa *IPU*.

Mara zote mada kuu hutokana na jambo linaloonekana kutishia amani, usalama na demokrasia Ulimwenguni, ndiyo maana mwaka huu mada inayopendekezwa ni “Tokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake ili kuleta Usawa wa Kijinsia (*Achieving Gender Equality Ending Violence Against Women*).”

Mheshimiwa Spika, hii itakuwa fursa nzuri sana kwa Wajumbe kutoka Tanzania kueleza hali halisi ya uwakilishi wa Wanawake katika ngazi mbalimbali. Kubwa zaidi ni mchakato wa Katiba Mpya, ambapo rasimu imependekeza uwepo wa 50% kwa 50% katika nafasi ya Ubunge. Jambo ambalo hata Wanawake Wabunge kuitia Chama chao cha TWPG walipendekeza. Kwa mantiki hii, si ajabu Tanzania ikawa nchi ya pili Duniani kwa ushiriki wa Wanawake kwenye Vyombo vyta Uwakilishi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, *IPU* ni Taasisi ya aina yake kwa kuwa siyo ya Kiserikali na wala si ya Kiserikali (*Is not nongovernmental wala intergovernmental*). Hii ni Taasisi inayoundwa na

Wawakilishi wa Wananchi, vilevile ni Taasisi ya kisiasa na tatu ni Taasisi inayotetea demokrasia kupitia Mabunge ya nchi husika.

Mheshimiwa Spika, *IPU* imefanya mambo mengi hasa utetezi wa usawa wa kijinsia. Kwa miaka 50, *IPU* imekuwa ikihamasisha, ikifanya utafiti na kutoa taarifa zinazohusu ushiriki wa Wanawake katika siasa. Hivyo, ukitaka kujua chochote kuhusu quarter jinsi zinavyofanya kazi utapata kupitia *IPU*. Taarifa za *IPU* zimehamasisha nchi nyingi hasa zile za Uarabuni, kuongeza idadi ya Wanawake, mfano nchi kama Tunisia na nyingine nyingi. Hii ni kwa kuwa katika kila Mkutano wa *IPU* ni lazima idadi ya Wanawake Wabunge waliohuduria itangazwe na vilevile mada nyingi kuhusu umuhimu wa Wanawake kushiriki katika siasa hujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, *IPU* imekuwa mstari wa mbele sana katika kutetea Wabunge wanaoshitakiwa, wanaodhalilishwa na mara nyingi Wabunge wa Upinzani huwa wanakumbwa na misukosuko mingi sana. Hivyo, *IPU* huwatembelea Magerezani na kujadili na wahusika kuhusu kuachiwa kwao huru. Pia *IPU* hujitahidi kuhakikisha haki zao zinaheshimika na wanaendelea na kazi zao za uwakilishi wa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, *IPU* kwa kutambua hili, ilianzisha Kamati inayohusika na Haki za Wabunge (*Committee on Human Rights of Parliamentarians*) Mwaka 1976. Kamati hii imeshughulikia mashauri katika nchi 100 na kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa. Hii ni pamoja na kuwaondoa kifungoni, kurudishiwa Ubunge wao, kulipwa haki zao (fidia) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo yanayowasibu Wabunge hao ni pamoja utekwaji, kutoheshimu haki na kinga za Mabunge, uteswaji, ushambuliaji (*attacks*), tishio la kuuawa, mauaji, kupotezwa, kuwekwa kizuzini na mengine mengi. *IPU* imetembelea Wabunge walioko vifungoni nchini Burundi, Zimbabwe, Myanmar na sehemu nyingine nyingi.

Maeneo yenye matatizo makubwa ya ukiukwaji wa haki za Wabunge ni Asia (51.8%), Afrika (26.8%), Marekani ya Kati na Kusini (11.8%), Ocenia (5%) na Ulaya (4.6%).

Mheshimiwa Spika, *IPU* imekuwa ikisaidia Mabunge katika nchi mbalimbali ili kuwa makini, kuwajibika na kuwa wawakilishi bora wa Wananchi. Kwa mfano, katika nchi zinazofanya mabadiliko ya kiutawala kama Peru na Myanmar, *IPU* ilikuwa taasisi ya kwanza kwenda kusaidia Mabunge yao katika mchakato wa demokrasia kwa kutengeneza mpango mkakati wa jinsi gani Bunge litakuwa la kidemokrasia.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania *IPU* imefanya programu mbalimbali; kwa mfano, mwaka 2007 Brusel's Program of Action ambapo walieleza jinsi gani nchi za LDC (Least Developed Countries), zitatekeleza mpango huu. Mwaka 2008 *IPU Committee on UN Affairs* ilifika Tanzania kuangalia jinsi Umoja wa Mataifa unavyofanya mabadiliko na kutathmini namna bora ambayo Mabunge yanaweza kushirikiana na UN katika kusaidia mkakati wa kupokea kwa pamoja (*delivery as one*) Kitaifa na Kimataifa. Vilevile mwaka 2012 *IPU* ilifanya semina kwa baadhi ya wadau wa masuala ya jinsia kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na jinsi gani tunaweza kupunguza tatizo la unyanyasaji wa kijinsia (*Stop Violence Against Women*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunajivunia uwepo wa Taasisi hii kubwa Duniani kwa kazi kubwa inayofanya ya kuhakikisha Mabunge yanakuwa chombo imara cha uwakilishi wa Wananchi na kwamba, yanasmama ipasavyo. Inawezekana wengi wetu hatufahamu umuhimu wa Taasisi hii kutokana na hali ya amani iliyopo nchini kwani ni nadra kusikia Mbunge ametekwa au kupotezwa. Kwa nchi zilizokumbwa na haya wanaelewa umuhimu wa chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema mwaka huu ni muhimu sana kwa Waafrika kwani tarehe 13 Machi, 2014 katika Historia ya IPU, Mwafrika wa kwanza, Martin Chungong kutoka Cameroon, alichaguliwa kuwa Mtendaji Mkoo wa Umoja huu. Hivyo, wakati tunaadhimisha miaka 125 tokea kuzaliwa kwake, vilevile tunashangilia ushindi wa mwenzetu katika nafasi hii nyeti ya Kimataifa. Hii ni kwa kuwa kwa kipindi cha miaka 125 nafasi hii ilikuwa ikishikiliwa na wenzetu kutoka Bara la Ulaya pekee; (Ufaransa (1), Italia (1), Sweden (1), Norway (1) na Switzerland (4). Kwa hiyo, tunaona kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 125 tunapata Mwafrika wa kwanza kuwa Katibu Mkoo wa IPU.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa, IPU inafanya kazi nzuri sana na Mabunge ya nchi mbalimbali Duniani na mifano michache imeelezwa hapa juu. Ni ukweli kuwa bado Wabunge na Watanzania wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu Taasisi hii muhimu na hali hii inatokana na kutokuwa na mrejesho katika Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ili inapota taarifa yake basi na taarifa ya IPU iwemo.

Mheshimiwa Spika, bado ushiriki wa Wajumbe wako ni dhaifu au hafifu kwani mbali na kushiriki vikao viwili vyta kikanuni (mwezi wa Tatu na wa Kumi), vipo vikao vingi ambavyo hawahudhuri kutokana na tatizo la kifedha. Mfano ni Vikao vyta Wanawake, vile vyta UN Affairs na hata vyta fedha. Katika hali hii Tanzania haiwakilishi ipasavyo; hivyo, kukosa mwendelezo (*continuity*). Ni rai yetu kwamba, jambo hili litapatiwa ufumbuzi ili Tanzania iendelee kupata sifa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kipekee, ninakushukuru sana wewe binafsi, kwa kuhakikisha ada ya Uanachama wa Bunge letu inalipwa kwa wakati na hivyo kutokuwa mionganii mwa wadeni kama ilivyo kwa baadhi ya nchi Wanachama wanavyoshindwa na hata wengine kusimamishwa Uanachama. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wajumbe wote wa IPU kwa ushirikiano mkubwa tunaoonesha hasa pale zinapotokea nafasi Tanzania huombwa kusaidia ufanisi wa kampeni na mara zote tumekuwa tukihakikisha ushindi. Mfano ni huu wa Ndugu Martin, ambapo Wajumbe wote wa Tanzania walifanya uhamasishaji mkubwa na kampeni. Wajumbe hao ni pamoja na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe na mimi mwenyewe Mheshimiwa Susan Lyimo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, ninamshukuru sana Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuwezesha Wajumbe katika kutekeleza majukumu yao ya Kimataifa. Vilevile tunamshukuru sana Katibu wa Dawati la IPU hapa Bungeni, Ndugu James Warburg, kwa ushirikiano mkubwa anaotupatia katika mikutano yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi, naomba kuwasilisha. Mungu ibariki IPU, Mungu libariki Bunge letu. Nawashukuruni sana kwa kunisikiliza, ahsante sana. (Makofii)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema, IPU kama ilivyo CPA, ni vyombo vyta siku nyngi sana. Vilianzishwa kwa mazingira tofauti, lakini sasa hivi IPU imechukua hata nafasi ya uangalizi katika Umoja wa Mataifa. Wanashirikiana sana na Umoja wa Mataifa katika mambo mengi hasa yanayohusu haki za binadamu. Kwa hiyo, katika chombo hicho mtaona kwa utaratibu wake ni Spika anayeteua watu, hampigi kura kama vile vyombo vingine.

Kwa sababu hiyo, kwa sababu kuna complex nyngi, inawezekana mikutano sita au saba inafanyika kwa pamoja, kwa hiyo, tumejaribu kujenga continuity. Continuity hii imefanywa vizuri sana na Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Hamad Rashid. Wengine tunaowa-train

ni akina Mheshimiwa Dkt. Kikwembe na wakati fulani alikuwa na Mheshimiwa Angellah Kairuki. Wako active kwa sababu lazima utumie na mitandao kujua mukutano gani unafanyika wapi. Delegation ya Tanzania wamekuwa very active na wanajulikana pale uwepo wao na *impact* yetu huwa inaonekana moja kwa moja. (Makofij)

Kama alivyosema Mheshimiwa Susan Lyimo, IPU huwa inakutana mara mbili kwa mwaka katika nchi mbalimbali. Hivi sasa nadhani Mheshimiwa Hamad Rashid anakwenda New York kwenye *sustainable development* kesho kutwa kwa sababu ni kikao cha IPU. IPU ina ofisi yake Geneva lakini ofisi ndogo iko New York.

Mimi ndiye niliyewasilisha ombi la kuingia katika Bunge lile la Umoja wa Mataifa na nilitoa Hotuba ya Kwanza ya IPU kama *observer status* katika ya IPU miaka kama kumi iliyopita. (Makofij)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kama nilivyo sema, kesho tutaendelea na michango ya hii Hotuba. Mategemeo yetu inaweza kuisha kesho na Bunge linategemewa kumalizika kesho.

Ninaomba nitangaze kwamba, Mheshimiwa Mabumba anasema, baada ya kuahirisha Bunge kesho, Wanachama wanaojihusisha na Wanyamapori watakuwa na semina yao. Semina hiyo itakuwa katika Ukumbi wa Msekwa, kesho baada ya kuahirisha kikao hiki.

Kwa hiyo, wale watakaojiandaa kesho, wengine siwajui, nafikiri nitawataja pale pale kuna watu hawaonekani sana. Nitawataja kesho, wale wote walioomba wafike hapa.

Ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.43 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 28 Juni, 2014 Saa Tatu Asubuhi)